

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 2 Julai, 2009

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri Miundombinu kuwasilisha Hati, napenda mtambue kurejea kwa Mheshimiwa Naibu Spika, ambaye hatukuwa naye kwa wiki moja alikuwa na udhuru kule nyumbani Njombe. Karibu sana Mheshimiwa Naibu Spika kila mara tunategemea sana uzoefu wako katika shughuli za hapa ndani na mimi nimefarijika sana ahsante. (*Makofi*)

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Juu ya Uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania uliofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India.

Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya Utendaji wa Kazi usioridhisha, wa Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)*.

Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Juu ya Uuzwaji wa Nyumba za Serikali.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Randama za Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri Mkuu ametua dakika tano zilizopita pale kiwanja cha ndege Dodoma alikuwa na safari ndefu kutohana Musoma, lakini nusu saa yake iko pale pale. Kwa hiyo, Katibu hatua inayofuata. (*Kicheko*)

MASWALI YA KAWAIDA

SPIKA: Kwa hiyo, tutaanza na maswali ya kawida wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa njiani kuja hapa ukumbini.

Na. 148

Mikopo ya Wajasiriamali na Vikundi vyat Jamii

MHE. KHERI KHATIBU AMEIR aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa na utaratibu wa kutoa fedha nyingi kusaidia miradi ya wajasiriamali na vikundi nichini kwa dhana ya kujajiri na kujikwamua kwenye janga la umaskini:-

(a) Je, Serikali imefanikiwa kwa kiasi gani katika dhana hiyo hasa kwa miradi ya *MACEMP* kanda ya Pwani ya Tanzania Bara?

(b) Je, ni vikundi vingapi vimeanzishwa mpaka sasa vikiwa na wajasiriamali wangapi na fedha kiasi gani zimeingizwa kwenye Mradi huo tangu ulipoanzishwa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kupambana na umaskini katika jamii za wavuvi ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kwa kuwajengea uwezo wa kuibua na kutekeleza miradi ya jamii ya kiuchumi kuititia Mradi wa *MACEMP*. Mradi huu ulianza kutekelezwa katika wilaya tatu za mfano (*pilot districts*) za Kilwa, Mafia na Rufiji kuanzia Desemba, 2005 hadi Juni, 2008. Kuanzia mwaka 2008/2009 mradi ulianza kutekelezwa pia katika Halmashauri nyingine 13 za Mwambao wa Pwani. Halmashauri hizo ni Mkinga, Muheza, Pangani, Bagamoyo, Lindi vijijini Mtwara Vijijini, Mji wa Lindi, Manispaa za Kinondoni, Ilala Temeke, Mtwara-Mikindani na Jiji la Tanga. Wananchi katika Halmashauri hizo wamevezeshwa kuibua miradi inayohusu fani za uvuvi, ufugaji wa samaki, unenepeshaji wa kaa, kilimo cha mwani ufugaji nyuki uzalishaji wa chumvi, bustani, ufugaji kuku, ususi na utengenezaji wa mashua.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa mradi wa *MACEMP* umewezesha kuanzishwa kwa vikundi 189 ambavyo vimebuni na kutekelezwa miradi 189 yenye thamani ya

shilingi 2,387,933,355. Miradi hiyo ina jumla ya wajasiriamali 3,062 ambapo kati yao, wanawake ni 1,033 na wanaume ni 2,036. Mchanganuo wa miradi hiyo ni; Kilwa miradi 63 yenye jumla ya shilingi 859,061,510, Mafia miradi 43 kiasi cha shilingi 376,185,072, Rufiji miradi 60, kiasi cha shilingi 724,118,395, Halmashauri ya Lindi Mjini ina miradi 6 yenye kiasi cha shilingi 90,319,998 na wilaya ya Bagamoyo miradi 17 yenye thamani ya shilingi 338,248,380.

Miradi hiyo imeanza kutekelezwa baada ya fedha hizo kupelekwa kwenye Halmashauri kupitia *TASAF* na Wizara imeidhinishwa fedha nyingine kiasi cha shilingi 860,900,026 kwa ajili ya kutekeleza miradi 55 mipy. Miradi hiyo ni ya Halmashauri za Bagamoyo (miradi 8, shilingi 152,508,290), Muheza miradi 5 ya shilingi milioni 83,498,550, Mkinga miradi 12 yenye thamani ya shilingi 193,174,450, Pangani (miradi 15, shilingi 209,990,011) na Jiji la Tanga (miradi 15, shilingi 220,758,725). Aidha miradi 191 imeibuliwa na Halmashauri 9 za Mkinga, Muheza, Pangani, Jiji la Tanga, Kinondoni, Mkuranga, Lindi Mjini, Mtwara Vijijini na Mtwara/Mikindani na miradi hiyo ipo katika hatua za kuhakikiwa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri Mkuu ameingia naomba tumpokee kwa makofi kwa sababu sio rahisi kutoka safari ndefu na moja kwa moja kutoka Musoma amekunywa chai Musoma saa hizi tuko naye hapa. Karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu kipindi chako kitaanza saa tatu na nusu. (*Makofi*)

MHE. KHERI KHATIBU AMEIR: Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kati ya miradi hii ambayo imeanzishwa imesita kutokana fedha ambazo walikuwa wamepewa hazikutosha kutokana na baadhi ya vifaa kupanda bei. Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia hao waliokuwa miradi misita kwa sababu hizo wanawasaidia vipi.

Pili kuna baadhi ya miradi iliyoanzishwa kuna waliokuwa wamekimbia miradi hiyo na miradi inaning'inia Mheshimiwa Waziri anayo taarifa hiyo na kama anayo Wizara inachukua hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hivi karibu kuna miradi iliyoanza 2005/2008 na vitu vimeduja kupanda bei sana. Katika hali ya namna hiyo watu wanapokuwa wamepungukiwa na mradi haujamalizika bado mradi unazohela na kama mwaka huu tukipitishiwa Bajeti tutakuwa na dola milioni 2. Katika hali hiyo hatutasita kuwasaidia hela zingine ili waweze kukamilisha mradi, kuhusu kwamba suala la pili kwamba kuna watu wamekimbia miradi taarifa nilizonazo ni kwamba miradi inatekelezwa vizuri na kama watu wamekimbia hizo habari hazijafika ofisini.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, kwa kuwa *MACEMP* unawahuishwa na wilaya ya Pangani, na kumbukumbu nilizokuwa nazo kwamba mpaka sasa zimetolewa milioni kati ya 51 na 57 je, Serikali kwa vile Pangani imepangiwa zaidi ya milioni 200, miradi hii itakwenda kwa miaka mingapi ili tuweze kupata mgao uliobaki kwa sababu waombaji ni wengi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, ni kweli huo mradi umeanza 2005 na utaenda mpaka mwaka 2011 Desemba, na kuna wilaya ambazo zimekuja kuingia humu karibuni na moja wapo ikiwa Pangani. Napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na kuwa kwamba alikuwa anapata hela chache lakini kwa sasa hivi wilaya ya Pangani imeshaibua miradi 15 na ambayo tayari tumeitengea shilingi milioni 219,990,011.

Kwa hiyo wilaya yako ni kwamba wilaya yako itaendelea kupata fedha zaidi kutoka kwa huu mradi na naamini huu sio mwisho wa wilaya ya Pangani kupata hela kwa sababu mwaka huu kama wataibua miradi tunategemea kutumia dola milioni 2 ambazo ni kama shilingi bilioni 2.6. Kwa hiyo wilaya ya Pangani nayo itaendelea kupata fedha namna watakavyoibua miradi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini ningependa niongeze majibu kwa Mheshimiwa Rished Mbunge wa Pangani. Kwamba mradi wa *MACEMP* ambao unahusisha Halmashauri 13 kwa sasa hivi utekelezaji wa miradi yake unategemea sana ushaphu wa wakurugenzi katika Halamshauri hizo kuwasilisha miradi hiyo na kubuni miradi inayotakiwa. Kwa hiyo kila mkurugenzi ambao tuliiingia nao mkataba mwaka jana wa kutekeleza miradi mbalimbali inayohusu *MACEMP* ningeweza na ningeomba nitoe wito kupitia Bunge kwamba wakurugenzi wote wa Halmashauri hizo 13 tulizoingia nazo mkataba, wawe shaphu katika kuleta mikataba na miradi mbalimbali kutoka kwa wananchi wanaowawakilisha ili waweze kuzitumia hizi fedha.

Kwa sababu kwa taarifa tulizonazo sasa fedha ziko nyingi lakini vikundi haviibuliwi kupitia wakurugenzi wanaohusika. Kwa hiyo wakurugenzi watumie wajibu wao katika kufanya kazi ipasavyo, ili kusudi miradi hii ya fedha ambazo zipo ziwe kutumika kikamilifu. Ningewaomba Wabunge wahusika katika Halmashauri hizo wawabane wakurugenzi hao ili wakashindwa Mheshimiwa Waziri Mkuu awachukulie hatua kwa kutotumia fedha za *MACEMP*. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa hiyo ya ziada imetusaidia wote katika majimbo yetu. (*Makofî*)

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, kwa kuwa sekta hiyo ya uvuvi inatabiriwa na changamoto kubwa sana licha ya miradi mingi ambayo imewekwa katika kusaidia wananchi kutoka Serikalini na kutoka kwa wafadhili ambapo changamoto kubwa sana imekuwa ni uvuaji haramu haswa kutumia mabomu. Na kwa kuwa katika nchi yetu zipo kambi nyingi sana za jeshi ambazo ziko katika fukwe katika maeneo ambayo ni pembezoni mwa bahari, lakini kumekuwa na ushirikishwaji mdogo au kutokuwa na mfumo rasmi wa jeshi hili kuweza kusaidia katika yale maeneo ambao yanakuwa matukio ya ulipuaji wa mabomu kama ilivyokuwa kule Tanga.

Je, Seriakali haioni umuhimu sasa kuweza kutumia jeshi hili kusaidia kwa sababu ingawa wana kazi kubwa lakini pia wana muda wa kuweza kusaidia katika maendeleo walau kusaidia katika kulinda rasilimali zetu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:
Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni lazima tukiri kwamba jeshi lake lina shughuli zake ambazo limetengewa.

Lakini mimi ningelipenda kusimama hapa na kulispongeza jeshi letu la wananchi kwa kazi nzuri inayofanya limetusaidia sana katika kupambana na uvuvi haramu tunapolihitaji ila kinachokwu kinaleta saa zingine matatizo ni ufinyu wa Bajeti.

Lakini kama mngekumbuka siku ambayo tumekamata meli kule bahari kuu inavua kwa haramu, jeshi letu likiwa pale na lisisaidia nalo kusaidia katika hali hiyo. Kwa hiyo jeshi letu liko imara na linatusaidia sana. (*Makofi*)

Na. 149

Barabara Inayounganisha Wilaya za Kwimba na Misungwi

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA aliuliza:-

Kwa kuwa, sera ya Miundombinu hususan barabara ni kuunganisha Wilaya kwa Wilaya; na kwa kuwa, barabara ya kutoka Sumve kwenda UKiriguru na barabara ya kutoka Sumve kwenda Misungwi ni mbovu sana na katika maeneo haya hakuna mawasiliano kati ya wilaya ya Kwimba na Misungwi:-

Je, Serikali itatengeneza lini barabara hizo?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuona kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote nchini yanaunganishwa kwa barabara zinazopita muda wote.

Makao Makuu ya Wilaya ya Misungwi na Kwimba tayari yanaunganishwa na barabara ya Ngudu - Jojiro Mabuki hadi Misugwi, zinazohudumiwa na Wizara yangu kupita *TANROADS* Mkoa wa Mwanza. Barabara hizi zinafanyiwa matengenezo kwa kutumia mradi wa *PMMR* na zinapitika.

Barabara za kutoka Sumve kwenda UKiriguru na ile ya kutoka Sumve hadi Misungwi ni barabara za Wilaya zinazohudumiwa na Halmashauri za Wilaya za Misungwi na Kwimba. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ashauriane na Halmashauri

husika ili barabara hizo ziweze kutengewa fedha za matengenezo kupitia fedha za mfuko wa barabara ambazo Halmashauri zote nchini hutengewa na mfuko wa barabara kupitia TAMISEMI.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Serikali yangu napenda kuchukua nafasi hii kushukuru kweli kwamba hii barabara ya Gundu, Jojilo kwenda Misungwi imetengenezwa lakini kutoka Jojilo kwenda Gundu haina hadhi ya kuwa ni barabara ya kwenda Makao Mkuu ya Wilaya.

Lakini pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Mheshimiwa Mbunge ashauriane na Halmashauri yangu. Ni kweli Halmashauri zangu zote mbili nimewasiliana nazo, tumeshauriana nazo lakini kwa kuwa ni Serikali moja na Halmashauri hizo hazina fedha nyingi za kuweza kutengeneza mabarabara tajwa hapo juu. Sasa Serikali Kuu haiwezi kuzisaidia Halmashauri hizi?

Kwa kuwa barabara ya Mondo Misungwi, iliahidiwa kupewa milioni 60 lakini hazijatoka kwa ajili matengenezo ya hiyo barabara. Je, Serikali inanieleza nini kuhusu matengenezo ya barabara hii?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizi zinazotengwa kwenye Halmashauri kutokana na mahitaji makubwa zilizoko kule kwenye Halmashauri fedha zinakuwa hazitoshi kutengeneza barabara hizo zote.

Lakini kama nilivyosema ni suala tu la kupanga mipango kuona kwamba kipaumbele ni kipi, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati mwingine kunapokuwa kuna umuhimu wa kipekee kabisa Halmashauri imeshindwa kutekeleza utengenezaji wa barabara fulani fulani, uwasiliane na Wizara yangu ambayo kwa kadri uwezekano wa fedha unavyopatikana huweza kutusaidia. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Mbunge aendelee na ushauri mliompa lakini wakati huo huo kama kutakuwa na namna yoyote ambayo naweza kuwasilisha maombi na sisi tunawenza tukayatazama hayo.

Lakini kuhusu hilo la pili la fedha zilizotengwa kati ya barabara ya Mondo kwenda Misungwi ambazo hazijafika, nataka tu nimhakikishie kwamba totalifuatilia tuone ni mahali gani zilizokwama kama zilitengwa ili ziweze zikafikishwa kwenye eneo la utekelezaji wa barabara hiyo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kuongezea majibu mazuri sana ambayo yametolewa na Mheshimiwa Chibulunje Naibu Waziri wa Miundombinu kama ifuatavyo. Hii barabara inayozungumzwa hapa imekuwa inafuatiliwa sana na Mheshimiwa Shibili, na kwa hiyo na figure zake ninazo hapa shilingi milioni 60 zimetengwa kwa ajili ya barabara hii kwa

hiyo asiwe na wasiwasi kabisa nina hakika kwamba hizi hela zitakuwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

MHE. JOSPEHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, naomba kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza, matatizo yaliyoko Misungwi, ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko Kigoma, Kasulu na Kibondo. Je, ni lini barabara hizo zinazounganishwa kwa kiwilaya ambazo ni barabara za wilaya zinazotakiwa kuunganishwa kimkoa zitaunganishwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika wakati wote hizi za ngazi ya wilaya tumesema kwamba kwa sasa hivi tutahakikisha kwamba zinakuwa na uwezo wa kupitisha magari wakati wote kwa kiwango chochote kitakachokuwa kinawezekana hasa changarawe. Sasa ni lini barabara hizo zinazounganisha wilaya zitajengwa kwa kiwango cha lami nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba suala hilo kwa sasa hivi kwa kweli si rahisi kutekelezeka kwa sababu kuna mpango kabambe sasa hivi ambao tunalenga kuunganisha kwanza makao makuu ya mikoa yetu yote nchini kwa kiwango cha lami.

Kazi ambayo kwa kweli tumeifanya kwa kiwango kikubwa na imebakia mikoa hiyo minne ambayo tumeitangaza jana katika hotuba yetu ya Bajeti, kwa maana ya mkoa wa Rukwa, Kigoma, Tabora na Manyara. Kwa hiyo mpaka kazi hiyo itakapokamilika hatua hatua tunaweza tukafika huko kwa kadri ya uwezo wa Serikali kifedha utakaporuhusu.

Na. 150

Ukarabati wa Barabara ya Old-Shinyanga - Salawe

MHE. JACOB D. SHIBILITI - (K.n.y. MHE. AHMED A. SALUM) aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya *Old Shinyanga* - Salawe inashughulikiwa na *TANROADS* na kila mwaka inapata fedha kidogo na kufanya ukarabati wake kuwa mdogo; na kwa kuwa makandarasi wanaopewa kazi ya kuikarabati barabara hiyo hawana uwezo kabisa na hata vitendea kazi vyao havitoshi.

- (a) Je, Serikali haiioni umuhimu wa kuongeza fedha ili matangenezo ya barabara hiyo yafanyike vizuri?
- (b) Je, ni kwanini mkandarasi huyo amepewa kazi hiyo wakati hana uwezo kabisa na hivyo kusababisha ukarabati usio na viwango vyakuridhisha?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ahamed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuongeza fedha za matengenezo ya barabara ya *Old-Shinyanga-Salawekwa* nia ya kuifanyia matengenezo makubwa ili iweze kuititia majira yote ya mwaka.

Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali imeshindwa kutenga fedha inayokidhi mahitaji halisi. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kadri ya bajeti inavyoruhusu.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, zilitumika jumla ya shilingi milioni 137.8 kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya kawaida. Mwaka 2008/2009, Serikali imetenga shilingi milioni 339 kwa ajili ya ukarabati na matengenezo mengine katika barabara hii. Na katika mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali itaendelea kutenga fedha za kuikarabati barabara hii ili iendelee kutengenezwa na kuiwezesha kupitika wakati wote.

(b)Mheshimiwa Spika, kazi za matengenezo ya barabara ya Old Shinyanga - Silawe zimekuwa zikifanywa na makandarasi zaidi ya mmoja kwa kutegemea na kazi wanazoomba na kupewa. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 barabara hii ilifanyiwa ukarabati pamoja na matangenezo ya kawaida kwa kutumia wakandarasi wawili walioonyesha kukidhi vigezo vyote vilivyoanishwa katika zabuni.

Mkandarasi wa kwanza M/s Kambo *Holdings*, alifanya kazi ya ukarabati wa kilomita 5 kati ya Mwanakaranga na Busombo kwa gharama ya shilingi milioni 45.883. Mkandarasi wa pili alikuwa ni M/S Limar's *Enterprises* alifanya kazi za matengenezo ya barabara ya kawaida ya barabara hiyo kwa gharama ya shilingi milioni 106.118 kazi zote zilikamilika kwa wakati na ubora uliotakiwa.

Katika mwaka 2008/2009 barabara hii ilifanyiwa matengenezo na wakandarasi watatu. Mkandarasi wa kwanza M/s Nyakahara *Investment Ltd* aliyefanya matengenezo ya kawaida barabara yote kwa gharama ya shilingi milioni 151.831, Mkandarasi wa pili M/s Halem *Construction Co. Ltd.* alifanya ukarabati kati ya Shilabela na Mwang'hosha kwa gharama ya shilingi milioni 55.881 na watu M/s Mahende Sogoni *Construction Co. Ltd.* alifanya matengenezo ya muda maalum kati ya Manigana na Solwa kwa gharama ya shilingi milioni 109.961. Wakandarasi wote walifanya kazi vizuri, kwa muda mfupi na kwa ubora uliotakiwa.

Mheshimiwa Spika, makandarasi wote hao wamekuwa wakipewa kazi kwa kuzingatia vigezo vilivyoanishwa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi Na. 21 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swalii moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa niulize swalii kama ifuatavyo; kwa kuwa wananchi hawa maeneo aliyoyatia ikiwemo Zuzuri, Ipango, Salawi na Zonza

wamekuwa na matatizo ya muda mrefu hasa kwa barbara hiyo iliyotajwa ya *Old Shinyanga* kuja Salawe, lakini pia wamekuwa na option ya kutumia barabara nyingine ambayo inatoka Mwanangwa, Misasi Salawe. (*Makofit*)

Je, Waziri anaweza kulieleza Bunge hili barabara hizo mbili safari hii wametenga kiasi gani ili kuweza kuwahudumia wananchi wa maeneo hayo ambao wamekuwa kisiwani muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru kwa kutambua juhudzi za Serikali zinazofanywa kwenye barabara hiyo lakini pia niseme tu kwamba Serikali inalitilia umuhimu mkubwa sana katika barabara yoyote ile ambayo itakuwa ni fupi na rahisi kufikika katika eneo lolote lile la nje.

Lakini sasa kwa barabara hi aliyoitaja kwamba ni kiasi gani mwaka huu kimetengwa awali kwamba barabara hizi ziendelee kutengewa fedha za mfuko wa barabara kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya na pale inaposhindikana tuendelee kuwasiliana kuona ni namna gani tunaweza tukazisaidia barabara hizi.

SPIKA: muda naona umetutupa mkono na swali linalofuata Wizara ya Nishati na Madini lina jibu refu sana, sijui kama Naibu Waziri anaweza kulipunguza lakini basi tumalizie hilohilo.

Kwa swali linalofuata Mheshimiwa Hajjat Mhonga Said Ruhwanya!

Na. 151

Upungufu wa Umeme Mkoani Kigoma

MHE. MHONGA SAID RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa, umeme ni Nishati muhimu katika kuchochea maendeleo na ukuaji wa uchumi na kwa kuwa Mkoa wa Kigoma una upungufu mkubwa wa umeme ambapo inatumika mashine moja tu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatoa jenereta za dharura ili kuunusuru Mkoa huo na adha hiyo wakati umeme wa gridi ya taifa ungali ukisubiriwa?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa inachangia katika kurudisha nyuma maendeleo ya Wananchi hasa wajasiriamali kwa kutochukua hatua madhubuti kumaliza tatizo hilo ambalo limedumu kwa muda mrefu?

(c) Je, Serikali inatambua kuwa Mkoa kukosa umeme ni chanzo cha mfumuko wa bei ya kusaga katika mashine za dizeli kwa kuwa mafuta nayo yamepanda bei na gharama za usafirishaji nazo zimepanda?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Said Ruhwanya wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkoa wa Kigoma una upungufu wa huduma ya umeme ambayo ni kichocheo cha Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi.

Kwa sasa mahitaji ya umeme katika mji wa Kigoma ni Megawati 5.0, ambapo mitambo iliyopo kwa pamoja inazalisha *MW 2.8* hivyo kufanya upungufu wa *MW 2* katika mji huo. Kwa sababu ya uzee na uchakavu wa mashine hizi, hujitaji kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* imeweka mikakati ya muda mfupi na mrefu ili kuondoa tatizo la umeme Mkoani Kigoma. Kama ilivyoelezwa hapa Bungeni tarehe 30 Januari, 2009 wakati tukijibu swlai la Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika mipango ya muda mfupi, Serikali ilitnega katika Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2008/2009 kiasi cha shilingi bilioni 13.8 kwa ajili ya kununua mitambo mipya ya kuzalidha umeme wa MW 6.25 Kigoma Mjini na itajenga kituo kipyta kitakachokuwa na jenereta tano zitumiazo dizeli zenye uwezo wa Megawati 1.25 kila moja ambazo kwa sasa zinaundwa huko Uhlanzi.

Jenereta hizi zinatarajiwa kuanza ufuaji wa umeme Agosti, mwakani yaani mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizi ambazo Serikali imechukua ni pamoja na ujenzi wa kituo cha ufuaji wa umeme wa uhakika zaidi kwa kutumika maporomoko ya maji ya mto Malagarasi chini ya mradi wa *Millennium Challenge Corporation* (MCC).

Kituo hiki kitakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 8 ambazo zinaweza kuongezwa hadi kufikia MW 28. Mradi unatarajia kuanza mwezi Aprili, 2010 kwa ujenzi wa barabara iendayo kwenye eneo la kufulia umeme.

Aidha, Serikali iko kwenye majadiliano na Serikali za Rwanda na Burundi ili kuikamilisha mradi wa umeme wa maporomoko ya rusumo, ambao upembuzi yakinifu umebainisha kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme hadi MW 80. Hatua zote kwa pamoja

zitachangia kupatikana kwa umeme wa uhakika, utakaosafirishwa na kusambazw aUvinza, Kigoma/Ujiji, Kasulu, Kibondo na viunga vyake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukarabati wa mashine mbili aina ya *Perkins* zinazotumia diseli zenye uwezo wa Megawati 1.0 kila mmoja na ununuzi wa injini mbili mpya za *Perkins* zitakazotumia mafuta ya diseli ambazo zitatumika wakati wa kipindi cha mpito, hadi mitambo mitano yenye uwezo wa MW 6.25 itakapo kamilika kwa ajili ya Kigoma Mjini.

Wizara ya Fedha na Uchumi imethibitisha kuwepo kwa kiasi cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya kuwepo kwa kiasi cha fedha kinachojitajika kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa injini za *Perkins*. Wawakilishi wa Perkins wamethibitisha kuwa injini zinatarajiwa kuwa tayari kwa kuleta nchini mwishoni mwa mwezi Julai, 2009.

Aidha, inatarajiwa kuchukua muda wa wiki tano kuikamilisha ufungaji wa injini za *Perkins* baada ya kuwasili kwa injini hizo mjini Kigoma. Mashine hizi mpya zikisaidiana na zile zilizopo zitaweza kukidhi kabisa mahitaji ya umeme wa uhakika kabla ya kupata umeme kutoka kituo kitakachokamilika mwakani.

(b) Mheshimiwa Spika, katika nadharia ya vipaumbele na mikakati ya kuondoa umaskini, Wataalam wa masuala ya uchumi na jamii walichukulia maji, Elimu na afya kuwa ni masuala makuu ya kukabiliana nayo katika kuondoa umaskini. Katika miaka ya hivi karibuni masuala ya miundombinu na Nishati ni masuala ambyao yanatambulwa kama sehemu muhimu ya vita dhidi ya umaskini. Kwa kutambua na kufahamu hivyo Serikali ya Tanzania imekuwa inasimamia miradi mbalimbali yote ikiwa na lengo la kuwaondoa wananchi wake katika umaskini na kuboresha hali zao za maisha.

Kwa kuwa, ni kweli usiofichika kwamba maeneo yaliyokosa umeme yakipatiwa huduma hiyo inawapatia wajasiriamali na wananchi wake nafasi za ubunifu na kuwa ni kichocheo cha utekelezaji wa kazi zao, na biashara zao kwa ufanisi zaidi. Wizara yangu imetengeneza mipango ya kufikisha umeme kwa wananchi tukizingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya miradi mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la nishatiya umeme katika kipindi hiki kama nilivyoeleza hapo awali. Ni kweli utekelezaji wa miradi hii kwa sababu mbalimbali baadhi zilizo nje ya uwezo wa Serikali, zimechelewa. Wizara yangu inahuzunishwa na hali hii na itaendelea kuyafanya kazi kwa kushirikiana na uongozi wa Kigoma na Idara na Taasisi zingine husika ili kuyapatia ufumbuzi wa haraka masuala haya.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mabasiliko ya bei za mafuta na haswa dizeli yana athari pana kwa bei za nafaka kuwa siyo tu zinaongeza gharama za kusaga pale ambapo kazi za kusaga hufanywa kwa kutumia mashine za dizeli, ila pia kwa kuwa kupanda kwa bei za dizeli zinaongeza pia gharama za usafirishaji na bei za nafaka maaassokoni.

Kwa hiyo, mchango wa mabadiliko ya bei za mafuta kwa uchumi kwa ujumla na siyo tu gharama za kusaga nafaka kwa mfumuko wa bei kwa tafsiri pana unafahamika. Hata hivyo inafahamika pia kwamba kama nchi, uchumi wetu hauna uwezo wa kudhibiti mwenendo wa bei za mafuta kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kukamilika kwa miradi hii ya umeme Kigoma Mjini na Mkoa wote kwa ujumla kutachangia kupunguza gharama za maisha kwa wananchi wa maeneo hayo haswa kama Nishati mbadala pale yanapotumika bidhaa za mafuta ya petroli, ikiwemo dizeli na mafuta ya taa.

MHE. MHONGA SAID RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, Bunge hili lilianza kabla sijazaliwa, maana yake ni kwamba Wabunge walikuwepo mpaka nimezaliwa nimesoma na nimefika mpaka Chuo Kikuu maana yake ni kwamba ahadi ziliendelea kutolewa mpaka leo hakuna utekelezaji.

Je, Serikali itaacha kutoa ahadi sasa na kutekeleza kwa sababu wananchi wamechoka na wanaona wanadanganywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa awamu zote kwa miaka 48 ya Uhuru.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba Mkoa wa Kigoma siyo *priority* ya Serikali na ndiyo maana anatuambia kwamba miradi mingi imekuwa haitekelezeki kwa sababu ya Serikali ilikuwa ikikosa uwezo. Ina maana ni kweli Serikali imekosa uwezo katika miaka yote hiyo?

Mheshimiwa Spika, ahsante! (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, maswali yake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Bunge hili limeanza kufanya kazi kabla ye ye hajazaliwa na hata kabla mimi sijazaliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niondoe hii dhana ya kwamba Chama cha Mapinduzi hakiweki kipaumbele kwa masuala ya Kigoma.

Kwa ruksa yako nimesema sasa hivi kwamba kwenye masuala ya kuondoa umaskini ni masuala mapana na suala la umeme lipo suala la miundombinu, maji afya na matatizo kwa ujumla ni mengi na uwezo wa Serikali una upeo wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba matatizo anayosema yeye ya umeme ya Mkoa wa Kigoma Serikali tunayafahamu, tunayafanya kazi usiku na mchana na ni matatizo yanayofanana na yale ya Masasi, Ruvuma na Mkoa wa Rukwa na hata Pwani. Kwa hiyo, katika hali hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba tumeyaweka katika kipaumbele ya utekelezaji wa mipango ya Serikaliya kumaliza tatizo hilo hasa tukitarajia kwamba mradi wa miundombinu unakwenda pia na utafungua pia hali ya uchumi wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa majibu hayo nimejibu maswali yake yote mawili. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa sehemu ya kwanza sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata ambayo tuliiahirisha.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa kioo cha utendaji wa kazi bora maana yake angeweza kupiga chenga leo na tusingekuwa na sababu ya kumlazimisha lakini kwa sababu ni mtendaji mzuri amefika kwenye Bunge kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kunukuu *Hansard* ya kauli ya Makamu wa Rais iliyopitia kwa Waziri wa Nchi Ofisi yake Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib na ninaomba kunukuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lingine amezungumza msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba Aboud Jumbe hakusikilizwa, Azimio la Tanganyika halikusikilizwa, Nyalali hakusikilizwa lakini hawasemi ukweli kuhusu Aboud Jumbe na Seif Sharif. Angesema kwamba aliyemfitini Aboud Jumbe ni Seif Sharif ndiye aliyeiba nyaraka kwenye droo yake akampa Nyerere. Kwa hayo, yote hayasemi hasa chimbuko la Aboud Jumbe kufukuzwa ni fitina ya Seif Sharif Hamad” (*Kicheko/Makofi*)”

Mheshimiwa Waziri Mkuu nafahamu kwamba mwaka 1984 Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere baada ya Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa kilichokaa hapa *CBE* Chuo cha Biashara kwa muda wa siku nne aliwatangazia Watanzania kwamba sababu ambazo aliyekuwa Makamu wa Rais Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Aboud Jumbe alijiuzulu kutokana na kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa Zanzibar.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu kauli hii iliyyotoka kwa Makamu wa Rais na kauli hii aliyoitoa Baba wa Taifa zinatofautiana. Ni ipi iliyo sahihi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kuliwezesha Bunge lako angalau linisamehe kwa kuchelewa kidogo kwa sababu ya safari ndefu. Niwashukuru sana Wabunge kwa kulielewa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la Hamad Rashid Mohamed ni gumu ni lazima tukubaliane hivyo, ukiniuliza kwamba lipi ni sahihi kati ya matamshi ya Viongozi wangu wote wawili nitakwambia sijui. Mimi nafikiri tunachoweza kujibu sahihi zaidi hapa ni kwamba kwa sababu ni jambo ambalo limeibuka katika mjadala ambao umepita hivi karibuni kutokana na hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano si busara tukataka kuanza kuendeleza maelezo haya katika mazingira tena ambayo yatazidi kufanya tutofautiane. Acha tulichukue tutakaa na Ofisi ya Makamu wa Rais upande wa Muungano tuone haya matamshi mawili yalikuwa na maana gani na baadaye tunaweza kuja kutoa maelezo namna tulivyolielewa kuliko kukurupuka hapa Mheshimiwa Waziri aanze kuleta mambo ambayo yatazidi kutuletea pengine mifarakan ambayo si ya msingi sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nilidhani Mheshimiwa Hamad limeeleweka hili, sijui.....

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nilitaka kumsaidia tu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubali kwamba wakati utakapokuja kutoa maelezo vilevile utaueleza ni namna gani hizo nyaraka za Mheshimiwa Jumbe ziliibiwa mpaka zikamfikia Nyerere maana kwa sababu ulisema bado unataka kuchunguza katika uchunguzi huo utakubali pia kuingiza hayo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani hapa sasa tutapata shida kwa sababu inawezekana kabisa mhusika katika Ofisi ya Makamu wa Rais alikuwa na taarifa ambayo aliweza kuileta hapa kutokana na yeye mwenyewe ama kushuhudia ama kusimuliwa na huyo tunayemtaja kwa sababu mambo haya unaweza kusema kwamba Bwana wewe mimi ndiye nimemchomea fulani, sasa hayo sidhani kama angemwambia Baba wa Taifa. Kwa hiyo, mimi sioni itakuwa rahisi kile kitendo cha kuchomoa kile kikaweza kuelezeza vizuri katika historia ya nchi.

Kwa hiyo, nadhani tuendelee!

MHE. MANJU SALUM OMAR MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, swali langu ninalotaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu linahusiana na *Tanzania Broadcasting Cooperation* yaani *TBC*. Hapo awali ilipokuwa *RTD* na baadaye *TVT* chombo hiki kilikuwa na utaratibu mzuri na ambao unaendelea mpaka sasa wa kila asubuhi wakati vipindi vinaanza wanaanza na vipindi vyta Dua kwa dini zote mbili yaani Waislam na Wakristo na utaratibu ulikuwa ni wa kupishana, leo inasomwa dua ya Kiislam na Mawaihda.....

SPIKA: Swali tafadhali!

MHE. MANJU SALUM OMAR MSAMBYA: Sawa! Kesho anakuwa ni Kasisi au Mchungaji. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu aniambie ni ipi dini rasmi ya Serikali nchini kwa sasa hivi kwa sababu kwa takribani kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa TBC katika kuendesha vipindi vyake wanapoanza vipindi asubuhi na hasa television saa kumi na moja na nusu muda wote wanaweka kwanza nafasi ya Wachungaji ndiyo wanaanza. Hivi na hao wanaozomea nawasikitikia kwa sababu hili lina maana katika mustakabali wa kuendesha nchi yetu.....

SPIKA: Uliza swali! Bado hujauliza swali! (*Makofi*)

MHE. MANJU SALUM OMAR MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, pengine hukusikia ila ulikuwa unaniambia mimi niulize swali wakati nimesema kwamba hivi ni dini gani rasmi ya Serikali?

SPIKA: Dah! Waheshimiwa Wabunge, nadhani leo tumeamka sijui vipi. Lakini jibu liko kwenye Katiba na kila mtu anafahamu. Nchi hii haiongozwi na dini yoyote, Watanzania kila mmoja yuko huru kuwa na dhehebu lake na dini yake lakini Katiba iko wazi kabisa kwamba nchi hii haiongozwi na Dini.

Tunaendelea na Mheshimiwa Victor K. Mwambalazwa!

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hapa nchini kwetu kuna magazeti yanayozidi 150 kwa siku na katika Afrika Mashariki ndiyo nchi pekee ambayo ina magazeti mengi sana na siku za karibuni yamezuka magazeti ambayo mengine yanavunja maadili ya nchi, mengine yanawekwa kwa siku moja ili kuweza kumlengesha mtu fulani au kundi la watu fulani.

Kwa kuwa, sasa hivi kuna mchakato wa kuileta na kuiboresha Sheria ya vyombo vya habari na kwa kuwa wenzenzu wa Kenya kwa kuchokozwa na magazeti haya wamegombana na wamepigana mpaka sasa hivi wametunga Sheria ya kukataza magazeti kuandika habari za uchochezi wakati wa uchaguzi. Na kwa kuwa, uchaguzi wetu unakaribia mwakani. Je, mpendwa wetu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye Muswada huo unaokuja Serikali iitaweka vipengele vya kuzuia magazeti kuchochea, kutukana na kutenganisha Watanzania?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Ndugu yangu Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, siku chache zilizopita wakati nilipokuwa nahitimisha hotuba yangu nilijaribu sana kulieleza jambo hili. Nilieleza kwa namna ambayo ilikuwa ni ya

kisera nikiamini kwamba Watanzania wote tunapaswa kujua kwamba nchi hii ni yetu na tunatakiwa tuipende na vyombo vyahabari vinaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza nchi hii kuwa tulivu na nchi yenye amani . (*Makofi*)

Lakini vyombo hivi pia vinaweza kuwa ni mwanzo wa mifarakano ambayo wakati mwingine inaweza kuwa si ya lazima. Nikavisihii vyombo vyahabari kwa dhati kabiba vijaribu kuzingatia maadili ya Kanuni ambazo wamejiwekea wao wenyewe. Na nikasema kwa nguvu sana kwamba Serikali si vizuri ikaonekana muda wote tunajaribu kuingilia kati mayyombo haya kwa kuyafungia au kuya *harass* kwa namna yoyote. Lakini ikibidi Sheria ipo. Kwa hiyo, tunaweza bado tukafanya hizo zinazotakiwa.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba bado Watanzania hili tutaendelea kulielewa na Wabunge tutasaidia sana katika kujaribu kujenga vyombo vyahabari ambavyo ni makini vipenzi na vyenye taaluma zinazotakiwa.

Kwa hiyo, Sheria inayokuja imejaribu kuzingatia mambo mengi katika kujaribu kuweka mwelekeo ambao tunadhani Watanzania wengi wataunga mkono.

Sasa sitaki kwenda kwa undani kwa maana ya kusema je na hili na hili na kadhalika. Tusubiri ule Muswada utakapoletwa hapa kama utakuwa na mapungufu utaboreshwah hapa hapa.

Lakini dhana na azma ya Serikali kwa kweli ni kujaribu kuweka misingi ambayo tunadhani vyombo hivi vitaweza kutusaidia kuendesha shughuli za Serikali na za wananchi kwa namna ambayo kwa sehemu kubwa inakubalika na Watanzania wengi.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapunduzi (CCM) ya mwaka 2005 iliahidi kukata kiu ya Watanzania wengi ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara kama vile ilivyo kwa ndugu zao wa Tanzania Visiwani.

Lakini kwa mshangao wa wengi juzi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ilidhihirika wazi kwamba Mahakama ya Kadhi Tanzania haipo tena kama walivyonukuu baadhi ya Magazeti kwa kusema kwamba Mahakama ya Kadhi yayeyuka, Serikali yazika rasmi Mahakama ya Kadhi. (*Makofi*)

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe kama mtekelezaji makini, mahiri na usiyeyumba wa Chama cha Mapinduzi na Serikalini. Je, unawaelezaje Watanzania kuhusu kushindwa huku?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwamba sikuwepo Bungeni haina maana kwamba Serikali ilikuwa haipo, Serikali ilikuwepo na maeleo yaliyotolewa ni ya Serikali sasa inawezekana maeleo yale yasikupendeze sana ukaona kama vile jambo hili

halijashughulikiwa. Lakini mimi nadhani majibu ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa ni mazuri yanajaribu kutupa mwanzo mzuri sana wa kujaribu kufikia hatua ambayo tunadhani ni ya dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mimi niseme tu kwamba jambo hili mnaweza mkaliona kwamba ni jepesi lakini katika nchi kama hii ambayo mnakuta mna mjumuiko wa madhehebu ya dini mbalimbali hatuna budi wote kujaribu kutumia busara kubwa sana katika kujaribu kufanya maamuzi yanayogusa imani za dini mbalimbali.

Hii ni moja kati ya maeneo ya aina hiyo na ndiyo maana unaona Serikali inajitahidi kujaribu kuona kama lengo ni kutaka kuwa na mfumo wa kisheria unaoweza kusimamia masuala ambayo ni ya kijamii lakini yanayoweza vilevile kuhudumiwa kwa mfumo ambao hauleti hisia za namna yoyote kwa nini tusiende na mfumo huo? Sasa ndiyo maana umeona Waziri juzi alieleza vizuri kwamba tunadhani labda kwa njia hii tunaweza lakini najua si jibu inawezekana hamlipendi lakini mimi nasema chondechonde jambo hili la masuala ya dini katika mazingira ya nchi ya Tanzania hamwezi mkalisukuma tu kwa namna ambayo mtu anadhani akifanya hivyo ata *achieve* kitu. Mnaweza mkazua zogo kubwa likawashinda hata namha ya kuweza kulisimamia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nadhani twende nalo taratibu tutaweza kufika mahali tutaelewana.

Mheshimiwa Spika, labda niongeze tu kidogo na inawezekana ni maoni yangu tu kwamba Wizara ilisema wamejaribu kutazama kutazama mifumo ya nchi nyingine katika kujaribu kuona namna gani tunaweza tukajaribu kushughulikia jambo hili. Mimi nafikiri tungeipa muda Wizara kidogo na ninyi wenyewe mpate nafasi ya kuona hiyo mifano aliyoitao ya *South Africa* ni kwa kiwango gani inaweza ikakidhi jambo hili bila kuudhi madhehebu mengine mengi ambayo yapo hapa. Tumeishi vizuri kwa raha, kwa amani na bila kugongana. Mimi nafikiri tukilenga huko tunaweza tukafanya vizuri na nchi ikaendelea kuwa ya amani na utulivu. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubaliana nami kwamba ilani iliandikwa kwa dhamira njema kabisa na namna swali lilivyopindwapindwa na kuchukua mifano ya *South Africa* badala ya mifano ya Zanzibar au ya Kenya inaonesha kwamba hakukuwa na nia safi katika utekelezaji wake lakini Ilani hii inaonekana kwamba iliwekwa kwa ajili ya kutafuta kura za Waislam Tanzania. Utakubaliana na mimi kuhusu hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu nisamehe. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi haikusema itaanzisha Mahakama ya Kadhi, ilisema kuangalia uwezekano wa kulishughulikia suala la Mahakama ya Kadhi, ndivyo hivyo wamelishughulikia. Sasa wewe unaweka maneno na hisia zako kwenye ilani ambayo wala hayapo, hakuna mahali popote CCM imeahidi itaanzisha. Kama ingekuwa ni hivyo ingekuwa ni suala la kuanzisha tu lakini ilisema italishughulikia na kutazama uwezekano. Maneno hayo ndiyo yako kwenye Ilani.

Tunaendelea, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir!

MHE. MUDHIHIRI M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Waziri Mkoo kwa kuwa umekuwa ukionyesha kwa vitendo juu ya dhana ya Serikali yetu sikivu na katika dhamira ya kuthamini mchango wa sekta binafsi katika ustawi wa nchi yetu na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkoo hivi karibuni ultamka kwamba ungependa Tanzania *iwe the reading national* yaani yene utamaduni wa kusoma vitabu. Lakini wakati huohuo Serikali tumeshatoa tamko kwamba katika mfumo wa Elimu kutoka msingi mpaka Sekondari tutakuwa sasa na kitabu kimoja tu badala ya vitabu vingi kama ilivyokuwa hivi sasa jambo ambalo litaleta ugumu kutengeneza *reading nation.* (*Makofii*)

Je, utakuwa tayari kukubali ombi la chama cha Wachapishaji wa Vitabu kukutana na wwe kabla ya siku ya Bajeti ya Wizara ya Elimu ili tusiwe tunabadilika baada ya michango ya Wabunge tuonekane kwamba sisi Serikal yetu ni *Pro active* badala ya kuwa *Reactive?*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mudhihiri anauliza jambo hili kwa sababu yeye mwenyewe ni mtu mmoja ambaye anapenda sana kusoma ukimsikiliza wakati akijadili hapa ni mtu mmoja mwenye uwezo mkubwa sana wa kunukuu mambo mengi tu. Kwa hiyo, ni dhahiri ana kila sababu.

Lakini niseme kwamba tatizo la wachapishaji wa vitabu hapa nchini ni kubwa na mimi nalielewa na wameshatuandikia na baadhi nilikutana nao. Kwa hiyo, kuna mlundikano mkubwa sana wa vitabu vyao.

Lakini mimi niseme kwamba huu uamuza ambaa ulifanywa na Rais si lazima kwamba ndiyo sababu pekee ya matatizo ya wachapishaji wa vitabu, yako matatizo mengine vilevile. Sasa mimi nakubali na kimsingi nilishakubali kabisa hata kabla hujauliza swali. Kuna mtu alikuja akaniona kwamba tutaonana tutazungumza na nitajaribu kuwapa mtazamo wangu ninavyoona na siku za mwanzoni niliwahi kushiriki hata kwenye maonyesho yao pale Dar es Salaam nikawapa ushauri wangu lakini naona kama vile bado ulikuwa haujatekelezwa.

Kwa hiyo, ni jambo jema tu Mimi sioni kama kuna tatizo Mheshimiwa Mudhihir kukutana na Viongozi hawa tukazungumza tuone namna ya kuwasaidia. (*Makofii*)

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkoo.

Mheshimiwa Waziri Mkoo mwaka 2001 nchi yetu iliingia katika dhahama iliyotokana na maandamano ya wananchi, maandamano ambayo yalizalisha waathirika wengi wakiwemo Wanawake, watoto na wengine wengi.

Serikali wakati huo iliunda Tume chini ya Bwana mmoja aliyejewa akiitwa Hashim Bitta, kutazama chanzo na kupendekeza mambo kadhaa mionganii mwa

walipendekeza kutolewa kwa kifuta machozi kwa waathirika kwenye maandamano hayo. Tokea muda hadi leo ni mwaka wa nane kifuta machozi hicho hakijatolewa, Serikali inasemaje katika suala hilo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kuna siku nilimwekea maneno ndugu yangu Hamad hapa baadaye akanisahihisha, kwa hiyo niliamini na wewe utakuwa ulisikia majibu ya Hamad kwa maana kwamba alichokuwa anasema ndicho unakisema. Kwa hiyo, kama halijatekelezwa maana yake ilikuwa tu ni kwamba basi Serikali italitazama tuone kama tunaweza tukalipatia ufumbuzi mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Majibu hayo ambayo anayatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo nilshapewa humu Bungeni zaidi ya mara nne, mimi mwenyewe suala hili nilishaliuliza karibu mara nne na nilishalichangia katika Wizara ya Waziri Mkuu zaidi ya mara tatu, majibu yamekuwa ni hayo hayo. Sasa inaonekana ni tatizo kwa Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania.

Je, sasa isingekuwa vema sasa Serikali ikatoa kauli rasmi kwamba sisi tumeshindwa kutoa kifuta machozi kwa Watanzania hawa ambao wanatoka Pemba ili tukaielewa Serikali ya Muungano?

WAZIRI MKUU: Sasa mimi niikisema hivyo wewe itakusaidia nini? (*Makofi*)

Kwa sababu na wewe huwezi ukawalipa fidia. Kwa hiyo, haisaidii lolote na mngekuwa na uwezo huo mngekuwa mmeshafanya kazi hiyo zamani yakaisha, ndiyo maana nasema hebu tupeni nafasi, acha tulianglie ni kweli tumechukua miaka nane lakini kutakuwa na sababu nyingi tu zilizotufikisha hapo.

Kwa hiyo baada ya hapo tena ukija kuniuliza siku nyingine nitakuambia sina jibu lakini kwa leo nasema wacha na mimi nijaribu kama umejaribu nyuma ikashindikana acha nijaribu tena na mimi tuone kama kuna namna ya kuweza kulimalizi. (*Makofi*)

MHE. MCHUNGAJI GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali kwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kampuni ya *Zain* imekuwa ikiendesha mashindano ya vyuo vikuu vya Afrika kwenye luninga na nchi kama Nigeria, Siera Leon, Cameroon, Kenya na hata nchi za Malawi, Zimbabwe na Zambia na nchi za Afrika Mashariki yote zimekuwa zikishiriki.

Lakini kwa masikitiko makubwa vyuo vyetu vikuu vya Kitanzania vimekuwa vikishika mkia na sababu kubwa iliyojitezea ni kwamba wengi wanashindwa kujieleza kwa lugha ya kingereza na nyingine ni kwamba wanakosa ile *general knowledge* ya kujua mambo mbalimbali na kupata *division one or two*, na vilevile wanakosa kujiamini na ujanja wa kuweza kujibu haraka kama wenzao. (*Makofi*)

Je, Serikali imeliona hilo? Inachukua mikakati gani kusaidia kizazi hiki ambacho ni taifa letu la kesho? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu dada yangu, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Rwakatare, swali lake zuri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nami nimekuwa nafuatalia fuatilia hili jambo, lakini sikuwa nimelitazama kwa mtazamo wake. Yeye amejaribu kutoa changamoto hapa kuonesha kwamba, tatizo letu ni Luga ya Kiingereza na anataka kujua tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, mimi siamini sana kama hiyo hasa ndiyo hoja ya msingi, kwa mtu wa Chuo Kikuu na wengi hapa tumetoka Vyuo Vikuu, hata Kiswahili chenyewe Bungeni kinatushinda, kila siku tunachanganya Kiingereza na Kiswahili. Nadhani inaweza kuwa ni matatizo ya mwanafunzi mmoja mmoja, wale wanaojitokeza bila maandalizi ya kutosha bila kujua wafanye nini, kabla ya kwenda katika vinyang'anyiro kama hivi. Mimi napenda niamini kwamba, wasomi wetu wengi luga hii wanaijua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, sitaki tujivune sana kwamba, kuonekana unajua sana Kiingereza wewe ndiyo msomi mkubwa, hapana. Mimi siamini hilo. Kusema kweli, bado nadhani ni lazima tujitahidi tuiimarishe Luga ya Kiswahili, tuijengee heshima yake, ikibidi hata kama tunakwenda huko, wajue kwamba, tunakwenda kule lakini Kiingereza ni lugha ya pili tu, lugha yetu hasa rasmi ni Kiswahili na twende huko ikibidi tutumie ukalimani kama nchi nyingine wanavyofanya. Kwani Mchina akienda pale kushindana atafanya vizuri?

Unless ni Mchina ambaye amesoma, amejitahidi kulenga lugha ile kama msomi wa Lugha ya Kiingereza, lakini kusema kweli, kujaribu kuonesha kama vile kutokushinda kwa sababu Kiingereza kinatushinda, mimi siamini sana. Mimi bado naamini wasomi wapo wanatosha, lakini hawa wanaokwenda kule wajiandae vizuri ili tuweze kufanya vizuri.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE. Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ahsante pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maeleo mazuri. Nilikuwa napenda niweze kutoa angalizo kama Mtanzania na mdau wa elimu; sisi kama Tanzania hatuko kwenye kisiwa, wanafunzi wanaohitimu hapa Tanzania lazima watakwenda nchi za nje na inakuwa masikitiko makubwa ya kwamba, hatuwezi kupata *international posts*, kwa sababu watu wetu wengi wanashindwa kujieleza au kuchagia kwenye mikutano mbalimbali; kama mliona tangazo la Vodacom, bwana mmoja Massawe amepata *investor*.

SPIKA: Lenga kwenye swali Mheshimiwa.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Eeh yaani, Kiingereza kama vile madarasani yule, kijana alikuwa anashindwa kueleza *global warming*, lakini

ameweza kueleza kwa Kiswahili. Kwa hiyo, ni muhimu sasa, tuungane na wenzetu kama wa Rwanda, waliokuwa *Franco Phone*, sasa hivi wanabadilika wanakuwa *Anglo-phone* kwa sababu kuna Afrika Mashariki inakuja, sisi tutashindana vipi? Sisi tutashika *posts* gani, kama hatuwezi kuwaandaa watu wetu na wao wajue Kiingereza? Tukipuuzia Kiingereza ambacho ni lugha inayozungumzwa ulimwenguni kote. (*Makofit*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, hivi kweli Wanigeria wanajua Kiingereza kuliko Watanzania? Kama hoja ni hiyo, mimi siamini. Ninachosema tu ni kwamba, tunao Watanzania wako kwenye vyombo vya kimataifa, wanafanya kazi vizuri. Tunao Watanzania hapa tunakwenda kwenye mikutano na tuna-*perform* vizuri sana. Aah! Mama Rwakatare, hata wewe naamini ukienda Uingereza, unaweza ukazungumza Kiingereza kizuri tu.

Nadhani tuzungumze jambo hili kwa mtazamo kwamba, Kiingereza ni lugha ya pili. Kwa hiyo, kama lugha ya pili, haiwezekani tukafanya kana kwamba, kwa kuwa ni lugha ya pili, basi tunaweza tukafanya vizuri sana. Kwa sababu ni lugha ya pili tu hii, kwa hiyo kama upo upungufu wa hapa na pale, unaweza kutazamwa, lakini mimi bado naamini kwa dhati kabisa, jamani Watanzania tuliofika Vyuo Vikuu, wengi wetu uwezo wa Kiingereza ni mkubwa sana. Sasa kama iko kasoroo hapa na pale moja moja, hilo ni tatizo ambalo linaweza likatazamwa kwa namna ambayo tunaweza kuifanya vizuri zaidi. Mimi nasema jamani hata Kenya hawa wasikilizeni Kingereza chao, nisikilize na mimi Mtanzania nikizungumza Kiingereza, Tanzania *is much better off if I may put it in English* kuliko hata wao wenyewe. (*Makofit*)

SPIKA: Swali la mwisho Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Mara, nitumie fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla, kwa jitihada zao walizozionesha Mkoani Mara katika kusitisha mapigano yanayoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kukuuliza swali. Kwa kuwa, moja ya mikakati uliyoitangaza katika kukomesha hali ya mapigano ni pamoja na Serikali kutaka kuanzisha Kambi ya JKT. Je, ni utafiti wa kiwango gani umefanywa na Serikali na kuona kwamba Kambi ya JKT ndiyo itakuwa suluhisho la amani katika Wilaya za Tarime na Rarya? Na kwa kuwa Wilaya za Tarime na Rarya, kwa ujumla Wazee wa Jadi wana nguvu sana katika maamuzi.

SPIKA: Mheshimiwa unasoma?

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Nimeandika swali langu kwenye karatasi.

SPIKA. Aah ni kinyume cha Kanuni, wewe uliza tu, haturuhusiwi kusoma maswali.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa katika Wilaya za Tarime na Rarya, Wazee wa jadi ni Wazee ambao wanahehimika sana katika kufanya maamuzi ya kijamii; kwa hiyo ninataka kujua Mheshimiwa Waziri Mkuu, mmewashirikisha vipi, Wazee hawa wa Jadi katika suala hilo linaloendelea hivi sasa Wilayani Tarime? (*Makofî*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, tatizo la Wilaya mbili za Tarime na Rarya, unaweza ukalieleza kwa lugha nyingi, kwa maneno mengi, lakini kwa kifupi hali iko hivi; Tumekuwa na matatizo haya kwa miaka mingi, ndiyo maana wengine wanafikiria ni jadi ya Wakurya kupigana, kuuana, lakini mimi sitaki niamini hivyo.

La pili, ukienda pale unaambiwa na watu wote katika maeneo yote mawili, hakuna uhasama wowote kati ya Mluo na Mkurya, kwa maana ya makabila makubwa mawili. Lakini yapo matatizo ya kiutamaduni ya magomvi ya kiukoo kati ya baadhi ya koo mionganoni mwao, ndani ya kabila moja la Wakurya na mara nyingine ugomvi unaibuka kati ya Waluo na Wakurya, chimbuko lake wizi wa mifugo. Kwa hiyo, hata hili ambalo limejitokeza juzi, chimbuko lake ni wizi wa ng'ombe watano. Wameibiwa upande wa Waluo, wamefuatilia nyayo wakapata ng'ombe hao watatu upande wa Tarime, wakataka na wale wengine wawili wawapate, vita ikaibuka; nyumba zaidi ya 500 zimechomwa, watu 32 wamepoteza maisha na vitu vingine vya ovyo vingi tu. Mionganoni mwao, upande wa Tarime, watatu ni Wanawake, wawili ni Wanaume.

Sasa dada yangu ananiuliza, ninyi mnasema JKT ndiyo itakuwa suluhu ya tatizo la pale? Jibu ni hapana! JKT sio suluhu ya tatizo la Tarime na Rarya. Tunachokisema hapa ni nini? Ni kwamba, tujaribu kuunganisha nguvu zetu kwa kadiri itakavyowezekana, hawa Wazee wa Jadi tutawatumia lakini kuwepo kwa Kambi ya JKT pale nako kutasaidia vilevile kujaribu kuwapata hata vijana wa mle ndani nao kuwapeleka katika makambi haya, kwani ni sehemu ya wananchi ambao wanaweza wakatoka na mtazamo mpya wa namna ya kusaidia kuleta hali ya amani katika eneo hili. Ndio maana tumesema sio JKT tu, lakini tunafikiria vilevile pengine tuanzishe mfumo ambao utatuwezesha kuwa na mamlaka makubwa zaidi ya kipolisi kuliko ilivyo hivi sasa katika jitihada tu za kuweka uzito na suala la ulinzi na usalama kwa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa vilevile mambo haya yanachochewa na mpaka kuwa karibu, kwa hiyo tunahitaji, kama Serikali kuchukua hatua za ziada kidogo kuweza hata kuhimili na kudhibiti hali ya mpaka wetu, ambao unachangia sana utoro na utoroshaji wa mifugo kwenda upande wa pili. Kwa hiyo, sina jibu la moja kwa moja kwamba, JKT ndiyo suluhu, hapana, sote tutajitahidi kutumia kila litakalowezekana ili tuweze kurejesha hali ya utulivu.

Mheshimiwa Spika, kubwa nililojifunza pale ni kwamba, maeneo mengi yenye matatizo haya ya kiutamaduni, yana matatizo vilevile ya elimu, kutojikita katika maeneo haya kwa nguvu, yana matatizo vilevile ya kutokuwepo kwa dini ambazo zinasaidia kujenga maadili na fikra mpya za namna ya kuishi kama binadamu wa kawaida. Kwa hiyo, yote haya lazima twende nayo, kuongeza uwezo wetu wa kujenga shule pale, tupeleke walimu, wasome kwa nguvu, vilevile madhehebu ya dini na yenywewe yajikite

katika maeneo haya. Tukitumia njia mbalimbali hizi, tunaamini ndani ya miaka kadhaa ijayo, hali inaweza ikabadilika na tukaanza kupata tena hali ya utulivu na amani. Uzuri wananchi wapo tayari na tumeacha wameshaelewana vizuri na mimi imani yangu ni kwamba, hali itaendelea kuwa tulivu zaidi.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huo ndiyo mwisho wa dakika 30 za maswali kwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika - Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Kanuni?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7).

SPIKA: Endelea Mheshimiwa Zambi.

MHE. GODFREY W.ZAMBI: Mheshimiwa Spika, jana swali langu lilikuwa kwenye *Order Paper* na lilikuwa la 148 na Kiti kilitoa maelekezo kwamba, swali hili litapangwa leo na mimi leo nikawa natoka nakimbia najiandaa najua swali langu litakuwepo lakini, sijalionna kwenye *Order Paper*. Nataka maelekezo yako; swali langu litapangwa lini sasa?

SPIKA: Ahsante, eeh mwongozo huo ulioomba ni sahihi kabisa, kwa sababu unaambatana kabisa na kipindi hiki cha maswali ambacho tumekihitimisha. Nadhani itakuwa ni bahati mbaya tu, hatuna utaratibu wa kumminya Mbunge yejote kuhusu swali lake. Kwa hiyo, pengine mawasiliano na Ofisi ya Katibu, yaliweza kuwa hafifu, siwezi kukuhakikishia kwa kesho, lakini nina hakika kati ya hizi siku mbili, kesho na keshokutwa, itawezekana, ikishindikana kesho inaweza kuwa ni Jumatatu. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko ukumbini: Tunao Wanafunzi wa Udaktari 36 kutoka Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki Memorial (HKMU), ambao wamekuja kuangalia shughuli za Bunge hapa Dodoma.

Naomba pale walipo wasimame. Aah wale pale, ahsante sana Madaktari wetu watarajiwa, tunawasubirini kwa hamu, tunaomba sana Mungu awawezeshe muweze kufuzu ili mjaze nafasi katika eneo hili ambalo wananchi sasa hivi wana shida nalo sana. Ahsante sana na ninawopongeza kwa kuchagua kusomea Udaktari.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi, ambao ni Mwalimu Mzenga Zambi, pamoja na Bwana Michael Mwashiuya, nadhani kutoka Mbozi, ndiyo wale pale wawili, ahsante sana karibuni sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, ambao ni jumla ya wanafunzi 72 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi Kikombo, Wilaya ya Mpwapwa. Walimu na Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kikombo, ahsante sana, tunafurahi kuwaona vijana nadhifu kabisa na Walimu. Tunawashukuru Walimu

kwa kuwaleta vijana wetu hapa, kuja kushuhudia mambo ya Bunge na tunawataki mema katika kazi zenu ili kutokana na hao, Tanzania iweze kupata wataalam bora, pamoja na wale ambao watajua vizuri sana Kiswahili na Kingereza. Ahsante sana, tunawataki mema.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, ambao ni Wawakilishi wa Timu ya Mandela Queens, timu bingwa ya mpira wa miguu kwa Wanawake, Mkoa wa Dar es Salaam, ambao wanatoka katika jimbo lake. Wachezaji wa Mandela Queens, aah wale pale na Kombe lao, ahsante sana. Hongera sana Mheshimiwa Azzan na tunafurahi Tanzania inainuka katika mpira wa miguu kwa wanawake na sisi Wabunge, tunawapongezeni sana kwa mafanikio yenu. (*Makofii*)

Matangazo ya kazi: Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anahitaji leo saa nane mchana, Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini, mkutane Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Hassan Khatibu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ameniomba nitangaze kwamba, Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane leo saa saba mchana katika Ukumbi Na. 227.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo yetu. Katibu, kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2009/2010 – Wizara ya Miundombinu

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA. Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo hapa, kuna Wabunge wanne ambao hawajachangia, halafu na wengine walichangia mara moja; nitawatamka wale ambao hawajachangia na ndio watakwendwa kwa mtiririko huo. Wa kwanza Mheshimiwa Nimrod Mkono, atafuatiwa na Mheshimiwa Ephraim Madeje, halafu Mheshimiwa Tatu Ntimizi na baadae Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. Sasa namwita Mheshimiwa Nimrod Mkono.

MHE. SAID A. ARFI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika - Mheshimiwa Arfi.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7). Nilikuwa naomba mwongozo wako kuhusu majadiliano; ni kwamba, walikuwepo Wabunge ambao hawajawahi kuchangia hata mara moja, wamepewa fursa ya kwanza ya kuchangia, jambo ambalo tayari ulikuwa umeshalifanyia maamuzi na limeteklezwa kama ulivyokuwa umeagiza.

Wapo Wabunge ambao wamechangia mara moja, lakini Bunge hili ni la Mfumo wa Vyama Vingi, Wabunge wote ambao walikuwa hawajawahi kuchangia; Mbunge kutoka Kambi ya Upinzani alikuwa ni mmoja na waliochangia mara moja, Mbunge kutoka Upinzani yuko wa 17. Sasa Wizara hii itapita ikiwa imechangiwa na upande mmoja tu wa Chama Tawala na Mwakilishi mmoja kutoka Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Nini nafasi ya wachache katika kuwalilisha ndani ya Bunge? Naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa kutukumbusha hilo ingawa takwimu ulizonazo sio sahihi. Wabunge wa Upinzani kwenye orodha yangu ni wawili; Mheshimiwa Arfi, wewe ni wa 12 na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ni wa 16, lakini tutaangalia mwenendo unavyokwenda. Kila mara ndiyo maana kunakuwa na manung'uniko hapa na pale, *democracy* kamili ni kuchanganya dhahiri kabisa. Tutaona, bado ni saa nne tu na dakika chache; kwa uzoefu wetu, kwanza wewe nikuhakikishie utafikiwa, labda kwa maana ya jinsia na Kambi ya Upinzani, nitaweza kumpandisha kidogo Mheshimiwa Magdalena na kwa kufanya hivyo, mambo yatakuwa yametimia. Ahsante sana Mheshimiwa Arfi kutukumbusha hilo. Mheshimiwa Mkono.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, nami nichangie hoja iliyoko mbele yako.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, ambao wameungana nasi wakiwemo, Mheshimiwa Mwanjale, Mheshimiwa Charles Mwera na Mheshimiwa Bukwimba, nawapongeza sana kwa ushindi walioupokea kwenye Majimbo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa kutoa rambirambi zangu za dhati kwa vifo vilivyotokea; kwanza, kwa aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Bwana Chacha Wangwe, pamoa na Phares Kabuye na Profesa Othman, aliyetutoka ghafla.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda mrefu, ningependa kusema kuwa, hii bajeti mimi siiungi mkono, kwa sababu kubwa mbili. Mwaka jana nilipokuwa nikichangia bajeti, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri, Barabara ya kutoka Musoma – Fort Ikoma, ambayo ilikuwa imeimbwa zaidi ya miaka 40 imefika wapi; iko kwenye Ilani ya Chama wakati wa TANU mpaka CCM, mwaka hadi mwaka?

Mheshimiwa Spika, kama historia yangu iko sawa, wewe uliwhali kuwa Waziri wa Miundombinu wakati huo, bila shaka tatizo la ujenzi wa barabara hii na wewe pia ulilishughulikia. Tulipopata uhuru, jambo kubwa ambalo Taifa lilichukua kutoa uamuzi ni kwamba, barabara kutoka Musoma mpaka Arusha, ni lazima iwepo. Ilikuwa lazima tuunganishe Arusha na Musoma kwa njia mbili; Barabara na Reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa ndiyo maamuzi ya Serikali, sijapata maandishi yoyote yanayosema wameshabadilisha usemi huo. Haijawahi kusemwa kwamba, hiyo barabara ama reli hatupati. Wakati wa uhai wake Mwalimu, alikuwa anarudia kila mara, barabara kutoka Musoma lazima iende Arusha. Sasa kupitia wapi kwa wanyama?

Aliwahi kusema, kama kuna tatizo la hawa wanyama, basi wahamisheni ili wananchi waungane Musoma na Arusha. *Environmentalists* walipiga kelele kweli, kusema hawataki barabara Serengeti au Mbugani, sasa nataka kujua kama hiyo Sera bado ipo ama haipo? Mwaka jana sikupata jibu zuri, mwaka huu nimekuwa nafuutilia kwa karibu sana kwa Waziri, mpaka ameniandikia barua, alimwandikia mwenzangu barua na ningependa kuisoma: “Tafadhali rejea ujumbe wako, napenda kukujulisha kwamba, barabara hii ya Musoma – Tarime Junction – Makutano Juu – Butiama – Nyamuswa – Nata – Ikoma Gate – Nabihili imetengewa, jumla ya shilingi milioni 926 ni kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum.” Sisi hatuzungumzii matengenezo ya ukarabati wa ile barabara, tunazungumzia *re-development* ya barabara hizi kuunganisha Musoma na Arusha, kwa njia ya reli na njia ya Barabara, ndiyo Wananchi wa Mara wamekuwa wanasubiri kwa miaka 45 leo.

Mheshimiwa Spika, barabara mpya zinakuja, zinajengwa, Wananchi wa Mara wameachwa gizani. Sasa ilani inayozungumzwa na Mheshimiwa Waziri kwenye Kitabu chake, hakuna lolote alilotaja barabara ya kwenda Arusha ama Reli. Sasa Ilani ya Chama ni ya Chama cha Mapinduzi ama ni Ilani yake mwenyewe?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana, hata kwenye Ilani hii kuna mambo mengine amesema ya uongo na nitaomba unipe nafasi ninukuu. Ukurasa wa sita anasema, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Sekta ya Miundombinu ilielekezwa kutekeleza yafuatayo: Ibara ya 44 anazungumza kukamilisha ukarabati wa barabara zote ambazo zinaendelea na ujenzi wa kiwango cha lami, ikiwemo ninanukuu: “Kiabakari – Butiama.” Katika ukurasa wa 7 anasema, wametengeneza Barabara ya Kiabakari - Butiama kwa Kilomita 17. Hizo Kilomita 17 amezipata wapi? Kutoka Kiabakari kwenda Butiama ni kilomita 11 tu, sasa kama umetengeneza na umelipa wakutengenezee kilomita 17 ambazo sita ni hewa na hela zimelipwa; je, unataka na mimi niunge mkono wizi huu ama hapana?

Mwaka jana pia nilipata matatizo kumuelewa Mheshimiwa Waziri, alipokuwa akisoma hotuba yake. Alisema wakati huo, barabara ya kutoka Musoma kwenda Fort Ikoma ni kilomita sijui ngapi, ambazo pia zilikuwa sio za kweli, akarekebisha. Tatizo langu kubwa sasa ni hili; nini kinatokea? Kulikoni kwa barabara hiyo? Barabara itajengwa ama haijengwi na kama haijengwi kwa nini niunge mkono hoja hii?

Mheshimiwa Spika, ukiona nchi nzima ya Tanzania, barabara ambazo zinatengenezwa ni mpya kabisa, sasa nyingi zinakwenda kule ambako viongozi wanatoka, sasa huyu mzee wa watu aliyefariki miaka 10 iliyopita, aliomba waunganishe Mara na Arusha, hamumsikii miaka 10, mnataka sisi watu wa Mara tuwaeleweje? (*Makofi*)

Je, ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi ama ni ujanja unatumika? Nimesikia asubuhi hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anaeleza tatizo la Tarime kwamba, watu wanaufana hajui maana yake nini mpaka wanaweka naambiwa *National Services*, lakini matatizo ya Tarime yanachangiwa kwa kiasi kikubwa sana kwa kuwa hakuna muungano mzuri kati ya Musoma na soko la vyakula Arusha ama sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mkoa wa Mara sasa wanategemea sana Kenya sio Dar es Salaam. Hakuna barabara, hakuna reli, hakuna mwekezaji yeote anayeweza kwenda Mara kufanya kazi, utawekezaje Mara kama hakuna barabara, reli ama uwanja wa ndege; nani atakayekwenda huko? Wanakwenda Kenya kwa sababu Kenya wanatusaidia mengi, ukiugua una-cross border unakwenda unapata matibabu kirahisi. Ukiwa na ng'ombe wako wa kuuza, unapeleka soko la Kenya, maana Serengeti huruhusiwi kupita. Dar es Salaam ni mbali; miaka yote hii tunafanya nini? Vijana wetu hawana ajira, wakichukua mifugo kwenda kuiuza Kenya kwenye soko wanakamatwa, leo nimesikitika sana kusikia kwamba, mnaweka *National Service*, Polisi wawakamate hawa vijana wanaokwenda kufanya biashara; sasa waende wapi?

Mheshimiwa Spika, ndio maana siungi mkono hoja hii, hamuwatendei haki watu wa Mara, mmetuacha gizani miaka 45, tunakwenda wapi? Kwa maana hii sitaki kuendelea mbele, nataka njue kama tutapata reli na barabara au hapana?

Najua fika unavyopeleze jirani zetu wa Kenya wameweka ngumu hawataki barabara ijengwe, huyu tajiri wa Gurumet alijitolea kujenga barabara ingawa kuunganisha Mara kupitia Loliondo mpaka njia nyingine. Mpaka leo huyu mwekezaji anataka kutusaidia pia mmemzuia kufanya hivyo. Mheshimiwa Waziri, hajafika hata Butiama na kama amefika sio kwa shughuli ya kuona tatizo la barabara tulilonalo watu wa Mara. Nasema kwa masikitiko kweli, kama ndiyo hivi hatutafika, kwa nini tulipeleka kaburi pale, tumemzika pale ili Watanzania waende kumwona, tunajifunza nini?

Mheshimiwa Spika, kengele ya mwisho imelia, naomba kutounga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Nimrod Mkono. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ephraim Madeje wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Tatu Ntimizi.

MHE. EPHRAIM N. MADEJE: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu, kuchangia katika mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, kwa hotuba yake nzuri, lakini hasa kwa kazi yake nzuri, ambayo amekuwa akiifanya tangu aje katika Wizara hii. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri wake, ndugu yangu Chibulunje, Katibu Mkuu katika Wizara hii kijana wetu Chambo na Watendaji wote, ambao wamefanya kazi kubwa sana katika kutayarisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na nimekuweko huko tangu mwaka 2006, wakati awamu hii inaanza. Timu hii ambayo nimeitaja; ni watu ambao wanajituma sana na wanafanya kazi nzuri, lakini zaidi *experience* yangu katika Kamati hii ni kwamba; ni watu ambao ni wasikivu na nina imani kwamba, yote yale ambayo tumechangia na tunaendelea kuchangia, watayasikiliza kwa makini na bila shaka watachukua hatua za kuweza kurekebisha pale ambapo kuna hitilifu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie tatizo la kupanga miradi ya maendeleo katika Wizara hii ya Miundombinu. Kama tunavyojua, miundombinu ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yoyote, lakini pia inagharimu fedha nyingi sana, rasilimali nyingi sana na rasilimali watu. Kwa hiyo, hawa wenzetu wana kazi ngumu sana, lakini kwa bahati nzuri, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, imeelekeza kwa kiasi kikubwa, wapi tuelekeze nguvu zetu katika kujenga miundombinu na katika hili nasemea barabara mbili; ile ya Dodoma - Iringa na Dodoma - Babati, lakini nitakuja huko baadae kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye maeneo ambayo yanahuwanu Wananchi wangu wa Dodoma. Kwanza kabisa, naomba niishukuru Wizara hii kwamba, wamekamilisha zoezi la kulipa fidia kwa Wananchi wa Msalato na Chiteleta, ambao kwa muda mrefu sana walikuwa wanalia kutokuwa na maendeleo kwa sababu walikuwa hawajalipwa fidia. Nashukuru sana katika hilo. Baadhi yao wamekuwa wakilalamika kwamba, hawakulipwa fidia kama ambavyo walikuwa wamestahili. Najua kwamba, sheria zipo na utaratibu upo na inawezekana kabisa upungufu uliotokea ni kutokana na utekelezaji. Kwa hiyo, naomba Wizara hii popote pale wanapofanya fidia, wawe makini na watendaji kwa sababu hawa ndio mara nyingi wanatusababishia malalamiko ambayo huwa si ya kimsingi.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo naomba Wizara hii iangalie suala la fidia kwa wale watu ambao wataondolewa kutokana na barabara itakayojengwa hapa Mjini Dodoma kati ya *Roundabout* ya Shabiby na *Roundabout* ya Arusha Road. Watu hawa wamekuwa katika kutokujua hatma yao tangu mwaka 2004, walipoambiwa kwamba watahamishwa, lakini hadi hivi leo hawajaelezwa vizuri au hawajajua kitu gani kitakachofanyika. Aidha, naomba kuishukuru Wizara hii kwa ujenzi wa Barabara ya Dodoma hadi Manyoni. Ujenzi huu ulikuwa umesimama kwa muda, lakini nashukuru sasa kwamba, mkandarasi mpya amepatikana na kazi hiyo inaendelea vizuri.

Vile vile naishukuru Wizara kwa kuzipandisha daraja barabara mbili katika Wilaya yangu hii ya Dodoma Mjini, nazo ni Barabara ya Ihumwa kuititia Hombolo kwenda Gawaye, imepandishwa kuwa ya Mkoa. Vile vile Barabara ya kutoka Mkonze kuititia Bihawana kwenda Mbabala na kuelekea kwa ndugu yangu Kusila, nayo pia imepandishwa daraja. Hii itatusaidia sana katika kuhakikisha kwamba, kuna ubora wa kuaminika katika hizi barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie Barabara ya Dodoma - Babati. Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009, barabara hii ilitengewa shilingi bilioni 12. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha na kwa taarifa za uhakika, hata senti tano kati ya hizo fedha zilizokuwa zimepangwa zilikuwa zimetumika. Kwa maana hiyo ni kwamba, hakuna kazi ambayo ilikuwa imefanyika. Wakati fedha hizi zinatengwa baada ya bajeti iliyopita, sisi Wananchi wa Dodoma, tulifurahi sana na kama wanasiwa tulipiga debe sana na tulipiga kelele sana kwamba, sasa barabara inajengwa.

Naomba Waziri atueleze kitu gani kilitokea, kwa sababu sisi tutaonekana ni waongo, tumezusha kitu ambacho hakipo na pia tungependa hiyo shilingi bilioni 12 pamoa na kwamba haijatolewa mpaka sasa hivi, iingizwe katika ujenzi wa barabara hiyo.

Katika bajeti ya mwaka huu, barabara hii imetengewa shilingi bilioni 5.6. Kama kweli nia ni kujenga barabara hii, tulitarajia kwamba, kungekuwa na nyongeza ya fedha katika bajeti inayofuata kuliko kuwa na punguzo. Kwa hiyo, hapa pia tunauliza; je, nia hiyo ipo? Tunaomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Barbara ya Iringa - Dodoma katika bajeti hii imewekewa shilingi milioni 20 tu. Najua inawezekana kwamba, hiyo fedha imewekwa kwa ajili ya kulinda kasma kwamba, hakuna kinachotokea katika mwaka wote huu unaokuja. Tunaomba sana tukumbuke kwamba, barabara hii iko katika Ilani na kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami au itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami katika kipindi hiki kabla ya mwaka 2010. Sasa hivi sidhani kama muda upo, tuna nusu mwaka kabla ya uchaguzi ujao, kabla ya ahadi ile ya Ilani haijaishia muda wake. Kwa hiyo, tunataka kujua Serikali iko *serious* katika kujenga hii barabara?

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Iringa – Dodoma – Arusha ni sehemu ya barabara ambayo ni ya kihistoria na ya Kimataifa. Barabara hii ilikuwa inaitwa The Cape to Cairo Road hata sasa hivi nadhani inaitwa hivyo hivyo. Kwa bahati mbaya au kwa masikitiko ni kwamba ni sehemu hii kati ya Iringa, Dodoma na Arusha, ambayo bado haijawekewa lami. Wenzetu wote ukitoka huko South Africa ukipita Zimbabwe ukaja Zambia, Kenya kuelekea Cairo, wote wameweka lami katika hiyo barabara. Kwa hiyo, hatupigi kelele kwa sababu ni barabara ya leo au ya jana; ni kati ya barabara kongwe katika nchi hii, lakini bado haijawekewa lami.

Mheshimiwa Spika, pia ukweli ni kwamba, Waingereza wanasema *a straight line is the nearest distance between two points*. Kwamba, mstari ulionyooka ndio una umbali mfupi kupita yote ile kati ya sehemu mbili. Ukitoka Iringa unataka kwenda Arusha hivi sasa, magari yaliyo mengi; mabasi na yale yaliyobeba mizigo kama mbao na vitu vingine, inabidi yazunguke kupitia Morogoro – Chalinze – Korogwe – Moshi hadi Arusha.

Huo ni mzunguko, lakini mantiki inasema kwamba, tungepita Dodoma kutoka Iringa – Dodoma – Babati – Arusha utakuwa umeokoa umbali mkubwa sana. Ukiungeza umbali kwenye mambo ya usafirishaji, unaongeza gharama kwenye mafuta, uchakavu wa mitambo yenye kwa maana ya magari na kadhalika. Hivi vyote sisi hatuvizalishi katika nchi hii, tunaagiza kutoka nje. Kwa maana hiyo, sehemu fulani ya umaskini wetu, unachangiwa na gharama ambazo sio za muhimu kutoptana na barabara hii. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara iangalie suala hili ili hii barabara ijengwe na sisi tunadai kwa sababu barabara hii ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, aidha, barabara hii ikijengwa, itaongeza Biashara ya Kimataifa kati ya Kaskazini mwa Afrika na Kusini mwa Afrika. Kenya wanafanya biashara kubwa sana na watu wa Afrika ya Kusini. Hivi sasa nafikiri biashara nyingi inapitia kwenye meli, lakini barabara hii ikikamilika, bila shaka usafiri utaongezeka na usafirishaji wa mali utaongezeka. Mimi naomba nisisitize kwamba, barabara hii ni muhimu katika maendeleo ya nchi na pia ni muhimu katika maendeleo ya sehemu ya kati ya nchi ambayo ni Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye suala la ujenzi wa barabara za hapa Dodoma Mjini. Katika kipindi cha miaka miwili hivi iliyopita, tumebahatika kuongeza barabara ambazo ni za kiwango cha lami hapa Mjini na sehemu kubwa ya barabara hizo zimejengwa na TANROADS. Teknolojia ambayo wametumia ni ile ambayo wanasesma ni *surface dressing* na bila shaka, Wabunge walio wengi wameshuhudia kwamba, hali ya barabara zetu, pamoja na kwamba zinajengwa mara na mara, nyingine zinafumuliwa na kujengwa tena, sio nzuri sana. Tunaiomba TANROADS wabadilishe teknolojia inayotumika kwa barabara za hapa na watumie teknolojia ambayo katika miji mingine inatumika. Mimi sio mtaalamu wala sio *engineer*, lakini naambiwa sijui kuna *premix* badala ya *surface dressing*, hiyo ndiyo barabara ya uhakika na sisi tunaomba kwa Dodoma na kwa hadhi ya Dodoma kama Mji Mkuu Mtarajiwa wa Serikali ya Tanzania, nadhani tunatakiwa tujenge barabara za kudumu na za uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana mwenyeji wetu wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Madeje. Sasa namwita Mheshimiwa Tatu Ntimizi, wakati huo huo Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda ajiandae.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana leo kuniona. Kabla sijaanza, naomba na mimi nitoe rambirambi kwa Marehemu Alhaj Sheikh Suleiman Gorogosi, alikuwa kiongozi mzuri katika dini yetu, Mwenyezi Mungu, amlaze mahali pema peponi. *Ina lillahi waina illaifi rajiun.*

Mheshimiwa Spika, nianzie na reli, najua wamepewa shukrani Mawaziri hawa wanaofanya kazi vizuri, lakini yaliyo ya muhimu tuyakosoe hapa hapa. Sijui nianze kulia kidogo kama Nkumba. Mheshimiwa Spika, sijui nianze kulia?

WABUNGE FULANI: Lia!

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mimi nafikiri Tabora na Kigoma hatutendewi haki. Wenzangu wamezungumza sana kuhusu reli, sizungumzi kwa jazba, lakini nazungumza kwa uchungu kwa sababu nikianza kulia mtaacha kusikiliza ninalotaka kuzungumza. Reli ya Kati ilivyo hatari kwa sisi wasafiri; robo tatu ya Reli ya Kati katika Mkoa wa Tabora inapita kwenye Jimbo langu la Igalula.

Barabara hatuna, usafiri ni huu wa reli, hata wapiga kura wa Mheshimiwa Msindai na Missanga, wanakuja katika maeneo ya stesheni ambazo ziko katika jimbo langu. Mambo yanayotokea, nikueleze ukweli; hawa ndugu zangu treni zinaanza kugongana za mizigo kwa sababu injini mbovu. Mnataka tufe sisi au mafuta yanayopelekwa na hayo magusi yapate moto ili wananchi walio karibu na reli wapiga kura wangu wafe?

Mheshimiwa Spika, kama kweli treni mnataka zifanye kazi injini mbovu, sasa cha ajabu wiki iliyopita Mheshimiwa Spika na wewe mmojawapo, watu wako walikuwa

kwenye train ile wamekuja na abiria ilikuwa Siku ya Jumatano, baada ya kutoka Dodoma kufika Kintinku, treni ikasimama ghafla; la abiria sio la mizigo; kuna nini eti mafuta yamekwisha kwenye injini! Kama nasema uongo, mimi naomba Waziri anieleze kama hili halikutokea na bahati mbaya kulikuwa na dada yangu anakuja.

Nimekwenda stesheni nasema mbona treni haiji wanazunguka, jamani niambieni mimi ni Mbunge, wanasema mama tunakunong'oneza, injini imekosa mafuta ndio tunafanya utaratibu wa kuchukua mafuta tupeleke.

Mheshimiwa Spika, tumefika mahali hapo; kweli nikilia si itakuwa ni haki yangu? Hebu nitafute kitambaa nilie kidogo kabla sijaendelea.

SPIKA: Kanuni hazikuruhusu.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Saa nyingine kanuni ziruhusu kwa sababu hebu niambie, wamekesha pale wamekaa saa nane za usiku ndio wameingia hapa Dodoma, kuanzia saa 1.30 wako porini; kuna fisi chungu nzima katika maeneo hayo, watoto wanalia, maji hamna kwenye treni, injini imekosa mafuta; tunafikia hatua hiyo kweli ya kukosa mafuta, haijapata kutokea? (*Makofi*)

Mimi napenda sana kuzunguka katika treni hii mabehewa ya *First Class* na *Second Class*. Siku moja nilipomaliza Bunge kipindi kilichopita, nikapanda treni kwenye *First Class* kutoka Dar es Salaam, kabla sijaingia pale nikapiga dawa kidogo kumbe nilikosea. Nilipolala kufika Buguruni pale tukasikia mlion wa ajabu ikasimama treni, wakakorokochoa korokochoa karibu na behewa lile nililokuwa nimepanda, wakasema kuna pampu imefyatuka, wakafunga na kamba za katani, mimi shahidi tukaondoka; kufika Buguruni ndio treni likaanza kupiga kelele bububu eeh, eeh watu wanataka kuruka, tukaambiwa pampu imekatika walikuwa hawakufunga vizuri.

Mheshimiwa Spika, ikabidi sasa ije injini nyingine ituvute kuturudisha Dar es Salaam taratibu, tulipofika pale tumeondoka saa 7.00 za usiku. Kwa sababu wafanyakazi hawana motisha, hakuna wanachocheki, wanaauza mpaka spea, Menejimenti inauza mabehewa yale machakavu mpaka spea wanaauza. Hata mafuta nasikia wamekataliwa kwamba, hawaruhusiwi kuchukua kwa sababu wana madeni, tukarudi. Bahati nzuri nilikuwa na kijukuu changu kina miaka miwili; bibi mbona tunarudi nyuma, nikamwambia wewe vumilia tu ndio hali yenyewe. Halafu mnasema hawa Wahindi, mimi siwalamu Wahindi peke yao, tuna asilimia 49 ambayo lazima sisi Watanzania tuiangalie hao walioko pale wanafanya kazi gani?

Wahindi wapo na hawa wengine wanafanya kazi gani, wamekaa pale kungoja sasa wamepata *advantage* kwamba si wamekuja Wahindi kwenye Menejimenti tuwaone? Menejimenti ni sisi wenyewe, ndio tunauza vitu vyote hapa, mabehewa yamekuwa vioski hawana uchungu hawa waliobakia; ondoa wote basi. Ondo Wahindi na hao wengine Waswahili wenzetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Tito, alifanya kazi peke yake, lakini hana wasaidizi. Wafanyakazi hawasaidii, wame-take advantage hawa Wahindi kuja; shilingi ina *both sides of the coin*, sisi wa kulaumiwa na Wahindi wanalaumiwa. Sasa tunalitazamaje hata mkileta mamilioni katika hii reli kama Menejimenti hamjaitengeneza vizuri hakuna kinachofanyika, mnataka tufe sisi sio?

Wewe Naibu Waziri, kwani Wagogo wanatembea na nini si kwa mguu tu wanaingia Dodoma na wewe Kawambwa si kuna barabara huko Bagamoyo; mna uchungu na wapiga kura wa Tabora au wa Igalula? Kama hamuwezi ku-manage Menejimenti hii, sasa nyinyi mtakuwa Mawaziri kwa namna gani? (*Makofi*)

SPIKA: Elekeza kwenye Kiti.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru nawaambia hawa watoto. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, basi nimekuja na hiyo treni adha ya kwanza kurudi Dar es Salaam, adha ya pili baada ya kulala, kufika Kilosa nikaona niamke; nilipoamka hivi panya wameniuma kwenye vidole vyangu. Mende ndio nimewatimua kutokana na hiyo dawa. Shuka tunayojifunika rangi ya kahawia sio nyeupe tena na nimelipia *First Class*, hata shuka pia zinashindikana kuleta katika mabehewa.

MBUNGE FULANI: Uwe unabeba zako.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Nitabeba zangu mpaka lini? Mto wenyewe huulalii, punguzeni tuwe tunakata tiketi ya *Third Class* wote, hata wale amba wamo katika *First Class* haina sababu; panya wamo, kunguni wamo, nzi tele, chawa tele, sasa mende ndio sisemi wanaingia mpaka kwenye chai wanayotuletea kunywa.

Sasa nini maana ya kuwa na Menejimenti? Menejimenti inafanya nini, Mhindi aje anisafishie chumba, ninyi Waswahili mnafanya nini? Kwa kweli sijui; nasema jamani halafu wafanyakazi mmewapunguza, kweli tunajua mmewapunguza mnajipanga; mnajipanga kwa miaka mitatu?

Stesheni zimekuwa magofu. Katika kuhamasisha barabara na reli, mnasema kwamba, ulinzi wa umma walinde reli hii, wafanyakazi wote hawapo. Majambazi wamekaa katika yale magofu na treni zinasimama maporini hazina mafuta, wanawenza kutoka hawa watu kuja kutuvamia katika treni, mnataka tuibiwe sisi hela kidogo tulizonazo?

Mheshimiwa Spika, ninyi mnapanda treni, mwaka jana nilimwambia Waziri Mkuu, ilisimama treni kukungoja wewe upite ungesimama uone watu wako wa Mpanda wanavyohangaika na ninyi vijana wangu naomba hawa wa Maziwa huyu hajapanda treni. Hii Menejimenti wakianza kupanda wanapewa shuka mpya, wanahakikisha lile behewa analopanda Mkurugenzi sijui nani halikutoboka, wanampigia dawa na mimi ninayelipa

kukuwezesha wewe kupata huo mshahara sistahili heshima hiyo! Hii reli mnaifanya nini, yaani hebu nilie tena kidogo.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi mwezi uliopita hawakupewa *overtime* wanaambiwa fedha hakuna, taarifa nilizonazo wanasema; *Don't trust copy even if he is dead you remain with a copy*. Nimefanya utafiti mwezi wa jana zimeibiwa shilingi bilioni 10 kwenye akaunti yao.

Sasa naomba kabla hawajamaliza, wanieleze hizi shilingi bilioni 10 zimeibiwa na nani? Wafanyakazi *overtime* ya mwezi wa jana hawakupata zimeibiwa, nawaambieni hizi taarifa nina *source of information* yangu na nina uhakika zimeibiwa. Wafanyakazi hawapati *overtime* watakuwa wana motisha ya kufanya kazi? Sisi tungekuwa hatupati posho ya kikao, tungekaa hapa Dodoma na baridi yote hii?

MBUNGE FULANI: Thubutu!!!!!!!

MHE. TATU M. NTIMIZI: Sasa hawa wanyonge kwa nini hamuwapi *overtime* yao? Anaingia asubuhi saa 11.00 hatoki mpaka jioni au mpaka treni itakapoingia kama wale wa siku ile mafuta yamekwisha, imebidi badala ya kuondoka saa 12.00 au saa 2.00 asubuhi waliondoka saa 10.00 usiku.

Overtime mnawaambia hatuwapi kwa sababu hela zimeibiwa. Zimeibiwa, mimi najua nani ametajwa katika wizi ule lakini hapa sisemi. Naomba mtueleze nani ameiba shilingi bilioni 10 kwenye akaunti yenu; mwenye *access* ya kuingia kwenye akaunti na kuchukua hizo hela nani kama hamumjui, kama sio Menejimenti, Waziri utuambie kama ninyi mmehusika mseme tu hapa tutawasamehe, lakini naomba nielezwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba hii treni ya *express* nimesema wapiga kura wengi wa majimbo ya karibu wanapandia katika stesheni ambazo ziko katika jimbo langu. Naomba hii *express* hawa Waha, Wasukuma na Wanyamwezi, mnajua kwamba tunachukua viporo tunakwenda navyo kwenye treni, lakini viporo vyenyewe vinaoza kwa sababu treni haifiki kwa wakati. Hii *express* naomba iwe inasimama Igalula, hapo ndio watu wengi pia amba wanapandia na vile viporo vyetu tunavyo.

Mabehewa yaliyokuja na hawa wawekezaji, naomba siku moja mimi na wewe tupande treni hii ya *Third Class* uone zile nondo, utafikiri mabasi ya Magereza yanayochukua wafungwa. Sponji ndio nzuri bado mpya, lakini imewekwa nondo; *Allahu Akbar!* Leo ikianguka hiyo treni hakuna kutoka mle ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa ndio stahili mlizokwenda kupendekeza ninyi mliokwenda kufanya uwekezaji na ndio aina ya mabehewa mnataka kutuletea, hayo ya nondo kwani mmeambiwa sisi wafungwa au majambazi kwamba tukisimama tutavunja mabehewa?

Hivi nondo ndio stahili kweli ya kumpakia binadamu? Hata wafungwa wenyewe wanachukuliwa dakika 10 wameshafika, sisi kuanzia Jumatatu mpaka siku nne hatujafika Tabora, kwa sababu mafuta hamna, injini imekwama haya mabehewa yenu mkayarudishe.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni barabara ya Itigi. Kwa kweli asilimia 94 ya barabra ya Itigi inapita kwangu Igalula. Katika Ilani ya Uchaguzi tunesema na mimi naiheshimu sana Ilani kwa sababu ni ya Chama changu, mara inaanza Itigi kilomita 74, Tabora kilomita 74, mimi nasema msianze kokote kule, tuwekeeni changarawe angalau tupite, kwa sababu lami ni kilomita 80, hivi kweli huo ndio utakuwa ufanisi wa barabara? Kwa taarifa yenu hata, aah, jamani basi ngoja nilie kidogo ahsante!

(*Hapa Mhe. Tatu M. Ntimizi Alilia*)

SPIKA: Ukijisikia kulia unaweza kwenda nje kidogo, pole sana.

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu, wenzetu wa Kambi ya Upinzani, kwa hoja yao, nimewapandisha kidogo, kwa hiyo, Mheshimiwa Arfi atakuwa mse maji wa sita na Mheshimiwa Sakaya atakuwa mse maji wa kumi, hivyo ndivyo tutakavyochanganyika. Sasa namwita Dkt. Sigonda, ametoka, sasa tunaingia kwa wale waliochangia mara moja, namwita Mheshimiwa Lucas Selelii.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

SPIKA: Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, ujiandae.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza wenzetu wa *TANROAD* ambao katika Mikoa yetu, wanafanya kazi nzuri. Mimi Mara nyingi ninapongeza, ujue pongezi zangu ni za dhati. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kutoa angalizo, *TANROADS* wanapokuwa wanafanya kazi na hawa wawekezaji wawe waangalifu sana na hasa wanapotaka kuchukua hatua za kukatisha mikataba kwa sababu Wakandarasi wengi ni wa nje na ni wajanja, wanaweza kukugeuzia kibao wakati wowote ukaingia hasara. Lakini wawe waangalifu vile vile kwa kuhakikisha Wakandarasi ambao ni wabovu wanafukuzwa mara moja kabla hawajatufikisha mahali ambapo ni pabaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, juzi, Waziri alitoa idadi ya barabara, nashukuru kwa zile ambazo katika Mkoo wetu wamezipandisha, lakini zipo ambazo kwa kweli hawakuweza kuzizingatia kwa mfano barabara inayotoka Nzega kwenda Kahama ambayo ndiyo *original T-Three* badala ya kubaki kwenye *track road* imeshushwa na kuwa *regional road*, kwa kweli ni jambo baya, hatukulipenda. Lakini ili kutuliwaza, basi hiyo nayo ianze kufikiriwa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu naamini hata baadaye hiyo ndiyo itakuwa *T-Three* kwa sababu ukifika pale Nzega hakuna haja ya kwenda mpaka

Tinde baadaye ndio uende Kahama, ukikatiba pale Nzega kupitia Itobo unafika Kahama kwa urahisi zaidi na ni karibu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ipo barabara nyingine ambayo tulipitisha kwenye *RCC*, inapita katika Mikoa mitatu, ya kutoka Mpanda, kupitia Ugala, Kaliua, Ulyankulu, Kashishi mpaka Kahama, nayo haikuzingatiwa kwani barabara hiyo ni barabara ya kiwango cha Wilaya. Kwa hiyo, ninaomba na barabara hii izingatiwe na kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia kwenye ofisi ya Waziri Mkuu, nilizungumzia juu ya barabara ya Chalinze – Segera - Tanga na niweke tu mambo sahihi. Mimi niliona busara zaidi kama ingezingatiwa barabara ya kutoka Chalinze - Kibaha - Dar es Salaam ambayo ndiyo ina *traffic* kubwa zaidi na inapitiwa na magari mengi zaidi kuliko ile ya Chalinze – Segera - Tanga.

Mheshimiwa Spika, nipende kukubaliana na mwongozo wako ulioutoa, nauheshimu na kwa mujibu wa Kanuni zetu, siwezi kuujadili wala siwezi kuhoji, jinsi ambavyo umeona, mimi nakubali ni sahihi na pesa hizo kweli umeziona, nakubali, lakini hivi hawa ndugu zetu kwa upande mwingine wamekuwa na Bunge lingine? Mimi najua Bunge hili ni mmoja.

Mheshimiwa Spika, siku ile, Waziri alisema umetumia busara na mimi nimekubali kweli ultumia busara kukubali yaishe na mimi nimekubali yameisha. Lakini mbona sasa juzi nimekuandikia barua, bahati mbaya na nasikitika Makatibu bado hawajanjibuu, nimeandika barua siku ile ile ambayo waliiingia mikataba ya barabara ambazo sisi hapa ndani hatujawahi kuzijadili hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mzoefu kwenye Bunge hili, miaka 15 nimo humu ndani, hakuna hata siku mmoja tumejadili kupandisha barabara hizi kwa kiwango cha lami. Sasa hapa napo inahitajika busara yako tena, hapa hawa jamaa wameingiza barabara kiujanja ujanja, hakuna siku ambayo tumejadili juu ya barabara hizi za Korogwe, Handeni, Dumila, Kilosa, Mikumi, nimetoka *Hansard*, nimeangalia hakuna! Kwa nini sasa leo waje waseme tumeingiza shilingi milioni 100, tumezigawia hizi barabara na sisi tumekubali, labda kuna Mabunge mawili lakini mimi naamini Bunge letu hili hatujawahi kujadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana busara uliyotumia kwa Chalinze, mimi sihoji, ni sawa, inawezekana na hili hapa wametumia pesa bila sisi Bunge kuidhinisha. Hivyo basi, kama wanatumia Bunge hili tuidhinishe miradi ambayo haipo na wameingia mikataba, wametutendea vibaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naungana mkono na Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, amesema jana ataleta *Schedule of Amendment* na ninaomba Wabunge wote tumuunge mkono kwa sababu Kanuni inaturuhusu. Naomba barabara hizi ziondolewe na ziwekwe barabara ambazo tumezipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima hiyo, ninapenda barabara zinazoingia na kutoka Dodoma, ziwe za kwanza kwa heshima ya Dodoma. Tumekubaliana hivyo kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu, leo wanakuja watu sijui kutoka wapi wanabadilisha, wanasahau hata historia ya Dodoma! Naomba barabara ya kutoka Iringa kwenda Dodoma, Dodoma kwenda Babati ziwekwe kwenye bajeti, tufute hii barabara ambayo imeingia kinyemela, tuiondoe! Ninamwomba Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, aandike hiyo *Schedule of Amendment* na barabara ya kwanza iwe Iringa – Dodoma - Babati. Barabara ya pili kwa sababu ya umuhimu wa Dar es Salaam, sisi sote tunakwenda Dar es Salaam. Ninapenda kumwambia Mheshimiwa Maneno, sisi wote hata utoke wapi lazima utaenda Dar es Salaam pamoja na kwamba Dodoma ni Makao Makuu lakini Dar es Salaam ndiyo Mji Mkuu. Tuweke barabara kutoka Chalinze - Kibaha - Dar es Salaam, tuachane na hizi barabara za kwenda kwenye Wilaya, hilo ndilo pendelekezo langu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba sisi tulilalamika sana mwaka jana, wewe ni shahidi, tukasema kwamba Tabora mnatutende vibaya, hamtutendei haki. Akasimama Waziri Mkuu, akaahidi kwamba atatoa shilingi bilioni 10. Kwenye kitabu tumeona mwaka jana wametenga shilingi bilioni 6.7 kwenye barabara ya kutokea Manyoni - Itigi – Tabora, hatuna maneno nayo, tunachotaka kwa umuhimu wa Tabora mwaka huu pia watenge hela kwa barabara za kutoka Tabora - Nyahua, Tabora – Urambo - Kaliua kwa sababu barabara hii ni ndefu haiwezekani ikawa na Mkandarasi mmoja tu akaimaliza. Naomba watenge pesa hizo na ningeomba tuzione wakati ana-wind up, ili tuzione kwenye vitabu vya hesabu, haitoshi kuziona tu kwenye kitabu cha hotuba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningekuomba sana uweze kukubaliana na naukubali kabisa mwongozo wako, wala sikubishii na sikatai, lakini ikitokea mikataba hii imeingia katika fedha hizo walizoziomba kwenye Bunge hili la mwaka huu, tuzifute na liwe fundisho kwa miaka ijayo, wasije wakafanya mchezo wa namna hiyo wa kulidharau Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwa haraka kwa sababu muda hautoshi, niseme kwamba inasikitisha sana jinsi *ATCL* inavyofanyiwa. Shirika hili kubwa ambalo lingefanya kazi kubwa sana kuongeza uchumi hasa kwa kuleta watalii, linanyimwa mtaji. *ATCL* wameomba shilingi bilioni 20 lakini wamepewa shilingi bilioni moja, hivi kweli tupo makini kuhakikisha kwamba shirika hili tunalirudisha katika hadhi yake? Naomba Serikali iamue kwa dhati na kwa kweli kama unataka kuimarishe utalii na unataka kufanya biashara ya utalii, ni lazima uwe na shirika lako la ndege.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye reli, hapa ndipo kwenye matatizo. Amesema dada yangu, Mheshimiwa *Tatu Ntimizi*, namuunga mkono lakini mimi nasema kwamba tungejenga reli tungeokoa barabara kwa sababu sasa hivi magari mengi yanapita barabarani kwa sababu ya ubovu wa reli. Tungeimarisha reli, tukaibadilisha kutoka paundi sitini ya sasa tukaweka paundi themanini, mia moja ingetusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais, juzi alipokuwa anatuhutubia alisema kwamba anatenga shilingi bilioni themanini kwa ajili ya kuimarisha reli, nashukuru sana na ninampongeza. Lakini kwa menejimenti hii iliyopo sasa ya Wahindi, asiwape kwanza, asubiri kwanza, hawa Wahindi wameshindwa. Angalia migomo iliyopo, angalia matatizo yaliyopo, Mheshimiwa Tatu Ntimizi amesema, wameshindwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hapa kuna matatizo, hawa jamaa ni wahujumu uchumi, wamekuja hapa kuhujumu, wana lao jambo. Naomba Mheshimiwa Rais na Bunge lako, wasubiri kwanza huu mkataba urekebishwe ndipo waweze kuweka pesa hizi, hawa wana matumizi ya juu na ya ajabu sana. Wanatumia pesa za nchi yetu kwa kudanganya, wanatumia pesa kwa kujiita wao ni wawekezaji, wawekezaji gani ambao hawawezi kukopesheka? Wawekezaji gani ambao hawawezi hata kukarabati reli yetu? Mheshimiwa Waziri atakapomaliza, ahakikishe watu hawa tumewafuta wasiwepo kabisa.

Mheshimiwa Spika, juzi wamesafirisha injini kutoka India, kwanza mkataba ule wa Wahindi wakaingia na msafirishaji Mhindi mwenzao, kusafirisha Injini moja kutoka India kwa dola 30,000 lakini Injini hizo tumezikodi 25 kwa miaka mitano tumewalipa shilingi bilioni 33 pesa ya Kitanzania, kumbe pesa yetu tulikuwa nayo. Isitoshe, injini hiyo kila siku tunailipia dola 650 ifanye kazi isifanye kazi sawa na shilingi 800,000 kwa siku, yale yale ya *Richmond* na *RITES*, ni ubadhirifu, ni wizi, ni uhujumu.

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, hizi injini ambazo zinakosa mafuta, ni Injini za miaka ya 1960, tulikuwa na *TRC* yetu, tulikuwa na injini za Canadian za miaka ya 1970, tulikuwa na *TRC* yetu, tulikuwa na injini za miaka ya 1992, hawa wametuletea injini hizi za kokodi kwa sababu sisi sijui tunaogopa mikataba, injini hizo ni ndogo, zina *horsepower* 1,500 wakaacha hizi zetu kubwa za *horsepower* 2,000, wanazing'oa, wanaenda nazo India. Hawa ni wahujumu, hawa wana lao jambo na mimi napendekeza kwa kweli mkataba huu uvunjwe mara moja, hakuna kigugumizi juu ya suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunakodi hata mabehewa ya kwao? Haya mabehewa ambayo yanawekewa nondo, ni ya kukodi, kila mwezi behewa hizi zinalipiwa dola 3,500, ukipiga hesabu ya mapato ya behewa hizo ni shilingi milioni sita, kwa hiyo pesa yote unayokusanya ndiyo hiyo unayolipa kwenye *TRC*, mkataba gani wa namna hii? Tufike mahali ambapo tuamue moja.

Mheshimiwa Spika, pale walipokuwa hawajafika wao tulikuwa tunasafirisha tani milioni moja na nusu kwa mwaka wao wamekuja wameshusha sasa hivi tunasafirisha tani laki nne kwa mwaka, hawafai, hawawezi, hawatufai, waondoke mara moja. Mimi nawaaahidi, Mheshimiwa Waziri, kama atashindwa mwezi wa kumi na mmoja, mimi nakuja na Muswada Binafsi, nilishawishi Bunge lako, naamini nitaungwa mkono na Wabunge wengi ambao tunahangaika na usafiri huu ili ivunjwe mara moja na mkataba huu waweze kutulipa kwa sababu wameshatuibia vyakutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi nataka nitoe muda kidogo sana kama dakika mmoja ama mbili, unipe mwongozo, hii mikataba ambayo wamesaini juzi, ni pesa za mwaka jana au ni pesa za mwaka huu? Kama ni za mwaka jana, mimi nakubali sina tatizo lakini kama ni za mwaka jana kwa nini wameomba tena kwenye Kitabu cha Maendeleo mwaka huu, mimi napata mashaka. Natoa dakika mmoja, unipe mwongozo wako, uniambie hizi pesa ni za mwaka jana kwa sababu tangu juzi nilikuandikia ili nipate uhakika. Kama ni za mwaka jana, nitakubali tuendelee kujadili, kama ni za mwaka huu, hakuna haja ya kujadili kwa sababu kwa mujibu wa Sheria yetu na Kikatiba inasema, Bunge ndiyo linaruhusu matumizi na mipango yote ya Serikali!

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lucas Selelii. Tunaendelea Waheshimiwa, kwa hatua hii, hakuna haja ya mwongozo, hilo nitalifanya kazi, baadaye tutazungumza.

Sasa ni Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilson Masilingi ambaye hayumo ukumbini, kwa hiyo ajiandae Mheshimiwa Juma Killimbah.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na ili na mimi nichangie Wizara hii ya Miundombinu. Nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana bajeti hii, sehemu nyingine zina dosari ambazo zitarekebishika lakini sehemu nyingine imekwenda vizuri sana. Nikianza na Jimbo langu; naishukuru sana sana Serikali kutoa fedha za kujenga daraja la Mto Sibiti. Kama nilivyosema huko nyuma, mafuriko kwenye bonde la Sibiti, yanaanza mwezi Novemba mpaka mwezi wa Mei mwaka unaofuata. Kwa hiyo, naomba sana wahusika watangaze tenda hii mapema na kwa sababu fedha hizi zinazotumika ni za hapa ndani na ndiyo tunazipitisha, ujenzi wa daraja hilo uanze. Daraja hilo ni mlango na ni mkombozi kwa watu wa Singida hasa wa Iramba Mashariki na wa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga na kwa upande wa pili Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera. Hii njia ni muhimu sana na napongeza kwa sababu daraja tayari limeshajengwa Bariadi Mashariki kwenye Mto Simiu, kwa hiyo, itakuwa rahisi hata kwenda Mara na maeneo haya yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, napongeza barabara hii ya kutoka Iparandoto – Lalago – Mwanuzi – Iramba Mashariki na kuelekea Mkao wa Arusha, kupandishwa hadhi na kuwa barabara ya Taifa. Nawapongeza sana na mtaona faida ya barabara hii baada ya kipindi kifupi sana. (*Makof*)

Vile vile, niipongeza sana Serikali, imesikia kilio chetu cha Iramba Mashariki. Sisi tulikuwa na matatizo sana kwenda Wilayani, ilikuwa mpaka uzunguke Singida lakini tunashukuru kwa kupandishwa hadhi barabara iliyokuwa ya Halmashauri kutoka Kiomboi – Kisiriri - Kidauri – Ibaga – Mkalama - Nghinto mpaka Kidarafa, tunashukuru sana. Kwa sababu sasa imechukuliwa na Mkao, tunaomba mwaka huu ianze kutengenezwa. Ni ukombozi mkubwa kwa sababu huku inaunganisha Mikoa ya Tabora, Kigoma na upande wa pili ni Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Lakini niombe kwa kipindi

kinachokuja sasa, barabara ya kutoka Ibaga - Tulia -Mingera - Shelui nayo iwe ya Mkoa, itakuwa imesaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu alipotembelea Iguguno Kinyangiri, tarehe 4/5/2008, tulimwomba ile lami ambayo inaingia Mji Mdogo wa Iguguno, itoke na upande wa pili. Nashukuru nasikia hela imepatikana lakini tunaomba nayo ianze kutengenezwa mapema na kwa sababu ni barabara mpya, imeongeza mafuriko, nyumba za watu wa Iguguno Magharibi zinaingia kwenye mafuriko, naomba kazi hiyo waifanye mapema.

Mheshimiwa Spika, vilevile kona ya kuingia na kutoka Singida, waitengeneze. Niipongeze vilevile kwa kutenga fedha za kutosha kukarabati barabara ya Ilongero – Singa – Nduguti mpaka Gumanga, naipongeza sana. Kwa kweli Serikali yetu ya Awamu ya Nne, inafanya mambo makubwa na mazuri kwa faida ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nkungi – Kidarafa, imetengewa fedha lakini fedha hizo hazitoshi na naomba ianze kutengenzwa mapema.

Mheshimiwa Spika, mimi nipo kwenye Kamati ambayo ninazunguka sana nchi hii, Kamati ya *LAAC* na nimekaa sana Mkao wa Mara. Kwa kweli barabara za Mkao wa Mara bado tatizo sana. Naomba, kama Mheshimiwa Mkono alivyosema, ile barabara ianze kutengenezwa haraka ya kutoka Musoma –Butiama – Nyamuswa - Fort Ikoma maana ni barabara muhimu sana kwa watalii wetu. (*Makofi*)

Vile vile, niwapongeze, hivi karibuni nilikuwa Ruvuma, nawapongeza sana na nawashukuru sana, kwa niaba ya Mbunge wa Peramiho, kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya barabara ya Songea – Mkenda na Iwino – Ifinga, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tuliona kwenye magazeti, *TANROADS*, wametangaza nafasi za wawakilishi wao wa Mikoani kwamba waombe upya, je, hivi hizo nafasi zimeshajazwa? Maana bajeti ndiyo tunaipitisha leo na kama hawa watu hawajachaguliwa, nani watasimamia kazi hizo? Kwa hiyo, tunaomba sana Waziri atueleze hapa na tunasikia minong'ono kuna matatizotatizo huko juu. Tunashauri hayo matatizo yasahihishwe haraka ili kazi ziendelee. Mkianza kutafutanatafutana kwa maneno maneno, kazi hazitakwenda na Mheshimiwa Waziri umepewa dhamana ya kusimamia hiyo Wizara usisikilize ya nje, sikiliza yale yenze ukweli, yale yenze majungu achana nayo, waachie vijana wachape kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuzungumzia barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora kwenda Kigoma. Barabara hii ni muhimu sana na kwa kweli mwaka jana alitamka humu humu ndani ya Bunge kwamba shilingi bilioni 10.0 hiyo, barabara ianze kutengenezwa toka Tabora. Mwaka huu, ninachoshangaa, fedha zimetengwa na *tender* zimetangazwa barabara hiyo ianze kutengenezwa kutoka Manyoni – Itigi kwenda Tabora, jana nasikia barabara hiyo imesimamishwa, inatakiwa ianzie Tabora kuja Manyoni, maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, sisi tunaomba Serikali isiwe kigeugeu hizi fedha zilizotengwa Manyoni –Itigi kwenda Chaya mpaka Tabora, ziendelee kufanya kazi kama ilivyopangwa. Lakini tunaiomba Serikali ichukue uzito wa barabara hiyo, itafute hela zingine ianzie Tabora iungane na hii ya Manyoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka mingi tumekuwa tunasema juu ya barabara hii na kama mzungumzaji aliyepita, Mheshimiwa Selelii, wa Nzega, tuangalie, barabara ambazo haziko kwenye mpango ziondolewe zipewe hizi ambazo ziko kwenye mpango. Ni lazima Wabunge tuwe na msimamo na tunaomba sana Serikali isituburuze, isituletee maneno ya kijanakijanja huku wanatumiza, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema, zile fedha zilizotengwa kuanzia Manyoni – Itigi kwenda mbele, ziendelee na *tender* zake zitangazwe na vilevile zitafutwe fedha nyingine, jamani Tabora ni Mkoa muhimu sana, ni Mkoa wenyе historia kubwa nchini halafu Spika wetu anatoka huko. Kwa nini kwingine mnapeleka, kwa Spika hampeleki? Kwa hiyo, mimi naomba zitafutwe hela, barabara ile ienze kutengezwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga tena mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Msindai na hasa kwa kumsemea Spika kwa sababu hawezi kuongea humu ndani, nashukuru sana.

Waheshimiwa, tunaendelea na sasa namwita Mheshimiwa Juma Killimbah atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene na baadaye Mheshimiwa Arfi, simuoni ukumbini.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili namimi niwe mchangiaji katika hotuba hii ilioletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ndugu yetu Shukuru Kawambwa.

Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii na nitoe pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, lakini nisiwe mnyimi wa fadhila, napenda pia nitoe pongezi kwa Meneja wa *TANROAD*, Mkoa wa Singida, Ndugu Yusuf Kangoye. Meneja huyu tangu ujio wake katika Mkoa wa Singida kwa kiwango fulani amekuwa ni mmoja kati ya watu ambao wanatekeleza shughuli za barabara kwa umakini yuko karibu na Waheshimiwa Wabunge katika kuangalia maendeleo ya barabara katika Mkoa wetu. Mimi nampongeza sana Meneja huyu wa *TANROAD*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali, ni kweli kwa Mkoa wa Singida, kama mtakumbuka wakati tunaanza Bunge hili Tukufu mwaka 2006, wakati wa bajeti, Wabunge wa Mkoa wa Singida tulizungumza kwa kelele kubwa sana kuhusu

barabara na hususani barabara ya kati. Tuliongea kwa sababu hali ilikuwa mbaya sana. Ilikuwa mtu anaweza akasafiri kutoka Singida anakuja Dodoma akatumia zaidi ya masaa 20 na kuendelea. Lakini tunashukuru Mungu sasa ile hali japo tumbakia na eneo dogo ambapo wakati wowote, naamini kanaweza kakaisha kulingana na juhudzi zinazoendelea na ahadi inavyotekelze na Wakandarasi wanavyoendelea na kazi katika eneo hilo la Manyoni – Isuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri ambayo tumeshayapata, nitazungumzia barabara ya Jimboni kwangu inayotoka Singida mpaka Igunga. Tunakubali baadhi ya sehemu imetengenezwa vizuri lakini sehemu inayoitwa Sekenke eneo ambalo lilikuwa hatari sana; baada ya barabara kuhamishiwa upande wa pili, eneo hili limeharibika kwa muda wa mwaka mmoja. Nilikuwa nimekusudia nishirikiane na Wabunge kutoka katika Mikoa mingine ili kuweka *petition* kuipinga ile barabara. Barabara ile ina mwaka mmoja, eneo lile la Sekenke limebomoka kwa kiwango kikubwa kabisa. Sasa hatuwezi tukafika mahala pesa ambazo ni za walipa kodi, zinapotea kiasi hicho. Niliongea kwenye Kikao cha Kamati ya Miundombinu, bahati nzuri Katibu Mkuu, akanijibu akasema ile tulipata mkopo kutoka Benki ya BADEA.

Mheshimiwa Spika, lakini hata kama tunakopeshwa basi tusikiangalie na tusikitunze kile tunachokopa? Barabara imetengenezwa vibaya, eneo lile la Sekenke kwa muda mfupi limeshabomoka, zile kingo za yale madaraja yamebomoka na wala hakuna uangalizi. Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, hii kuja kujibu, ukajibu kwa haraka haraka tu humu ili kuturidhisha, kweli, tunaweza tukabanwa na Kanuni, lakini ujue kwamba unatengeneza matatizo kwa mwaka unaokuja kama utashindwa kutueleza vizuri. Majibu mnayo jibu yawe ni majibu yanayoendana na utekelezaji. Haiwezekani ukajibu, lakini ukaliacha hapa hapa na utekelezaji iwe hakuna. Mimi naomba sana muiangalie ile barabara kwa sababu inaleta aibu, barabara ambayo tumetumia pesa nyingi juzi tu, lakini tayari imeishaanza kubomoka.

Mheshimiwa Spika, wazungumzaji waliopita wamelalamika sana, nikianzia mzungumzaji wa jana, Mheshimiwa Zabein Mhita, amelalamikia kuhusiana na barabara ya kutoka Dodoma – Kondoa – Babati na akaeleza kwamba barabara hii kwa kipindi cha mwaka jana ilikuwa imetengewa pesa kiasi cha shilingi bilioni 12 ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Lakini pia malalamiko ya aina hiyo yapo kwa maeneo ya kutoka Manyoni – Itigi - Chaya - Tabora, pesa ambazo zilitengwa, shilingi bilioni 10 zinataka maelezo. Sasa hiki ni kigugumizi. Tatizo la Serikali, nafikiri haikumbuki hata ilichofanya mwaka jana ni kitu gani au imeahidi kitu gani, kwa hiyo, inapokuja mwaka mwingine wa fedha, unaingia na mipango mingine bila kuangalia ile mipango ya mwaka jana imeitekeleza kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, haya yametokea hata katika barabara ambayo wao wenywewe wameanza kuahidi toka mwaka 2006/2007, 2007/2008. Walikuwa wanazungumzia barabara yenyeye urefu wa kilomita 21 inayotoka Misigiri – Kiomboi lakini leo hii ukiangalia katika kitabu ambacho Mheshimiwa Waziri amewasilisha hapa, barabara ile haijazungumziwa, inazungumziwa kinadharia kwamba ile barabara itatekelezwa kwa

pesa za Mfuko wa Barabara kwa sababu tutazungumza na *TANROADS* Mkoa ili iweze kuendelea kuimalizia.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nauliza, katika ile awamu ambayo mlikuwa mmetuahidi, mkasema tutakwenda kwa kilomita tano tano mwaka hadi mwaka, kwa nini mwaka huu mnaiondoa wala haionekani kwenye vitabu? Jambo hili ndio maana linaleta utata mkubwa sana kwa sababu Serikali haiwezi ikasimamia ile mipango ambayo imeiainisha kwa mwaka ule wa fedha ambao tunao. Kama ingekuwa inasimamia, tukaja na mipango mingine kwa mwaka unaofuata, wala matatizo ya namna hii yasingeweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana barabara hii ni ya *TANROADS*, niliwahi kuisemea, lakini lipo eneo ambalo bado linasumbua kidogo, la kutoka Shelui – Sekenke - Konkilangi – Ntwike – Nsunsu. Eneo la Nkonkilangi, ni korofi sana na ni eneo ambalo mvua ikinyesha, barabara haiwezi kupidika, ina maana utakuwa umeua mawasiliano ya watu wanaotoka Tulya wanaokuja Shelui na watu wanaotoka Shelui wanaokwenda Tulya Doromoni kwa ajili ya kwenda kwenye samaki. Sasa pale tulikubaliana tukasema kwamba kwa sababu *TANROADS* ndio wanahuksika, sasa waweke makaravati katika eneo lile korofi ili barabara ile iweze kupidika mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, naamini barabara ile imetengenezwa, lakini siamini sana lile karavati linalowekwa eneo lile korofi la Nkonkilangi. Lile karavati linaonekana limeokotwa sehemu tu, ndio maana tunaomba *TANROADS* wasogee karibu na yule *contractor* ili waangalie kama lile karavati analoweka ni la viwango ambavyo vinawenza vikakidhi haja ili barabara iweze kutumika kwa muda mrefu. Tusiweke kwa ajili ya kuridhisha tu halafu baada ya muda fulani hali halisi ikawa barabara haiwezi ikapitika na malalamiko yakarejea kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia barabara ya kutoka Shelui - Mtoa - Mtekente – Kimbai – Ulugu - Ndago – Kibaya. Tulikuwa tumeomba, barabara hii nayo iwe ya Mkoa na tumeomba kwa kipindi kirefu sana kwa sababu barabara hii ni kiunganishi cha Iramba. Barabara hii inaunganisha na Wilaya ya Singida vijijini, inaunganisha na sehemu inaitwa Sepuka. Barabara hii, kwa wakazi waliopo maeneo hayo, kuna wakazi wasiopungua 30,000.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa kuipandisha hadhi barabara ya Kidaru kuwa barabara ya Mkoa lakini naomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na vigezo hivyo ambavyo ulivizungumzia juzi, sasa hivi barabara hiyo ina mahitaji makubwa sana au la kama mnaona haiwezekani, mzdisheshe mkono kidogo katika hizo fedha za Mfuko wa Barabara ili barabara hiyo iweze kutengenezwa kwa sababu matumizi yake ni makubwa sana. Barabara hii kipindi fulani wakati Sekenke ililetu matatizo, ndiyo ilitumika kama barabara kuu, watu waliweza kupita muda wote na kuwawezesha kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapa rai hasa watu wa Miundombinu na rai yangu inahusiana na suala zima lililoagizwa na Chama cha Mapinduzi. Kupitia

Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 - 2010, kwa ridhaa yako, nitaomba ninukuu eneo moja dogo tu linalohusu miundombinu ya kiuchumi, ukurasa wa 24 - 25. Napenda ninukuu kwa sababu ya kuwasaidia watendaji wetu ili waendane na nini CCM inachoagiza kupitia Sera zake za miaka 2000 – 2010, inasema:-

“Ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa, lazima uambatane na ujenzi wa miundombinu ya kisasa. Miundombinu ya kisasa ni pamoja na barabara za kisasa za lami na za changarawe, reli, viwanja vya ndege, bandari na mawasiliano mengine... ”.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tutakuwa na bandari mbovu, bandari ambayo tungeweza tukaitegemea ikanyanya uchumi wa nchi yetu lakini haiendelezwi. Tukawa na reli ambayo kama alivyozungumza Mheshimiwa Tatu Ntimizi, sasa ni mahutihuti, tunatafuta mwekezaji, mwekezaji anakuja anakuwa ni kero zaidi ya ile tuliyokuwa nayo sisi, hivi kweli tutafikia huu mwelekeo wa Sera za Chama chetu?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kwa kutumia utalaam wenu na mnalipwa mishahara mikubwa kwa sababu tunaamini ninyi ndio mtaipeleka nchi yetu katika maendeleo, naomba sana watendaji wetu waendane na Sera za Chama chetu cha Mapinduzi zinavyozungumza, naamini matatizo yote yataondoka. Lakini kama watendaji watakuwa wanatenda wanayoyafikiria wao, bado tutaendelea na lawama, bado nchi yetu itaendelea kupiga *mark time* na hatutafanya jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Killimbah. Namwita sasa Mheshimiwa George Simbachawene. Naona Mheshimiwa Arfi amerejea ukumbini, ndiye atakayefuatia, wakati huo Mheshimiwa James Lembeli, ajiandae.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi maana nafasi kama hizi za kuzungumzia mambo muhimu yanayotuhusu kwenye Majimbo yetu kama hili la miundombinu, unapoipata basi unamshukuru Mungu.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwanza kwa kuwapongeza na kuwashukuru watendaji wa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mpwapwa, kwa namna ambavyo wamekuwa wakipanga vizuri miradi yetu na kutumia vizuri fedha za Mfuko wa Barabara. Hali ya Kibakwe katika barabara kwa sasa si mbaya sana. Lakini hii inatokana na ushirikiano tulionao ikiwa ni pamoja na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Lubeleje na Mwenyekiti wangu wa Halmashauri ya Mpwapwa, Mheshimiwa Mkanwa na Mkurugenzi wetu Mark na Injinia wetu Kayungi, wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru na kuipongeza Wizara ya Miundombinu kwa kukubali na kupandisha hadhi barabara ya kutoka Gulwe – Kibakwe – Ikuyu – Njiapanda – Rudi – Mtamba – Uyenzele – Chipogolo kuwa barabara ya Mkoa, nawapongeza na nawashukuru sana. Lakini pia, kukubali kupandisha hadhi barabara ya Mpwapwa – Godegode – Bwaga – Lumuma kuwa ya Mkoa, nawapongeza na

ninawashukuru sana. Kwa maana hiyo, katika Wilaya sasa tukibakia na zile barabara za milimani, milima kama ya Wota, milima kama ya Mbuga, Galigali, Matonya, Mang'alaiza, tunaweza tukatumia Mfuko wa Barabara, fedha zile zikaweza kututosha.

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee kuomba kwamba barabara ya muhimu sana ambayo katika maombi yetu ya kupandisha daraja ambayo wameiacha ya kutoka Njiapanda – Kinusi – Malolo na kuunganisha na Ruaha Mbuyuni, ilikuwa ya muhimu sana kwa sababu inakutanisha Wilaya tatu na inakutanisha Mikoa mitatu, yaani Dodoma Iringa na Morogoro. Barabara hii ilikuwa ni ya muhimu sana na ni ya kibiashara sana. Kama ingelichukuliwa na kuwa ya Mkoa, tunaamini kabisa wangeweza kui-*Maintain* lakini kwa fedha za Halmashauri, ni vigumu sana kuweza kufikia kiwango kizuri cha utengenezaji. Nadhani Serikali na Wizara kwa usikivu walio nao, nadhani wanaweza kulifikiria jambo hili upya wakati mwingine kuona umuhimu wa barabara hii ambayo ipo kibiashara zaidi.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye suala zima la barabara ya Iringa – Dodoma – Babati. Kama kuna kitu ambacho kiko wazi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ni suala la barabara hii. Pamoja na kutajwa katika mtiririko wa barabara zilizopo kwenye Ilani, lakini hii imepewa umuhimu wa pekee na hasa inapokuja kutajwa inapozungumziwa masuala ya Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba ninukuu na uone umuhimu wa barabara hii na jinsi ambavyo imekuwa haipewi umuhimu katika Wizara ya Miundombinu. Sijui ni kwa nini pengine wenzetu wataweza kutueleza inawezekana wana maelezo mazuri, lakini sidhani kama tutaelewana maana sasa hivi huu wakati ni mbaya tunaenda kwenye kuhojiwa kwamba tuliahidi na tumefanya kitu gani.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 155, naomba ninukuu, unazungumzia habari ya kuhamia Makao Makuu, Dodoma. Inasema hivi:-

“CCM itaendelea kusisitiza na kusimamia utekelezaji wa uamuvi wa kuhamia Dodoma Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2005/2010, hatua zifuatazo zitachukuliwa kwa lengo la kuzidisha kasi ya kuhamia Dodoma”.

Mheshimiwa Spika, Kipengele (b) anasema:-

“Kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa – Dodoma – Arusha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Dodoma – Mwanza kama mkakati wa kuendeleza Mji wa Dodoma ili uweze kuvutia vitega uchumi”. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mawazo na fikra na pengine hali ya kawaida pia kufikiri na kuonyesha kwamba kuna mkazo mkubwa katika Ilani yetu ya Uchaguzi juu ya barabara hii. Lakini kinachosikitisha ni kwamba mwaka jana tulitengewa shilingi bilioni 12 kwa kipande cha kutoka Dodoma – Babati. Shilingi bilioni 12 zile hatupati maelezo ya kueleweka kwamba zimekwenda wapi na zimefanya kitu gani. Lakini cha

kusikitisha zaidi, kutoka kwenye shilingi bilioni 12, mwaka huu sasa zimetengwa shilingi bilioni 5.6. Hizi nazo, tunashangaa sasa zitafanya kazi gani maana umetoka kwenye shilingi bilioni 12, sasa unazungumzia shilingi bilioni 5.6. Sasa sisi kwa akili yetu ya kawaida na wananchi tutakaokwenda kuwaambia, tutawaambia hivi, sisi tuna mtaji wa shilingi bilioni 17.6 na hapo mtakapotueleza, mtuambie hizi shilingi bilioni 17.6 tunazitumiatumiaje? Hii ndio hoja ambayo itabidi tukubaliane kabla hatujaanza kulilia hicho kingine ambacho tunaona wenzetu hamgawi pesa kwa barabara hii kwa umuhimu tulio nao.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kufika pale Wizarani katika kufuatilia habari ya barabara hii hii. Afisa mmoja nadhani kwa bahati mbaya au kwa utafiti aliokuwa amefanya, akasema barabara hii *is not economic*, nilishangaa sana. Leo tunazungumzia Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, tunajiliza sisi Watanzania tutauza nini katika soko hilo, ni lazima tutauza chakula na chakula hiki, Mikoa minne ambayo tumeitaja katika *The Big Six* katika kuzalisha chakula, ya Ruvuma, Iringa, Rukwa na Mbeya, iko upande huo ambako barabara hiyo inapita, ukifika Iringa ni lazima utauza Arusha, utauza Nairobi, utauza Uganda, lazima upite *shortcut*.

Mheshimiwa Spika, tofauti iliyopo kutoka Iringa kuzungukia Chalinze kwenda kwenye soko ambalo litakuwa Arusha ni kilomita nyingi sana karibu kilomita 1000 wakati kupitia barabara hii ni kama kilomita 600, unaona tofauti ya kilomita 400, je, *is this not economic* na wakati huo umebeba mzigo unaupeleka kule? Yule anayetoka Kenya kuleta kwenye soko na yule anayetoka Uganda kuleta kwenye Soko, ni dhahiri kwa Tanzania soko litakuwa Arusha, je, sisi huku wanaotoka Mikoa ile inayozalisha chakula watauza kwa faida maana gharama yote itaishia kwenye kusafirisha! Kwa hiyo, hii barabara ni *economic*. Dhana na fikra kwamba si *economic* kwa sababu inapita kwenye nyumba za tembe ni dhana potofu, tunazungumzia biashara.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana na mimi naomba tutakopomaliza, watuambie hapa mtaji wetu wa shilingi bilioni 17.6 upo pale pale au hizi shilingi bilioni 5.6 tayari zile 12 zimepotea? Hii hoja iwe wazi na waijibu na si kwa kupigapiga juu juu, tunataka kuelewana hapa.

Mheshimiwa Spika, mambo kama haya ndiyo yanayopelekea watu kuzungumzia wao wa Mashariki, sisi wa Magharibi, wao wa Kusini, sisi wa Kaskazini. Ni jambo baya kuzungumza hivyo na mimi nisingependa tujenge hoja ya namna hiyo. Nadhani tuzungumzie kwa maana ya hoja ya *priorities* lakini wao wa Mashariki, sisi wa Magharibi, si hoja ambayo inaweza kuijenga nchi hii kuwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya amani ya nchi yetu, tukianza wao wa Mashariki, sisi wa Magharibi, tutaishia pabaya. Lakini, inalazimika wakati mwagine kufanya hivyo kwa sababu ya hali ilivyo. Barabara imeahidiwa kwenye Ilani, lakini haipewi umuhimu, tutajibu nini sisi kwa wananchi na tunaenda kwenye uchaguzi? Nadhani wenzetu walione jambo hili na walione katika hali ya uwazi na ukweli na haki pia ili lisituletee matatizo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti ya mwaka 2006, Wizara hii ilipokuwa inawasilisha bajeti yake, ilizungumzia ujenzi wa barabara za Dodoma Mjini na likaja wazo kwamba wanafikiria kutafuta fedha kutoka BADEA. Tukaamini kabisa mipango hii inaweza ikakamilika katika kipindi hiki lakini wote ni mashahidi tunapozungumzia Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi, barabara zetu za Mji wa Dodoma zinatengenezwa katika kiwango cha chini kuliko pengine hata Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam na kwingineko ambako barabara zinatengenezwa katika kiwango kizuri.

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali ije na mpango madhubuti, mpango maalum wa kujenga barabara za Mji wa Dodoma. Tukiachia tu Manispaa, tukiachia tu *CDA* peke yake, kama hatuji na mipango madhubuti, hatuwezi kuwa na barabara nzuri Dodoma. Tunaisifu tu kwamba Dodoma ni Makao Makuu ya nchi yetu, lakini hatuipi hadhi, hatupeleki *resources* pale ambazo zitafanya Dodoma iweze kunyanyuka.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa hatua inazochukua katika kuleta uwekezaji hasa wa elimu katika Mkoa wa Dodoma, nipongeze sana. Tumekuwa na vyuo vikuu kwa mara moja vingi tu, takriban vyuo karibu vitano ambavyo vimeleta idadi kubwa ya watu katika Mji wa Dodoma na kuchangamsha soko la Dodoma na hivyo Dodoma mambo yanakwenda vizuri, mfano Chuo Kikuu cha Dodoma. Lakini kama hatutakuwa imara na mipango madhubuti katika miundombinu hasa ya barabara, basi Mji huu utakuwa ni sawa sawa na Miji mingine ambayo haina malengo ya kuwekwa katika kipaumbele kama cha Mji wa Dodoma. Kwa hiyo, sioni tofauti unapoizungumzia Tabora na unapoizungumzia Dodoma. Tunavyosema katika Ilani ni tofauti kabisa na jinsi tunavyoigawia fedha za miradi hasa ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nitaunga mkono hoja endapo nitapata maelezo mazuri juu ya shilingi bilioni 17.6 za mwaka jana na shilingi bilioni 5.6 za mwaka huu ili tuelewane, bila hivyo itakuwa vigumu sana, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, napenda sana kukushukuru kwa dhati kabisa kwamba uliona umuhimu wa hoja yangu na umeweza kufanya marekebisho na umenipa fursa sasa ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, nakushukuru sana.

Napenda pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mungu ambaye ameniwezesha kusimama hapa na kuweza kuzungumza leo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kuzielezea zile hisia zangu nilizokuwa nazo wakati ule Mheshimiwa Rais alipoamua kutangaza Baraza Jipyaa la Mawaziri, alipowateua Mheshimiwa Kawambwa na Mheshimiwa Chibulunje, kuongoza Wizara hii na baadaye kumteua ndugu yangu Chambo kuwa Katibu Mkuu, nikasema kazi ipo. Nikasema amewekwa Sheikh, Padri na Ustaadh katika hii Wizara ambayo mimi naifahamu, nimekuwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu toka mwaka 2006, kumbe nilikuwa nimekosea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu hawa ukiwatazama kwa wajihii wao, ni wapole mno, lakini ni mahodari, wasikivu na wanafanya kazi vizuri. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Kawambwa, Mheshimiwa Chibulunje na Katibu Mkuu, watendaji wa Wizara ya Miundombinu na viongozi wote wa taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara hii ya Miundombinu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa kuzingatia jambo moja muhimu sana na la kihistoria ambalo lilikuwa limesahafulika kabisa. Sijui wangapi kati yetu wanakumbuka *Mlungushi Club!* Sijui! Lilikuwa ni kundi la Marais watatu likiongozwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, liliunganisha nchi ya Uganda na Zambia. Katika Azimio lao la *Mlungushi Club*, walilofanya kule Zambia, lilikuwa ni kuimarisha barabara itakayounganisha kutoka Kampala mpaka Mbala, Zambia. Barabara hii ilikuwa inapita Bukoba, inakuja katika Mkoa wa Kigoma, Kibondo, Kasulu kisha hatimaye Mpanda, Sumbawanga hadi Kasesha. Toka wakati huo wa *Mlungushi Club*, jambo hili lilifunika kabisa, amekuja kulifunua Mheshimiwa Kawambwa sasa kwa kuanzisha kujenga barabara inayoanzia Kasesha – Sumbawanga – Mpanda hadi Nyakanazi, nawapongeza sana. Barabara hii, ina umuhimu huo kwamba inaunganisha nchi kadhaa, si Uganda tu kama walivyokuwa wamekusudia viongozi waasisi wa mataifa haya, lakini pia inaunganisha Rwanda na Burundi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa msikivu juu ya kilio changu mimi pamoja na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Rukwa. Kwa pamoja tumekuwa tukipigia kelele sana juu ya maendeleo ya Mkoa wa Rukwa na hasa njia za kuingia katika Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa umekuwa hauna kiwanja cha ndege cha kudumu, viongozi wote wa Kitaifa ama wakitaka kuja Rukwa, wateremke Tabora au Mbeya, wafuate kilomita 400 kuja Tabora au wafuate zaidi ya kilomita 500 kwenda Mbeya. Ilikuwa ni aibu na fedheha na usumbufu mkubwa kwa viongozi ambao walikuwa wanakuja katika Mkoa wa Rukwa. Wametusikia kilio chetu, napenda kuwashukuru sana kwa kutengea fedha, pengine najua ni kidogo, lakini si haba kwa ajili ya kuimarisha uwanja wa ndege wa Mpanda. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri katika hilo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, pia napenda nitoe pongezi maalum kwa Mamlaka ya Usalama wa Anga. Nilikuwa siamini, kumbe ni kweli kabisa wako wanawake mashujaa na wanaoweza kuthubutu. Napenda kumpongeza sana dada yangu, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga, kwa hatua aliyoichukua ya kuisimamisha *Air Tanzania*, nampongeza sana. Alitimiza majukumu yake, utaaliam na weledi wake katika kazi yake, akaamua kuthubutu kulisimamisha shirika ambalo ni la Serikali. Wachache mionganoni mwa viongozi tulio nao wanaoweza kuwa na uthubutu wa aina hiyo. Nampongeza sana kwa sababu alitanguliza kwanza usalama wa watu wanaosafiri na ndege na kama wengine wataiga, itatusaidia sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, lakini bado pia katika eneo hili la usafiri wa anga, tuna tatizo sana la Marubani. Marubani waliopo, ni wachache na kwa bahati mbaya sana wako Watanzania ambao wanaweza kuwa Marubani, lakini kwa sababu wanatoka katika

familia maskini, wanashindwa kuweza kujisomesha na kuwa Marubani. Wanapohitaji kupata mkopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, wanashindwa kupata kwa sababu hizi *rare profession*, hazipewi mikopo na Bodi ya Mikopo. Ninaomba waangalie eneo hili ili hawa vijana ambao wanapata fursa ya kwenda kusomea Urubani, waweze kupata mikopo kutoka kwenye Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, aidha, pia niipongeze sana *SUMATRA* kwa uamuzi wake wa kuisimamisha MV Muongozo. Hawa kadhalika wametekeleza wajibu wao ipasavyo, nawapongeza sana katika hilo. Ilikuwa ni adha kubwa sana katika usafiri wa meli hii ya Muongozo pamoja na mahitaji yalivyo katika Ziwa Tanganyika lakini pia nao wamezingatia uhai na usalama wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Mamlaka ya Bandari, kwa jitihada wanazozifanya sasa hivi za kupunguza michanga katika bandari za Maziwa. Ni hatua nzuri na itasaidia sana kuboresha huduma katika maziwa yetu. Lakini niseme masikitiko yangu kwamba wako watu ambao wanaongoza taasisi wanaoweza kuchukua maamuzi na taasisi zingine wanashindwa na hasa nionyeshe masikitiko yangu juu ya *NEMC* (Baraza la Mazingira), kwa kushindwa kuchukua hatua juu ya uvujaji wa kemikali kule katika Mgodi wa *Berrick – North Mara*, inasikitisha sana. Inasikitisha hasa pale nilipokuwa naangalia taarifa ya habari, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Balozi Kagasheki anasema kwamba ye ye amedanganywa na Barrick, amepelekwa mahala sipo, kumbe kweli kemikali inavuja. Kama Waziri anadanganywa, sembuse hawa? Nina mashaka sana na taarifa hiyo kwa sababu ziko jitihada zinazofanywa kupitia Bunge hili hili, juu ya Mgodi wa *North Mara*, nadhani ukweli utafahamika.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie usafiri katika Maziwa yote; Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika na hususan nitajikita katika Ziwa Tanganyika ambalo nalifahamu zaidi kuliko Victoria. Victoria najua kuna tatizo la ile meli ambayo imebakia moja, MV. Victoria nayo imekuwa ya muda mrefu, imechakaa, inahitaji ifanyiwe matengenezo ili kuboresha huduma katika Ziwa Victoria lakini Ziwa Tanganyika ni mbaya zaidi na hasa katika kipindi hiki ambapo kuna hizi pepo za kusi. Meli inayofanya kazi katika Ziwa Tanganyika ni moja tu, Liemba.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako, meli hii inapofanya safari kwenda Zambia inapita katika Majimbo matano ya Uchaguzi ya Kigoma Kusini, Mpanda Magharibi, Nkasi na Kalambo. Majimbo yote haya yanaongozwa na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Kwa bahati mbaya sana, wananchi wa maeneo haya, wanalamika wana shida kubwa mno, lakini sisi kazi yetu ni kuwasemea Watanzania wote bila kujali hivyo vyama tunavyotoka.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo katika ziwa Tanganyika, kubwa sana, meli inasafiri aidha mara moja au mara mbili kwa mwezi. Kwa hiyo, wasafiri hawa ambao wapo katika mwambao wa ziwa hili la Tanganyika hawana njia nyingine ya usafiri isipokuwa kutumia boti na kuhatarisha maisha yao na usalama wao. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo katika bandari ya Kigoma, naiomba Mamlaka ya Bandari iangalie juu ya Wakala wa Kupakua na Kupakia Mizigo pale bandarini. Naomba pia waangalie umuhimu wa kuanzishwa kwa Bandari ya Ujiji.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa, kwa hizi dakika tano zilizobakia, nijikite katika reli. Nimejaribu kwa makusudi tu kuacha kuzungumzia reli kwa sababu imezungumziwa sana na Wabunge waliotangulia. Umuhimu wake umesisitizwa lakini nimhakikishie tu ndugu yangu Mheshimiwa Selelii wala asihangaike, hoja ya wananchi ipo juu ya Meza ya Spika, tunasubiri majibu tu atakayoyawasilisha leo ndugu yetu Waziri wa Miundombinu, ili tujue hatua gani tunachukua, hayo ni kwa mujibu wa maelekezo niliyoyapata kutoka katika Meza ya Spika.

Mheshimiwa Spika, lakini linalotisha na kusikitisha, ni hili ambalo nitataka pia nipate ufanuzi. Imeenea sana katika mtandao kwamba Wahindi wa *TRL* watoweka na mabilioni. Taarifa nilizozipata toka chanzo cha ndani kabisa, kwa maana ya mtumishi wa *TRL*, Makao Makuu kuwa wale vibosile wa *TRL* ambaeo ni Wahindi, wametoweka na kiasi kikubwa cha fedha na kubakiwa na Wahindi wachache wa kada za chini, ambaeo hata hivyo nao wamekuwa wakiondoka mmoja baada ya mwingine. Naomba kafanyike ka-kazi, ili kuthibitisha ukweli huu au ye yeyote mwenye *assessment* ya *TRL* atujaze juu ya tetesi hizi. Hizi ni tetesi zinawezekana zina ukweli lakini wamekwenda mbali sana katika mitandao kuzungumzia juu ya *TRL* hata ukiingia katika *Website* ya *RITES*, huoni kama wana mradi wowote huku Tanzania. Tuna mashaka sana juu ya kampuni hii na uwezo wake. Kwa hiyo, tutahitaji kupata maelezo na tuondolewe wasiwasi juu ya fedha hizi kwa sababu anayesimamia fedha ni Mhindi, fedha zinawekwa katika *Bank of India, Bank of Baroda*, hakuna Mswahili yeyote anayejua ni kiasi gani kimewekwa na kiasi gani kimebaki. Hizi habari zinaweza zikawa zina ukweli, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu basi atueleze hilo.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi ambayo yanahu reli ambayo wenzangu wameyazungumzia, wala sina sababu tena ya kuyarudia. Nililetu hoja binafsi hapa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu ilitoa mapendekezo yake, tunasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri mchana huu kisha hatua zitazofuata tutachukua, kwa sababu tayari maombi ya wale wananchi mia moja na thelathini na ngapi yako kwako Mheshimiwa Spika.

Mhesimiwa Spika, la mwisho kabisa, nataka nimkabidhi Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu haya makaratasi, ni madai ya wale watumishi waliokuwa *TRC* ambaeo wanadai mapunjo. Naomba Waziri ayafanyie kazi, wananchi hawa walipwe fedha zao, nakushuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Arfi, Wahudumu watakusaidia, huna haja ya kuyabeba na inabidi yaende kwa Spika, huwezi kumpelekea Waziri moja kwa moja, ndio utaratibu.

Sasa namwita Mheshimiwa James Lembeli atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Kwaangw'.

MHE.JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, napenda nianze mchango wangu, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kahama na hususani wale wa Jimbo la Kahama, kuishukuru Serikali kwa kupandisha hadhi barabara ya kutoka Kahama Mjini kwenda Chambo, umbali wa kilomita 45 kutoka barabara ya Wilaya kuwa barabara ya Mkoa. Naishukuru sana Serikali. Barabara hii imekuwa ni kero na kilio kwa wananchi hususani wa Chambo na Chona.

Mheshimiwa Spika, sambamba na shukrani hizi, kwa niaba ya Wanachi wa Jimbo la Kahama, napenda niwasilishe masikitiko yao kwa jinsi ambavyo Serikali imeshindwa kupandisha hadhi barabara nydingine mbili ambazo ni za Halmashauri ya Wilaya na Mkoa ambazo walipendekeza zipandishwe hadhi. Hii ni kutokana na kwamba barabara hizi ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Wilaya ya Kahama, lakini pia uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Shinyanga. Barabara hizi ni pamoja na ile inayotoka Kahama kwenda Kata ya Uloa kuititia Kata sita ambazo ni muhimu kwa uzalishaji mkubwa wa mazao ya pamba, mahindi na zaidi zao la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, barabara hii iko katika Jimbo la Kahama lakini kuna barabara nydingine inayotoka Kahama mjini kuelekea Bulige katika Jimbo la Msalala kwa Mheshimiwa Maige ambayo kimsingi ndiyo inayosafirisha mpunga mwingi unaolimwa katika Wilaya ya Kahama hadi Kahama mjini na kutokea hapo kuelekea Shinyanga mpaka Pemba na Zanzibar. Ninapata kigugumizi kuamini kwamba zoezi la kupandisha hadhi barabara hizi linafanywa kwa uadilifu. Ninahisi, zoezi hili linafanywa katika maofisi kule Makao Makuu na kwamba hawana habari kabisa na hali halisi ya mapendekezo ambayo yametolewa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, barabara hii ya kutoka Kahama Mjini kwenda Uloa. inapita katika Kata sita. Kata ya Zongomela , Nyadekwa, Ukune, Kisuke, Uyogo, Ushetu hadi Uloa umbali wa kilomita takribani 120. Barabara hii ambayo inahudumiwa na Halmashauri msimu wa kiangazi, wakati wakulima wameshavuna inapitisha malori yenye tani kuanzia 20 mpaka 60, sasa mtaalamu anaposema kwamba barabara hii haifai, nashindwa kuelewa na Halmashauri kwa vyovypote vile haiwezi kuhudumia barabara ambayo malori makubwa yanayokwenda kuchukua Tumbaku kule Uloa, kupeleka Morogoro malori ya tani 60 yahudumiwe na Halmashauri hili ni jambo la kusikitisha. Ninaomba sana Maafisa hawa wa Serikali watoke maofisini na waende kule ambako wananchi wana shida.

Mheshimiwa Spika, nina mashaka makubwa na zoezi zima hili. Ukiangalia katika Mkoa wa Shinyanga, barabara zilizopandishwa hadhi ni zile ambazo kimsingi hazina umuhimu mkubwa katika uchumi na uzalishaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kinachofanyika nahisi ni watu hawa wanaangalia kule kuna nani, basi wanaamua kupeleka hizo barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Kahama. Mwezi wa kumi mwaka 2005, wakati Rais akiwa katika *campaign* ya uchaguzi, aliwaahidi wananchi wa Mji wa Kahama kwamba inahitaji lami na kusema

kwamba katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake, Awamu ya Nne atahakikisha kuna barabara ya lami pale Kahama Mjini. Nimengalia vitabu vyote sioni dalili yoyote ya barabara ya lami kujengwa katika mji wa Kahama, hakuna pesa ambayo imetengwa kuteleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi ni kwamba mwaka 2007, wakati Rais amefanya ziara pale Kahama, aliyahakikishia wananchi wa Kahama kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Chenge, akamwambia kuwa waeleze hao ndugu zako kwa kilugha na Chenge aliwaeleza kwa Kinyamwezi kwamba barabara hiyo iko mbioni kujengwa. Mwaka huu tarehe 31 Mei, akizungumza na wananchi wa Mji wa Kahama Rais alirudia ahadi hiyo akasema kwamba itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja hii mpaka nimepata maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais. Haiwezekani ahadi ya Mheshimiwa Rais, kipenzi cha wananchi wa Kahama, ikaachwa, ikapigwa danadana hivi hivi na mimi mwalikishi wa wananchi wa Kahama, niko ndani ya hili Bunge. Nitasita kuiunga mkono hoja hii mpaka nihakikishiwe Rais ahadi yake inatekelezwa. Sioni mantiki ya Serikali, ya watendaji wa Wizara hii kumgombanisha Rais na Wananchi ambao wamemuunga mkono kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nzungumzie kidogo barabara ya Manyoni – Singida. Hivi kuna mzimu gani kwenye barabara ile? Haiwezekani barabara ya urefu wa kilomita 60, ikachukua miaka sita kujengwa. Nimesoma makabrasha hapa, naona barabara ya kutoka Manyoni mpaka Isuna itakamilika mwaka 2010 mwishoni. Sasa ni barabara gani ya aina hii inajengwa kwa ziadi ya miaka saba? Barabara hii ilianza kujengwa na Serikali ya Awamu ya Tatu mpaka sasa ni kitendawili.

Mheshimiwa Spika, sisi wa Kanda ya Magharibi hasa Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kigoma mpaka Mara, kipande hiki cha barabara ni kero kubwa. Sielewi kimetokea kitu gani lakini nina wasiwasi na mambo haya ya mikataba ambayo baada ya kuwa imetiwa saini inaanza kuleta migogoro na yote hiyo inatokana na suala zima la rushwa, 10% ndio inanimaliza nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi pekee ambayo usafirishaji wake unategemea barabara. Mimi sijawahi kuona, nimezunguka duniani kote, usafirishaji wa mizigo mikubwa unafanywa na reli lakini kwa Tanzania ni kwa babara. Hili ni jambo ambalo kwa kweli linahitaji kutazamwa kwa kina na kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi mimi namsikitikia sana ndugu yangu, mtani wangu Kawambwa kwa sababu kwa jinsi alivyo, ni mpole sana, hawezi kukemea mtu. Mheshimiwa Chibulunje huyu alikuwa ni bosi wangu wa zamani kule Ushirika, naye ni mkimya sana, sidhani kama anawaweza hawa watu, hawa watu wa Wizara ya Miundombinu ni watu ambao kwa muda mrefu sana ni wakorofi na kila mara ukiwahoji watakwambia hili ni suala la kiufundi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, kidogo muwe wakali, haiwezekani nchi hii tukaendelea kuendesha jinsi ilivyo. Suala la kipaumbele katika barabara, mimi linanipa mashaka makubwa, wakati Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Mwanza na nizungumzie Mkoa wa Shinyanga, ndio Mkoa wenye idadi kubwa ya watu katika nchi hii, ni Mkoa ambao ni hazina kubwa kwa Chama cha Mapinduzi, unapokuja wakati wa uchaguzi lakini miundombinu yake katika Wilaya zote, ni mbovu kupindukia. Lakini unashangaa maeneo mengine ya nchi hata barabara za kwenda kichochoroni ziko kwenye Mkoa, barabara za ajabu ajabu, ni za lami, kulikoni? Mimi nafikiri tufike mahali, nchi hii igawiwe rasilimali sawa kawa sawa bila kuangalia mkubwa anatokea wapi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga unazalisha 60% ya pamba inayosafirishwa nje ya nchi hii lakini barabara zinazoelekeea kule inakozalishwa pamba hazifai. Mkoa wa pekee wenye migodi mikubwa za dhahabu ya Bulyanghulu na Buzwagi. Vilevile kuna almasi, ukiuliza wananchi wa maeneo haya wanafaidika nini na pamba yao, wanafaidika nini na dhahabu yao, wanafaidika nini na almasi yao watakwambia hakuna na watu wanaendelea kuwa maskini, jambo hili linanisikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, *TICTS*, kwa maoni yangu, wafukuzwe kesho, waondoke, ni watu ambao wanakejeli kubwa. Juzi nilikuwa nasoma gazeti la Jumanne la Tanzania Daima, wametoa tangazo, naomba ninukuu kidogo walichosema, wamesema:-

“Uongo unaoenezwa na ukweli. Hadithi, TICTS haiwezi kuendesha Bandari, ukweli TICTS ni sehemu ya HPH inayosimamia bandari 49 ulimwenguni na ina historia kuanzia karne ya 18”.

Huu ni wizi mtupu na uongo wa kuwadanganya Watanzania. Inawezekana katika hizo bandari 48, inafanya vizuri, Tanzania *TICTS* haifanyi vizuri, inawaibia wananchi, inadidimiza uchumi wa nchi hii, hawa ndugu waondoke haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu walioingiza mkenge Serikali kwenye tatizo hili la *TICTS* wapo, tunawafahamu na Serikali inawafahamu lakini inazidi kuwakumbatia. Rushwa nchi hii itatumaliza. Mimi ninapenda ule ukiritimba ambao *TICTS* amepewa, uftutwe ili taasisi na makampuni mengine yaweze kusaidia katika kuboresha huduma katika bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mwisho reli, wenzangu na hususani wale wa Kanda ya Magharibi, wamesema sana kuhusu jambo hili, ni aibu kwa nchi hii. Nchi hii ilipopata uhuru ilirithi reli iliyokuwa inafanya kazi. Serikali ya Awamu ya Kwanza, imeiendesha reli hii mpaka pale ilipomalizia muda wake. Wapo viongozi hapa, yupo mzee Athumani Janguo, alikuwa Kiongozi Mkuu wa Shirika la Reli, reli ilifanya kazi vizuri. Wakati nikisoma, nilipanda treni kutoka Isaka mpaka Dodoma na kutoka Dodoma mpaka Njombe. Mambo yalikuwa yanakwenda vizuri, ukiingia *buffet car* kila kitu kipo, chai na nini, leo hii tumeleta wawekezaji hapa hamna kitu. Hawa watu ni wez. Waondoke.

Wakati wanaingia hapa nchini kuomba kazi, walikuja mikono ikiwa mbele, tunaomba kazi, kuna msemo wa Wahindi wanasema:-

“Wewe omba kaji kono mbele pata kaji kono nyuma”.

Mheshimiwa Spika, msemo huu umedhihirika. Hawa watu wakati wanaomba kazi wamekuja mikono mbele sasa wamepewa kazi mikono nyuma, wanaendelea kuiibia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini niulize wakati Serikali inataka kuingia mkataba na hawa *RITES*, ndani ya Bunge hili, kuna watu walihoji na kutoa *data zinazohusu kampuni* hii lakini ndugu yangu Chenge wakati huo akiwa Waziri alisema hawa ni watu wazuri.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono mpaka nimepata maelezo kuhusu barabara za lami Kahama Mjini, nakushuru sana. (*Makofî*)

MHE. OMARI S. KWAANGW’: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na hasa kwa hoja hii ambayo kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia jambo ambalo na sisi wengine linatugusa kwenye barabara ya Dodoma - Babati - Iringa. Pengine nisingepata nafasi hii mawazo ya sisi tulioko huko pengine yasingepatikana na ninadhani ni mimi peke yangu kwa Mkoa wa Arusha na Manyara, ndio nimepata nafasi hii, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze na pongezi na shukrani. Nilipoingia Bungeni, hotuba yangu ya kwanza kabisa, *maiden speech* ilikuwa inahusu barabara ya Dodoma - Babati - Iringa mwaka wa 1996. Pia maswali yangu ya kwanza kabisa na Mheshimiwa Lekule aliyejuka shahidi hapa, yalihu barabara hiyo, nashukuru kipande kidogo kimeanza kutekelezwa nacho ni kutoka Minjingu - Babati, japo sasa ndio inachepukia Singida, kwa hilo tunashukuru na fedha zimetengwa kwa barabara ya Minjingu - Babati. Ninataka nipongeze kwamba zimetengwa fedha za ndani na nje na kwa kweli fedha za ndani shilingi bilioni 11.27 na fedha za nje shilingi bilioni 10.3 jumla shilingi bilioni 21.6, tunashukuru sana, kazi imeanza. Kwa hiyo, tunawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka nishukuru vile vile, ni upandishwaji wa hadhi barabara na kuwa barabara za Mkoa. Sisi Babati tumebahatika kwamba barabara muhimu sana ya kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya ya Mbulu, imepandishwa hadhi. Barabara hiyo, inatoka Babati - Imbilili - Kiru - Eri - Kuta - Mbulu, kwa kweli jambo hili limefungua mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya yake moja ya Mbulu.

Mheshimiwa Spika, fedha zimetengwa kwenye barabara za Mkoa ambazo zinaingia pale Babati. Barabara inayotoka Babati - Magara - Mbulu, inatengenezwa vizuri na fedha zimetengwa na nyingine inayokwenda Mbulu inatoka Babati - Bashnet - Dongobashi - Mbulu, kwa hiyo, tunashukuru kwa sababu barabara hizi zinafungua milango ya Mkoa na Wilaya zake. Vile vile nimeona barabara ya kutoka Babati - Kiteto -

Kibaya kule na Kibaya – Orkesmeti, nayo imetengewa fedha, nashukuru kwamba imetengewa fedha na marekebisho yanaendelea na hasa baada ya kumfukuza Mkandarasi aliyejwa anajenga barabara hiyo, nashukuru sana. Kazi hiyo ilikuwa kazi nzuri, Wizara pale imeonyesha wanao uwezo wa kumfukuza Mkandarasi ambaye ni mbabaishaji. Kwa kweli hilo tunawapongeza lakini inasikitisha, tunasikiasikia yupo kwenye Mikoa mingine, Mkandarasi kama anaharibu, ashushwe, asubiri ajifunze, sio tena anatoka Babati anakwenda kwenye Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba nirudi kwenye barabara ya Babati - Dodoma - Iringa. Kwanza, barabara hii, ilitengewa fedha mwaka 2008 – 2009 shilingi bilioni 12, kama walivyosema na mimi naungana na Wabunge wote waliochangia kuhusu barabara hii na hasa Mheshimiwa Dada yangu, Mheshimiwa Zabeni Mhita, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Dr. Chegeni, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Mheshimiwa Malangalila, Mheshimiwa Madeje, Mbunge wa hapa Dodoma, Mheshimiwa Selelili, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Simbachawene na wengine wote waliozungumzia barabara hii, ninawapongeza sana kwa kuona umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, sisi wengine tumeizungumzia kwa miaka yote hiyo. Sasa kwenye Kitabu cha Nne ilitengewa shilingi bilioni 12, ukurasa wa 176, cha kusikitisha, ukienda Kitabu cha Nne cha mwaka huu wa 2009 – 2010, barabara hii, ndio huu mchezo ambao nadhani unachezwa ambao sio sahihi sana, kwa kawaida ni lazima uonyeshe makisio yaliyopita unapoweka makisio ya sasa, kwenye kitabu hiki cha mwaka 2008 - 2009 kitabu hiki cha sasa kinaonyesha 0, tungepaswa kuona hizo shilingi bilioni 12 hapa na mwaka huu ndio wangetuonyesha hizo shilingi bilioni 5.6 walizotenga hapa. Sasa hapa zipo shilingi bilioni 5 lakini hizo zingine hazipo.

Mheshimiwa Spika, tutakuomba mwongozo mara ngapi? Kwenye Kitabu hiki cha Nne, hamna, kwenye kitabu kingine hiki zilikuwepo. Kwa hiyo, kuna tatizo kwenye eneo hili. Shilingi bilioni 12 zinazozungumzwa, mimi mwenyewe nilizizungumzia, ninayo *Hansard* ya mwaka jana, kwa ruhusa yako, naomba niseme tu nilichochangia, nilisema:-

“Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Dodoma – Babati, imetengewa shilingi bilioni 12”.

Mheshimiwa Spika, huu ndio ulikuwa mchango wangu wa mwaka jana, kwa kujua kweli zimetengwa, sasa leo kwenye kitabu cha mwaka huu hazipo.

Mheshimiwa Spika, nikaendelea kueleza kabisa kwamba bado inaelezwa kuwa kuna upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hii. Mheshimiwa Waziri alisema hivyo mwaka jana upembuzi yakinifu na mwaka huu tena amesema na katika majibu yake mwaka jana ye ye mwenyewe alieleza kuhusu barabara hii na naomba ninukuu kidogo ukurasa wa 250 wa *Hansard* alisema:-

“Niseme kwamba kati ya barabara hizo zimo hizi ambazo zimesemewa kwa hisia nzito kama barabara ya Musoma - Kigoma – Bunda – Ikizu – Fort Ikoma - Iringa - Dodoma – Babati”.

Mheshimiwa Spika, kakubali ye ye mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwamba zimesemewa mwaka jana kwa hisia nzito, hotuba yake iko hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliendelea kusema:-

“Aidha kipande cha barabara ya Dodoma – Babati – Minjingu, usanifu wa kina umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2008 – 2009”.

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka huu Waziri anasema nini? Waziri anarudia kusema kwamba:-

“Kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu barabara zifuatazo Babati – Dodoma - Iringa”.

Mheshimiwa Spika, sasa tuseme lipi sasa? Kwa hiyo, hapa kuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, nataka niende sasa kwenye majedwali yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasemea hapa. Tunalo tatizo la mipango, hatuna Tume ya Mipango, kama tungekuwa na Tume ya Mipango, haya yasingetokea! Kupanga barabara kwa mtindo huu, tatizo ni kukosekana kwa Tume ya Mipango, tunafika mahali kila mtu anajipangia barabara anavyoona ye ye mwenyewe, ndio kinachotokea hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama barabara zilizotajwa zimeainishwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, je, ilishindikana kufanyika uchambuzi wa kuonyesha vipaumbele ni nini? Barabara hii ya Babati – Dodoma – Iringa, imeandikwa sana na ipo kwenye Ilani kama alivyosema Mheshimiwa Simbachawene lakini sio tu imeonyeshwa kwenye *list* ya ukurasa wa 54 wa hizo barabara zote ikiwa ni pamoja na hizi ambazo ni mpya lakini barabara hii imeandikiwa aya tofauti, sina haja ya kuisoma kama aliviyosoma Mheshimiwa Simbachawene kwa maana ya kuhakikisha Makao Makuu ya nchi, yanaunganishwa na umuhimu wa barabara hii. Kama kuna mtu anazungumza huko Wizarani, basi tuna watu wenye mawazo mgando kwa sababu utalii wote unaotoka Afrika unakuja mpaka Kaskazini mwa nchi yetu, unataka uende mpaka Afrika ya Kusini kule, unapita kwenye barabara hii, unashindwa kuunganishwa kwa sababu ya kipande hiki ambacho hakina lami kutoka Minjingu – Iringa.

Mheshimiwa Spika, utalii ni jambo muhimu sana. Sasa hivi utalii wa Kusini Mbeya, Iringa, kote huko pamoja na wa Kaskazini ambao ni mkubwa, hauunganishwi kwa sababu hakuna kitu hapa na huwezi kwenda kwenye nchi zingine kule. Barabara hii Kuu ya Kaskazini, *The Great North Road*, umuhimu wake mkubwa ni kwamba nchi zote ambazo barabara hii inapita ndiko Makao Makuu ya miji yao imewekwa, Addis Ababa,

Nairobi – Dodoma. Nenda Lusaka mpaka Cape Town kule, miji mikuu yote iko kwenye barabara hii, halafu mnasema haina umuhimu!

Mheshimiwa Spika, sasa hebu angalia kuhusu barabara hizi mpya, hivi unaposema Korogwe – Handeni, kilomita 65, umeipa shilingi bilioni 7.6 umeacha Dodoma – Babati kilomita 272, wao wameandika kilomita 261, mimi najua ni kilomita 272, umeipa shilingi bilioni 5, Handeni – Mkata, kilomita 54 tu, umeipa shilingi bilioni 6.9, unaacha Dodoma – Iringa, kilomita 267 unaandika shilingi milioni 20, aah, hapa inachechesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara Dumila – Kilosa, kilomita 78 imepewa shilingi bilioni 8.7, unaacha Dodoma - Babati kilomita 272. Kwa hesabu zangu au za kwao 261, Dodoma – Iringa, kilometra 267, unatoa kama bilioni 5 na milioni 20 kwa barabara nzima hii, sasa hivi kweli tunafikiri sawa sawa? Nadhani tuna tatizo la kufikiri nah ii yote ni kutokana na ukosefu wa Tume ya Mipango, ndio inatufikisha hapa.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na hoja yoyote itakayoletwa Serikali ibadili, ihakikishe kwamba Shilingi bilioni 12 zilizowekwa na hizi Shilingi bilioni 5.6 kwanza hizi ni za madaraja tu wanatuambia barabara hii ianze kujengwa. Ni aibu sana kwa ilani yetu ambayo ndiyo inasisitiza na imeandikiwa aya ya peke yake halafu hatuitili maanani. Ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shilingi bilioni 17.6 iwekwe na Serikali iseme fedha hizo sasa zipo na barabara inaanzwa, vinginevyo hizo nyingine mpya nilizozitaja zifutwe, fedha zile zihamishwe kwenye barabara hii, kama wanataka kuzifuta watafute fedha na baadaye mje mtuambie kwenye *supplementary estimates* kwamba tumetafuta hizi bilioni na tumeziweka kwenye barabara hii vinginevyo hatueleweki hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishie kwanza hapo, suala la kuunga mkono kwa kweli sina hakika maana haieleweki.

Mheshimiwa Spika, barabara za Mkoa ambazo zimepandishwa daraja zimetengewa Shilingi bilioni 32.6. Kwa kuwa, zimetengwa hela Shilingi bilioni 32.6 namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie mmezipandisha daraja, fedha zipo sasa ili sisi kama kule Babati barabara iliyopandishwa inayotoka Babati Mbili kwenda Mbulu, basi fedha zile ambazo tumezoea kule Halmashauri tuzipeleke kwenye Kata nyingine ili sasa ye ye azichukue moja kwa moja maana umeshatutangazia hapa, tunataka kujua kwenye Shilingi bilioni 32.6 zimo hizi ambazo umezipandisha madaraja?

Mheshimiwa Spika, tabia ya wakandarasi, lipo tatizo kubwa kwamba hawasimamiwi hata kidogo! Wanapoweka makambi yao wanazua mambo mengi, ugomvi, wizi, mtindo wa kazi *rough* na mazoea ya kufanya mambo ambayo kwenye jamii hayakubaliki. Makambi haya ni matatizo! Yupo mmoja ambaye sasa ameanza tu barabara ya Mijingu - Babati ameshaleta kasheshe chungu nzima pale, wanasulubu watu, kama raia wanafanya makosa kuingia kwao na raia tunasema wasiingie, basi wachukue hatua za kisheria, vituko vile sina sababu ya kuvitaja hapa, baadaye nadhani nitanon' gona

na Mheshimiwa Waziri halafu nimweleze yaliyotokea. Ni mabaya sana, maana ukishasikia mkandarasi anaanza barabara halafu na vituko vingine vya ubakaji na ugomvi na kadhalika, hii sasa ni balaa! Watu wametumwa kuja kujenga barabara na siyo kufanya hayo mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme kwamba kwenye barabara hizi ambazo zinajengwa wakati wakandarasi wanajenga hizi ambazo zinakuwa nje ya *road reserve* ambazo zimeshafidiwa, kama mkandarasi anakwenda tena nje anaharibu vitu vya watu ninadhani vinastahili kupewa fidia, maana wanatakiwa waishie kwenye *road reserve* kwenye kiwango chao kile.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Sitaunga mkono hoja mpaka tupate maelezo kama hizo bilioni zimerudishwa. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) nina mamlaka ya kuongeza muda ikiwa hoja itakubaliwa. Nayo inasema hivi: “Bunge litakutana hadi saa saba mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni isipokuwa kama Spika akiona inafaa, Bunge linaweza kuendelea kukutana kwa muda usiozidi dakika thelathini au kusitishwa wakati wowote kabla ya saa saba mchana.”

Waheshimiwa Wabunge, sasa nakusudia kwamba kwa kuwa saa 11.00 Naibu Waziri atapewa nafasi halafu Waziri waendelee kujibu hoja, kwa hiyo, nimeona ni vyema tutumie nusu saa kama mkikubali ili tusikie wachangiaji wengine na ituwezeshe tukitoka hapa sasa tuwe tumeongeza idadi ya wachangiaji ili saa 11.00 tutakapokuja kwa sababu natazamia Kamati kidogo itakuwa ndefu, basi tuweze kwenda kwa utaratibu huo. Sasa ili hoja hiyo iweze kuamuliwa namwomba Waziri wa Nishati na Madini aweze kutoa hoja chini ya Kanuni ya 28(3) halafu nitawahoji.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(3) na kwa kuzingatia Mwongozo wa maelekezo yako, naomba sasa Bunge lako Tukufu liliridhie kutengua Kanuni ya 28 (2) ili hatimaye majadiliano kuhusu mada au hoja iliyopo mbele yetu iendelee kwa muda wa dakika thelathini za ziada.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naafiki

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Bunge liliridhia Kutengua Kanuni Zilizotajwa*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja iliyopo mbele yetu ni kwamba itakapofika saa 7.00 tuweze kuendelea kwa kipindi kisichozidi dakika thelathini, hoja hiyo imetolewa na kuungwa mkono. Nawashukuru sana kwa kukubali hilo kwa maana mjadala wa hotuba hii ni mzito kidogo.

Baada ya kupata ridhaa hiyo, nawataja Waheshimiwa wanenye wanaofuatia katika kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Kwanza ni Mheshimiwa Fred Mpandazoe, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na baadaye Mheshimiwa Mtutura, aah! Nimemruka, baada ya Mheshimiwa Fred ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. FRED M. TUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuweza kuamua kwamba sekta ya miundombinu iwe mionganini mwa sekta nyingine muhimu ambazo zimepewa kipaumbele katika bajeti hii ikiwemo Sekta ya Maji, Sekta ya Afya na Sekta ya Elimu. Naipongeza Serikali sana kwa uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani ambazo zimeendelea ziliweza kupiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo baada ya kuamua kuweka mkazo mkubwa sana kwa makusudi kuimarisha miundombinu yake. Kuimarika kwa miundombinu kwa nchi yoyote ile kunachochea sekta nyingine kukua kwa haraka na uchumi wa nchi unaweza kukua kwa haraka kutokana na kuimarika kwa miundombinu katika nchi yoyote iliyopo hapa duniani.

Mheshimiwa Spika upo umuhimu mkubwa sana kwa Serikali yetu kuendelea kuweka fedha za kutosha katika sekta ya miundombinu ili sekta hii iweze kuchochoea uchumi wa nchi yetu, hayo ni maoni yangu na nadhani ni maoni ya Watanzania ambao sio wachache.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie bajeti iliyowekwa mbele yetu ambayo tunaijadili na nieleze tatizo ambalo nimeliona na limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini na mimi naomba nizungumze kwa upande wangu.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo hapa nchini yamepewa upendeleo mkubwa sana, unaweza ukakuta yana miradi miwili mitatu, kuna ujenzi wa barabara na kuna ujenzi wa madaraja na kuna maeneo mengine hayakutendewa haki kabisa. Naomba nieleze maeneo ambayo hayakutendewa haki na nitoe mfano wa Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete mwaka 2007, Mei alipokuwa anatembelea Shinyanga, aliwahakikishia wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kwamba ahadi zilizotolewa na CCM wakati wa kampeni mwaka 2005 zitatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya ahadi hizo ni ujenzi wa barabara inayotoka Mwigumbi mpaka Maswa kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami na barabara nyingine ya kutoka Kolandoto kwenda mpaka Meatu kupitia Mhunze na yenewe aliwahakikishia wananchi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati Rais wetu alipokuwa anazindua mradi wa maji kule Shinyanga Mei thelathini na moja mwaka huu, aliendelea kuwasisitizia wananchi na akasema kwamba angependelea sana wakati atakapokwenda tena Shinyanga mapema mwezi Agosti, mwaka huu aweze kuweka jiwe la msingi kwa kuanza ujenzi wa barabara hizo mbili kubwa.

Mheshimiwa Spika, aliacha wananchi wa Mkoa wa Shinyanga wakiwa na shauku kubwa kwamba barabara hizo zitajengwa. Naomba niseme kwa masikitiko makubwa sana kwamba ukisoma katika bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na ahadi za Rais Mtukufu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais anayeheshimika duniani na anayependwa na Watanzania wengi, ahadi hizo hazijatengewa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wametenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya barabara ya kutoka Mwigumbi mpaka Maswa, kwa hesabu za sasa za ujenzi wa barabara Shilingi bilioni moja inajenga kilomita moja, sasa unamtaka Rais ahadi alizozitoa ni kwa ajili ya kilomita moja?

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo ambayo nimeyaona ambapo wakati kuna maeneo yametengewa miradi miwili, mitatu, sitaki kutaja kwa sababu tutaleta ugomvi usio na maana, lakini kuna maeneo kama Shinyanga tumetengewa kilomita mbili za lami. Kinachouma zaidi ni kwamba Mkoa wa Shinyanga ni moja ya Mikoa tajiri, una pamba, una dhahabu, una almasi, una ng'ombe na idadi ya watu ni kubwa kuliko Mikoa yote Tanzania. Ni Mikoa tajiri, lakini watu wake ni maskini kwa sababu ya miundombinu na suala hili litaendelea mpaka lini? Wakati maeneo mengine miradi inajirudia, sisi tunaambiwa tuendelee kuvuta subira. Nafikiri tumefika mahali kusema inatosha.

Mheshimiwa Spika, kinachouma zaidi, katika uchaguzi wa mwaka 2005 Mkoa wa Shinyanga ulikuwa Mkoa wa pili katika kutoa kura nyingi kwa Chama cha Mapinduzi na kwa Rais lakini ndio tunapewa kilomita mbili. Hii sio haki hata kidogo! Haki ya maendeleo ni kipimo kizuri cha kuheshimu haki nyingine za binadamu. Serikali inapoonekana kuegemea maeneo mengine na kuyaacha maeneo mengine, sio kutenda haki ni ukiukwaji wa haki za binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati na ninaomba warekebishe bajeti yao wazingatie ahadi ya Rais aliyoitoa, wazingatie ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, wazingatie wananchi wa Mkoa wa Shinyanga wanavyochangia katika pato la Taifa, warekebishe na watupe kiasi cha fedha kinachoweza kujenga hata kilomita kumi kutoka Mwigumbi mpaka Maswa na barabara ya kutoka Kolandoto mpaka Meatu kupitia Munze na yenewe ipewe fedha. Tuna haki sawa na Watanzania wengine ambao

wananufaika na utajiri wa nchi hii na hapo hapo sisi ndio tunachangia zaidi kuliko Watanzania wengine. Tunaomba hilo lizingatiwe sana na sitaunga mkono hoja hii mpaka nione kimeeleweka katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Shirika la Reli na hususan ukodishwaji wa Shirika hili kwa Kampuni ya *RITES*. Ukiangalia Bajeti zimetengwa Sh. 562,000,000/= kwa ajili ya Shirika la Reli ambalo lilikodishwa kwa kampuni ya *RITES*, lengo ni kulinusuru Shirika hili ili waweze kulipa mishahara. Lakini fedha nyingi zinakwenda kwa Menejimenti na taarifa zilizopo, mishahara mikubwa zaidi ni ya Wahindi. Inakuwaje wakati Shirika hili kabla halijakodishwa kwa *RITES* lilikuwa linafanya kazi vizuri zaidi, lakini kwa sasa huduma zake ni mbovu, hawawezi kulipa mishahara.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ielete ni mpaka lini kodi za Watanzania ziendelee kulipia Wahindi ambao walikuja kama wawekezaji na wameshindwa kuwekeza, wanashindwa hata kulipa mishahara, hivi sisi Watanzania ni nani aliyetuloga? Haiwezekani! Naomba Serikali kwa dhati ituelete ni vipi tuendelee kulipa na kodi zetu zitumike kwa watu ambao wameshindwa kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kwamba, sambamba na *RITES* na *TICTS*, imezungumzwa na Mheshimiwa Lembeli kwambani vyema *TICTS* wafunge mizigo waondoke, lakini vile vile waliohusika na mikataba hii wataendelea kuheshimika mpaka lini hapa nchini? Wapo, kwanini wasichukuliwe hatua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni rahisi sana kuuzunguka mbuyu, lakini ni kazi nzito sana kuukumbatia mbuyu huo. Kuukabili ukweli ni kazi nzito, lakini ni lazima uukabili, ukiuzunguka unaona unafanya kitu cha unafuu sana. Nilitoa mfano wa mtu mmoja aliyekuwa amehukumiwa kwa makosa aliyoafanya akapewa adhabu tatu achague, ya kwanza amnyweshe sumu mwanae, pili amuue mkewe na tatu anywe pombe. Yule mtu kwa haraka alichagua kunywa pombe. Alipomaliza kunywa pombe akamuua mkewe na akamnywesha sumu mwanae akaishia jambo aliloliogopa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaogopa kuchukua hatua thabiti kwa ufisadi unaotendeka hapa nchini. Vurugu zinazotokea duniani kote hazisababishwi na wananchi, zinasababishwa na viongozi ambao nafasi wanazozipata wanazitumia kwa manufaa yao na marafiki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vyema basi Serikali ichukue hatua kwa mafisadi ambao wametufikisha mahali hapa, katika ufisadi wa *RITES*, *TICTS* na kwingineko. Awamu ya tatu inahusika sana na Rais mstaafu anatajwa katika kashfa nyingi, hakuna sababu ya Serikali kumsemea Rais Mstaafu, anatakiwa yeye asimame mbele ya Watanzania awaeleze kwa nini Serikali yake ya awamu ya tatu imegumbikwa na ufisadi mkubwa. Hakuna sababu ya Serikali kumsemea, kazi ya Serikali ni kutekeleza programu zinazopitishwa na Bunge, Mahakama ndiyo inaweza ikaamua kwamba ni mwadilifu au siyo mwadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme wazi kwamba namheshimu sana Waziri Mkuu, lakini nakwenda kinyume naye kwa kusema kwamba Rais Mkapa ni mwadilifu asiguswe, hapana. Kuna tuhuma zinazomgusa katika maeneo mengi na Mahakama ni muhimili ambao upo kwa ajili ya kuamua kwamba ni haki au sio haki, ajitetee mbele ya Watanzania na Serikali kazi yake ni kuweka utaratibu wa yeze kusimama mbele ya Watanzania sio kumtetea. Aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu akayaseme Mahakamani wakati Mkapa yupo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kama inataka kuwatetea mafisadi iwatetee wote. Kuna Watanzania wako Mahakamani kwa ajili ya shutuma au kutuhumiwa kwa kufuja madaraka lakini hawatetewi na Serikali na walikuwa katika Serikali ya awamu ya tatu, iweje Serikali imtetee mmoja kati ya watu wengi amba wanatuhumiwa?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wajibu wa kuweka mazingira ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa kufikishwa katika vyombo vyia sheria, ajitetee mwenyewe kwa sababu yupo.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono baada ya hayo kujibiwa. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa namna ya pekee nikushukuru sana hasa kwa kuzingatia jinsia na kunipatia fursa hii muhimu ili niweze kuchangia hotuba ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii ili tuweze kujadili. Moja kwa moja niende kwenye mchango wangu ambaa ninaanza na barabara zetu za Mkoa wa Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Tabora umekuwa ni Mkoa maskini sana kwa miaka yote ndani ya miaka 48 ya Uhuru kwa sababu ya kushindwa kuunganishwa na angalau barabara moja tu ya lami. Pande zote za Mkoa wa Tabora Kusini, Kaskazini, Magharibi na Mashariki hatujuunganishwa na lami. Tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu sana uchumi wa Mkoa wa Tabora unashindwa kupanda kwa sababu hakuna barabara hata za kusafirisha mazao ambayo yanalimwa vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wanashindwa kufika Tabora kuja kuwekeza kwa sababu hakuna barabara. Ni kilio cha muda mrefu sana. Tunaomba sana Bunge hili leo jioni Mheshimiwa Waziri atuambie kabisa kwamba barabara itokayo Nzega kwenda Tabora bajeti yake imetengwa kiasi gani na ujenzi unaanza lini? Barabara ya kuanzia Tabora - Kaliua kwenda mpaka Kigoma ujenzi unaanza lini? Barabara ya Tabora - Itigi - Manyoni inaanza lini? Barabara hizi bila kufunguliwa Mkoa wa Tabora utaendelea kuwa maskini siku zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndani ya Mkoa wa Tabora pia ziko barabara ambazo ni muhimu sana lakini bado Serikali hajatoa kipaumbele wala kuzipa umuhimu barabara hizi. Ipo barabara inayoanzia Urambo inakwenda mpaka Mwongozo – Uyoa – Kashishi – Ichema mpaka mgodi wa Bulyanhulu. Barabara hii ni muhimu sana, kwanza mazao mengi ya chakula yanalinwa maeneo ya Uyowa na jinsi ya kusafirishwa mpaka yaje Wilayani ni matatizo. Vyakula vingi sana vinalimwa kule, lakini wananchi wa maeneo yale bado ni maskini kwa sababu hawawezi kusafiri kuja Urambo kwa ajili ya kufanya shughuli zao ndogo ndogo kwa ajili ya kuleta mazao yao. Mwaka jana nilizungumza na Naibu Waziri Mheshimiwa Makongoro wakati huo na alinisikiliza na Serikali iliahidi kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika, mwaka jana walipitisha greda peke yake, matokeo yake badala ya barabara kushindiliwa wametengeneza mabwawa. Kwa hiyo, barabara yote imekuwa ni mabwawa matupu kuanzia mwanzo. Haipitiki! Mvua ikinyesha barabara imekuwa ni bahari, watu wanaogelea badala ya kutembea. Tatizo la wananchi wale limeendelea kubaki pale pale. Naiomba sasa Serikali kwa kuwa iliahidi kutengeneza kwa kiwango cha changarawe itimize ahadi yake ihakikishe kwamba ndani ya bajeti ya mwaka huu barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha changarawe. Pia ipo barabara nydingine inayoanzia Kaliua inakwenda mpaka Kilometra 32 mpaka 60 na Mheshimiwa Spika unaifahamu ni Kilomita nyngi sana. Halmashauri haina uwezo wa kuweza kutengeneza barabara hii hata kidogo na nimeshalizungumza kidogo hapa.

Mheshimiwa Spika, nimeshalizungumza hapa Bungeni Serikali ikasema kwamba Halmashauri wakae waone umuhimu wa kupandisha chati ili iweze kuingizwa kwenye Serikali Kuu. Halmashauri imeshakubaliana lakini nashangaa kwenye vitabu barabara hii haipo. Wananchi wale wanaoishi km 60 kama wako kisiwani, hawaunganishwi kabisa kufuata huduma hata ya afya ni matatizo makubwa, hata elimu ni mbali sana. Naomba Serikali ihakikishe kwamba barabara hii muhimu inaweza kupewa kipaumbele ili wananchi wale wajione kwamba pia na wao wanachangia kwenye pato la taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine unaenda kwenye masuala ya alama za barabarani. Tumekuwa na ajali nyngi hapa Tanzania lakini ajali nydingine zinasababishwa na kutokuwepo kwa alama za barabarani. Inakuaje mkandarasi anapewa kazi ya kujenga barabara na kabitih barabara hakuna alama za kuongoza? Alama hizi ni muhimu kwa ajili ya kusaidia watumiaji barabara. Anatengeneza barabara anaweka matuta hakuna hata alama ya kuonyesha hapa kuna tuta. Kwa hiyo, magari yanavamia matuta matokeo yake ndiyo ajali na watu kupoteza maisha. Ninaomba sana, nimezungumzia barabara kutoka Morogoro kuja hapa Dodoma eneo la Kongwa pale, kumewekwa matuta makubwa kweli na kila tukipita tunarukia yale matuta. Tangu Januari mwaka huu mpaka leo karibu miezi saba hakuna alama yoyote. Hata wewe unapita na Waheshimiwa Wabunge wanapita wanayaona, hakuna alama hata moja, ni kwanini mkandarasi asiambiwe aweke alama jamani? Tunasubiri mpaka ajali itokee ndiyo tuchukue hatua kwenye masuala ya msingi kama haya?

Mheshimiwa Spika, mambo kama haya yapo kwenye barabara nydingine pia. Ni tatizo! Alama inapokuwa imeondoka barabarani Serikali ione umuhimu wa kurudisha.

Tunajali maisha ya Watanzania na tunajali maisha ya wanaotumia barabara kuhakikisha kwamba alama zilizo muhimu kwa ajili ya kuongoza watumiaji ni muhimu zikawepo ili kuhakikisha kwamba tunapunguza ajali kwa kuzingatia alama za barabarani na kuangalia barabara zetu zinakuwa katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la wakandarasi. Tumekuwa na tatizo la kuwa na wakandarasi wabovu sana kwa maeneo mengi kwenye utengenezaji wa barabara zetu. Tunatangaza tenda, tunapata zabuni, tunapata wakandarasi lakini tumekuwa tunashuhudia wakandarasi wengi amba o hawana uwezo.

Kwanza, wanachukua muda mrefu kutengeneza barabara; pili, barabara zenyewe zinakuwa hazina viwango, kwa muda mfupi barabara imeshaanza kuharibika. Wakandarasi hawa wakati wanakabidhi barabara hakuna *guarantee* ya muda fulani? Inakuaje barabara inakabidhiwa ndani ya muda mfupi inakuwa na mashimo! Inakuwa ni kazi ya kukarabati kila siku! Kwa hiyo, kazi ya kukarabati haiishi. Tuna *resources* chache sana. Ili tuweze kutumia vizuri *resources* zetu tuhakikishe tunapata watu amba o ni makini. (Makandarasi makini)

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa Serkali kwa kuwa sasa hivi tunatambua mkandarasi huyu ni mzuri, huyu sio mzuri, badala ya kuwa na *tender* kutangaza kila siku ambayo pia na yenye we inachangia rushwa. Serikali itambue wakandarasi amba o ni wazuri wanaofanya kazi kwa ufanisi tuwatambue na tuwe tunawapa *tender*, tuwe tunawapa kazi ya kutengeneza barabara. Tuachane na utaratibu wa kutangaza *tender*. Kwa hiyo, kwa kutumia utaratibu huu tutakuwa tume pata wakandarasi wazuri na tutakuwa na barabara bora ambazo zitatumika kwa muda mrefu na hivyo kuweza kusaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa Dodoma hapa mimi naishi *Area C*. Barabara ambayo inatoka eneo la *NAM Hotel* kwenda mpaka kwenye nyumba za *CDA* ile ni barabara ya ndani. Kwa kweli barabara ile magari yanakwenda *speed* ambayo ni kubwa sana. Hakuna tuta hata moja, kila leo watoto wanagongwa pale wanakoswakoswa na magari.

Kwa muda amba o nimekaa pale Karibu kila mwaka mtoto anagongwa. Nimeongea na Mheshimiwa Waziri tangu mwaka juzi, bado haijawekwa matuta. Pale ni makazi ya watu, magari yanakwenda kilometra 80 hadi 90 tunahatarisha maisha ya watoto wetu kila leo mpaka tunaogopa hata kuja na watoto kwa sababu ukiwa Bungeni huna amani. Naiomba sana Serikali iiangalie barabara ile, iwekwe matuta kwa ajili ya usalama wa wototo kwa sababu ile ni barabara inayopita katikati ya makazi ya watu na sio *high way*. Hivyo magari yaweze kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye Shirika letu la *TRA*. Mimi kwanza nakwenda kinyume kabisa na Serikali kwa kile kinachosema kwamba inaanda mpango wa kutafuta hela za walipa kodi kuendelea kudumbukiza tena kwenye *TRA* kwa madhumuni kwamba inaboresha huduma za *TRA*. Wabunge hapa wamezungumzia suala hili. Tatizo la *TRA* sio pesa. Tatizo ni *Management*. *Management* ni mbovu, imeshindwa

kufanya kazi. Kwa hiyo, hata tungeweka fedha kiasi gani, maadamu *Management* ni ya Wahindi ambao hawana uchungu na nchi yetu, hawawezi kuboresha ile huduma.

Mimi ninachoomba sana ni kwamba wenzangu wamechangia na wametoa ushauri mzuri ni kwanini tunaendelea kuwalea watu hawa? Tuna agenda gani ndani yake? Kwanini tusivunje mkataba huu kwa ajili ya maslahi ya Watanzania? Sisi ambao tunakaa kwenye Mikoa ambayo tunategemea sana reli ndiyo tunaopata uchungu zaidi kwa sababu tunaelewa ni kwa jinsi gani wananchi wetu wanategemea reli kwa ajili ya kujisaidia.

Mwaka huu tumekuja na Agenda ya Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza kwa Mikoa ya Tabora na Kigoma bila ya reli kuwa na uhakika hata zana za kilimo zitachelewa. Hata mazao yanayolimwa hayawezi kusafirishwa kwenda mijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana, *TRA* imeshindwa kazi, hawana nia nzuri na sisi, mkataba uvunjwe kwa ajili ya manufaa ya Tanzania kwa sababu sisi ndio wenye nchi hii ni lazima tupigane kwa nguvu zote tuhakikishe kwamba wananchi wetu wananaufaika.

Mheshimiwa Spika ninakwenda kwenye suala moja dogo sana la kumalizia. Kule Urambo Kaliua kuna tatizo. Wapo wananchi ambao walibomolewa nyumba zao tangu mwaka 2003 ili wapishe barabara. Lakini cha kusikitisha, mpaka leo wananchi wale hawajawahi kulipwa chochote. Sheria iko wazi kwamba kama Serikali inaanua kubadilisha matumizi yoyote ya ardhi wakati mwananchi alitangulia kukaa pale, mwananchi huyo analipwa haki zake.

Kwanza viongozi/watendaji walitumia ubabe kwa kuwabomolea nyumba wananchi wale bila hata kuhamisha chochote, wengine waliendelea kubaki maskini mpaka leo na wengine walipoteza maisha. Tangu nimeingia Bungeni nashughulikia suala hili lakini kuna vikwazo na vikwazo hivi vinaletwa kwa sababu ya wale waliosababisha wananchi hawa kupoteza haki zao ndiyo wanaendelea kushinikiza Serikali isiwalipe. Wananchi hawa ni wananchi wa Tanzania, wote wanastahili ya msingi, ninaomba sana wananchi wa Kaliula zaidi ya 23 ambao walibomolewa nyumba zao hawakulipwa hata shilingi wameendelea kunyanyasika mpaka leo, walipwe haki zao kwa sababu waliitii Serikali lakini hawakutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika, kanuni ya 68.

Mheshimiwa Spika, naomba leo niwe wa kwanza kusema, utupe mwongozo. Mimi naanza kuona Bunge hili sasa kwa lugha yenyewe kwamba limeanzisha jihadi na Rais Mkapa. Ningombaa utusaidie wale wote wenye ushahidi kuhusu Rais Mkapa waulete hapa ili kama ni kuundwa Tume iundwe *once and for all*. Haiwezekani kila siku mtu akisimama ni Rais Mkapa, ni nchi gani duniani! Naomba sana leo utusaidie, wale wote ambao wanaamini Rais Mkapa ameiibia nchi hii, walete ushahidi hapa, kama ni

Tume iundwe ichunguzwe, tutangaze duniani. *Otherwise hatueleweki kwa mataifa. Juzi nilikuwa Marekani, naomba nitoe mfano huu, mtu mmoja akamwuliza swali Rais Obama kuhusu kuanguka kwa uchumi duniani akasema tunamfanyaje Rais Bush? Akasema habari ya Rais Bush is over, it is our time to fix the economy and go for front.*

Sisi tunaamua tuishi *in the past*. Naomba utusaidie wale wote wenye uchungu na nchi hii watuletee ushahidi huu tuufanyie kazi tumalize. Hatuwezi miaka mitano tunaongea habari ya Mkapa! Wengine tumechoka! (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nazielewa hisia zako na heshima kubwa tulinayo kwa kiongozi wetu huyo wa awamu ya tatu. Lakini mamlaka ya kuwazuia Wabunge humu ndani, wakiwa ndani wasiongelee yale ambayo wanayajua na suala la kuleta ushahidi hapa sivyo, hatupokei ushahidi hapa. Labda mtu alete hoja mahususi. Kama akileta hoja mahususi kama ambavyo wengine walitaka kuleta, hiyo ndiyo. Lakini huwezi kujiletea tu ushahidi.

Mimi nadhani wanaoongelea hilo siyo wengi kiasi hicho. Kwa mfano leo wote walioongea ni mmoja tu ndiyo amesemasema vitu hivyo. Kwa hiyo, nasikitika sina mamlaka ya kuzuia Bunge kumzungumza kiongozi yeoyote, kwa maana ya mambo ambayo yametokea. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi.

MHE. MUSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nikuombe radhi wewe na Wabunge wengine wakati uliponiita nilikuwa msalani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na timu yake, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa bajeti hii ngumu ambayo imeleta maneno mengi kwa Wabunge ambao wanadai barabara katika maeneo yao na wanayo haki hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza na Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoitoa jana, tunaomba viongozi wa Bunge na watu wa Tarime waache haya mambo ambayo hayana msingi na wajenge Mkoa wao, familia zao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kuna mazungumzo yamezungumzwa na hasa nilianza mimi kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu suala la wakazi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila. Mimi nimewatembelea wakazi wale, wanaishi katika mazingira magumu kwa zaidi miaka 13. Nimeambiwa kuna maamuzi tayari yamefanywa ya kulipwa fidia na nimeambiwa kuna baadhi ya watu wanashubiri fidia, kama hawakulipwa fidia na wao watakasirika.

Mheshimiwa Spika, lakini hawa watu waelewe, kwanza makazi mapya sasa hivi kwa fidia watakayolipwa itawawia vigumu sana. Lakini hoja yangu ya msingi ni kuwa gharama ya fidia hii na gharama ya fidia itakayolipwa kwa hawa wenye mashamba kuwapa viwanja wananchi hawa wa Kipunguni ni kubwa mno na inaweza kujenga uwanja mwingine kwa eneo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja zangu zilikuwa tatu gharama na ukitazama eneo ambalo linalengwa sasa hivi la Kipunguni, Kigilagila na Kipawa. Kwa miaka inayokuja eneo hili ni dogo mno. Lakini hivi nchi gani leo inajenga uwanja mpya mjini? Viwanja vyote havijengwi mjini na nchi zote ukienda viwanja vinajengwa kilomita 60, 70 nje ya miji. Kwa mfano Dubai, wana maeneo madogo sana! Sasa walishauacha wanajenga Jebeally. Kama huna taarifa hizo zijue. Wanajenga Jebeally uwanja mkubwa sana kwa sababu kufanya ndege zi-*approach* katikati ya Miji nayo ina athari zake.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza juzi kuhusu suala la Serikali Kuu kutunyang'anya miradi yetu Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Meya wa Jiji Adamu Kihimbisa pamoja na Madiwani wa Jiji wote tulikuwa katika mkakati wa kutaka kujenga barabara ya Tegeta kwenda Mwenge. *Two lines*, huku mbili, huku mbili kwa mradi wa Oreti, hawa ni Waholanzi. Katika *process* ya kutaka kukubaliana nao masharti waliyotoa asilimia 50 ya mradi *grand bure*, asilimia 50 ya mradi itakuwa kwenye *export credit* kwa maana watumiaji wa barabara ile ndio watakaolipia mradi ule. Kwa mahesabu yaliyopigwa kila siku barabara ile inapitiwa na magari takribani 20,000. Kwa hesabu walizopiga wenyewe wahisani waliona kipindi cha miaka mitatu watarudisha faida zao kwa kupata sio chini ya Shilingi bilioni 60. Mradi huu umeyeyuka! Haukuyeyuka kwa sababu tulishindwa kupatana na hawa watu wa Oreti, uliyeyuka kwa sababu Serikali Kuu waliuteka huo mradi. Wameukimbilia, wameukumbatia na wameshindwa kuutekeleza, matokeo yake msongamano unazidi katika barabara ile na hasa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na mradi wa *DAT* ambao ulianzishwa na Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam nao vile vile umetekwa na Serikali na mpaka sasa unavyoona bado unayumbayumba tu.

Mheshimiwa Spika, huko ninakolenga nina hoja yangu ya msingi. Wabunge wote wanalamika kuhusu barabara zao kwa sababu bado Serikali inataka ijenge yenewe. Serikali uwezo wake wa kujenga barabara hizi ni mdogo sana. Nchi nyingi sasa hivi, barabara zinajengwa na watu halafu watumiaji wa barabara wanalipia ile barabara kwa muda hata wa miaka 20 na huu ndio mpango ambao Serikali inatakiwa sasa hivi wauchukue. Hivi nani atajisikia vibaya kutoka Dodoma aende Nzega, gharama ya kulipia Sh. 15,000/= mpaka Sh. 20,000/= *road toll* ya barabara hiyo ili afike mapema gharama ya *petrol* inashuka pamoja na vipuli ambavyo anabadilisha mara tatu kwa mwaka sasa atakuwa anabadilisha kwa kipindi cha miaka mitano? Mimi naiomba Serikali, watalaam tunao na ni wazuri sana. Hebu jaribuni ku-*scout idea* kama hizi za kuwa na *road toll* ili barabara zetu zitengenezwe. Huu ndio mfumo wa dunia nzima ambao sasa hivi unatumika. Gharama ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, basi la kawaida au gari la kawaida kuna taabu gani kulipia Sh. 15,000/= kwa kila mwendo ili kuisadia Serikali iweze kuwa na mfuko wa kutengeneza barabara nyingine? Kwa mfuko huu wa Serikali peke yake hauwezi.

Lakini mipango yote hii ikipelekwa, hakuna maamuzi kwa sababu wanaojadili ni watu zaidi ya 50 na kila mmoja anakuja na tamaa yake na kila mmoja anakuja na fikra zake. Barabara hii ya Tegeta - Mwenge alijitokeza mtu akaandika kwenye faili kwa nini barabara hii ilipiwe, barabara nyingine bure? Lazima tubadilike! Ndio nilisema juzi, tuwe

na *mind setting* nyingine ili tuweze kujenga miji yetu, kujenga barabara zetu. Ni lazima Serikali sasa itazame suala la *road toll*. Sio lazima kupata wawekezaji kutoka nje. Mifuko yetu ya pensheni inaweza ikajenga barabara ile ya Tegeta kwa miaka mitatu wakarudisha faida yao zao kwa mara tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na hasa namshukuru Katibu Mkuu kwa hoja yetu ya Barabara ya Uhuru. Barabara ya Uhuru ina *sentiment* ya nchi hii, ni barabara ambayo ndio Mwalimu alipita ya kwanza alivyotoka *UNO*. Hali ya barabara hii inasikitisha sana. Haipo katika mpango wa Serikali Kuu. Lakini tumepiga debe sana humu ndani, sasa Katibu Mkuu na Mheshimiwa Waziri wametukubalia, tumepata mita 800, sio mbaya *Alhamdulillah* nashukuru. *Point 0.8* ya kilomita tunashukuru na tutajua wapi tutaipanga na najua mwakani watatuweka tena kwenye program na mpaka tutakamilisha zile kilomita zote 4.5 ili barabara ile ipate heshima ya kitaifa na Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku hizi hata Mheshimiwa Waziri Mkuu simwoni kupita barabara ya Uhuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu ilitakiwa uwe unapitapita na wao waogope waitengeneze maana siku hizi ukipitapita ndiyo zinatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali, vile vile tuna matatizo makubwa sana. Mfereji wa Bungoni na kila kukiwa na mvua wananchi wanakaa wiki mbili ndani ya maji huduma zao za kijamii zote zinashindikana. Lakini baada ya kulipigia debe Serikali Kuu imetupa Sh. 2,300,000,000/=, ni hatua kubwa sana. Naipongeza Serikali kwa msaada wake kwa kutazama mfereji huu na kuweza kutengeneza na wanaweka daraja pale kwa Malapa, lile daraja ambalo huwa mnalionia litakuwa linapita barabara nne. Huku mbili, huku mbili, nikiunganisha na hizi mita 800 Ubunge mwakani hakuna shida. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nazungumza matuta ya barabara ya Kawawa. Barabara ya Kawawa inaua sana watoto. Watoto wadogo, kwa watu wazima wanafariki! Yote hayo ni kwa sababu mtu anataka kuwahi kwenda nyumbani kwake, lakini wanauawa watu ambaeo hawana hatia. Tumezungumza na *TANROAD* wanasema inaharibu barabara. Hii barabara ya Dodoma ina *highway* na bado ina matuta. Rais wakati anaweka jiwe la msingi la barabara ya Kilwa alitoa agizo. Barabara ya Kilwa na barabara nyingine zote ziwekewe matuta ili kupunguza ajali kwa sababu tumeshindwa kudhibiti madereva, sasa sisi tuwadhibiti mwendo wao. Watu ambaeo wanaona wanachelewa kwenda kwao waone kero wanazopata watu wanavyokufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu suala hilo ili alitazame ili watuwekee matuta kwenye barabara hiyo. Kuna sheria tumepitisha kwamba ni marufuku kwa gari iliyoharibika barabarani kuwekwa miti na majani. Hii barabara ya Dodoma imejaa majani barabarani, imejaan miti na inaongeza hatari za ajali kuwaumiza wanaoendesha na huyo aliyepaki gari pembeni. Tunaomba wanaohusika wajaribu kulidhibiti suala hili. Naomba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote pamoja na mimi ambaeo tunapita barabara hii tujaribu kuelimisha wananchi kwamba barabara siyo *sitting room*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamalizia Msemaji wa mwisho kwa mchana huu lakini pia ndiyo wa mwisho kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana hususan kwa maamuzi yako ya kuongeza muda ambao umeniwezesha na mimi kupata nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naanza kwanza kwa pongezi na shukrani kwa yale mazuri yaliyofanyika kitaifa na kwenye Jimbo langu. Naongea hapa kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini. Kwanza niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzito wanayofanya ambayo aliwasilisha, tunayo hapa. Tunaipongeza na kuikosoa, hii ni sehemu ya kazi. Kwa hiyo, hata pale ambapo hatuungi mkono sio kwa sababu hatuitaki, ila ni kwa sababu tunataka maboresho zaidi. (*Makofi*)

Naipongeza tena Serikali kwa barabara kuu inayopita Mjini Shinyanga ambayo ni takribani kilomita 25 sasa ni ya lami kupitia Kolandoto, pia kuna kilomita nne za barabara kuu inayopita *Old Shinyanga* zimejengwa kwa kiwango cha lami, ndani yake kuna daraja la Ning'wa ambalo linajengwa la kisasa. Pia nashukuru sana kwa mchakato unaoendelea wa Serikali wa upanuzi wa uwanja wa ndege wa Shinyanga.

Pia nashukuru sana kuendeleza mradi wa ujenzi wa barabara muhimu kwa kiwango cha lami nchini. Mwisho, katika shukrani ni kuitambua na kuipa hadhi ya barabara kuu barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanuhuzi – Sibiti - Matala mpaka Odeani. Nafahamu Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alishaahidi barabara hii kutokea Kolandoto mpaka Mwanuhuzi ndani ya miaka hii mitano ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, bahati mbaya sijaona hapa. Lakini ndiyo maana wakati mwingine tunasimama na kusema siungi mkono hoja mpaka kwanza nipate ufanuzi. Sasa na mimi nauliza, ingawaje sijasema siungi mkono, hii barabara imepotelea wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni ushauri. ukiangalia mpango wa ujenzi wa barabara nchini, unapata kishawishi kuwa hakuna mpango mkakati na ndiyo maana kuna kelele nyingi sana kwa sababu kama leo hii tungekuwa na mpango kabambe na unaotekelawa Mikoa yetu yote itakapofikia miaka 50 ya Uhuru itakuwa imeunganishwa kwa barabara za kiwango cha lami. Lakini hii haitafanyika kwa sababu ukiangalia mpango hamna. Kwa hiyo, nashawishika kudhani kwamba hakuna mpango.

Lakini la pili, ningependa kuelezw, hivi gharama za ujenzi wa barabara za lami hapa nchini hususan barabara kuu, zina gharama kiasi gani kwa kilomita moja na tunajilinganishaje na nchi nyingine hususan nchi jirani ili tusije tukajikuta sisi tunatumia hela nyingi sana kujenga barabara za lami bila sababu au kwa makusudi ya watu wengine kujitajirisha?

Mheshimiwa Spika, lakini pia swalí lingine ni kwamba, nini kiini cha ujenzi wa barabara hafifu za lami? Ndani ya mwaka mmoja au ndani ya kipindi hicho kinachojengwa unakuta barabara huko ilikoanza kujengwa ya lami barabara imeanza kubomoka. Sasa unajiuliza, nani wa kulaumiwa hapa? Mkandarasi au chombo kinachosimamia? Sasa mimi najua wakati mwengine ni siri. Siri iko hivi; huyu ni mkandarasi mzuri, lakini na fedha uliyoitenga ni hii hapa, lakini unafuata tena nyuma unataka unywe naye soda, unataka ule naye chakula, wewe unatarajia nini mwishoni? Tuwaache wakandarasi wafanye kazi bila kuwaingilia. Kama kuna 10%, hiyo ni rushwa, tuiache. Mwisho wa siku tukiacha, maana nadhani inafanyika kwa sababu kama ingekuwa haifanyiki haiwezekani barabara kuu ya lami ndani ya mwaka mmoja imeshaanza kupata mashimo. Haiwezekani! Kwa hiyo, tunashawishika kusema kwamba dosari ipo, siyo mkandarasi ila ni sisi wenyewe, yaani vyombo vinavyosimamia. (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wowote wa barabara ya lami una hatua za upembezi yakinifu, usanifu na hatimaye ujenzi wenyewe. Lakini sasa unajiuliza, hivi mbona hadi leo hii miji yetu ya Sumbawanga, Kigoma, Tabora, Kagera haijaunganishwa kwenye mtandao wa barabara za lami? Kwa nini? Kwa nini Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Kigoma, Mara, Kagera hadi leo hii ambazo kiuchumi, asilimia zaidi ya 50 ya uchumi wa Tanzania unatoka eneo lile, kwa nini leo hii inakuwa haijaunganishwa kwenye barabara za lami? Lazima kuna hitilafu kwenye mipango. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wewe tumefanya kazi, nakufahamu, ni makini sana. Lakini mwisho wa siku ndugu yangu sisi viongozi tunapimwa kwa matokeo ya kazi na siyo vinginevyo. Siyo kwa maneno, ni kwa matokeo ya kazi na kazi hiyo inaanza kwenye mipango jinsi tunavyoionyesha hapa. Sasa sikulaumu sana wewe kwa sababu una mwaka mmoja tu. Sasa kule Ingunge wengi kabisa, ukiendelea na ule upole upole wako ule utaingizwa mjini. (*Makofí*)

Hebu tuangalie mipango yetu. Barabara inayokwenda kwenye chimbuko la uchumi kwa nini ijengwe miaka sita? Kutokea Dodoma kwenda Singida miaka sita! Lazima tuna hitilafu katika mipango yetu. Kwa nini hii barabara (niongezee na mimi) ya kutoka Tunduma mpaka Arusha ambayo inaitwa *Great North Road* hadi leo hii haina lami wakati eneo hili la Kusini wanazalisha chakula cha kutosha kama mahindi? Leo Arusha, Kilimanjaro na Manyara wana upungufu wa mahindi, lakini ni lazima wazunguke njia ya Chalinze kilomita zaidi ya 1000 kuyapeleka hayo mahindi. Lazima tuna hitilafu kwenye mipango na ni lazima tuseme kwamba tuna hitilafu hii kusudi tuweze kusahihisha. (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kagoma – Lusahunga miaka mitatu kwa mipango jinsi ilivyo haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, mimi ningedhani barabara ya Itigi – Tabora – Kigoma badala ya kwenda kwa vipande vipande unaichukua kama *block* moja na fedha ikianza kujengwa wakandarasi hata watano kwa wakati mmoja wanaanza kazi, hapo ndipo *you are a strategic planner*, wewe unajua mipango. Mimi sizungumzii Shinyanga peke yake, maana ninazungumzia *in a strategic way* katika nchi yetu. Mimi huwa sipendi

kuzungumza *Kisw angl*ish lakini leo nimeona nizungumze *Kisw angl*ish kwa sababu ya kujaribu kuonyesha msisitizo wa aina fulani.

Mheshimiwa Spika, mwisho naongelea uwanja wa ndege wa Shinyanga. Uwanja huu ni mlango wa pili mkubwa sana katika utalii wa maeneo ya Ngorongoro na Serengeti. Maana leo Serengeti na Ngorongoro zinapitika kutokea Arusha. Ngorongoro lazima uende kilomita 158. Serengeti mpaka Serenora kilomita 325; ukianzia Shinyanga sio zaidi ya kilomita 150 unakuwa umeshaingia Serengeti na Ngorongoro.

Ni lazima tufungue mlango wa pili ili watalii wanaoingia sasa waweze kuingia maradufu na mapato yatokanayo na utalii huo na ajira vitaongezeka zaidi ya maradufu. Tukifanya hivyo, ndiyo itakuwa *strategic plan* hiyo. Uwanja wa Ndege wa Shinyanga ndiyo mlango ukisaidiana na ule wa Mwanza, lakini ukitokea Mwanza inakuwa mbali kidogo kwenda Serengeti na Ngorongoro. Kwa hiyo, sambamba na hilo ndiyo maana Mheshimiwa Rais akasema barabara ya Kolandoto – Lalago - Mwanuhuzi ijengwe kwa kiwango cha lami. Alielewa wazi kwamba kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeshafungua mlango wa utalii kutokea Magharibi mwa Tanzania.

Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri alichukue hili ili ahakikishe kwamba Uwanja wa Ndege wa Shinyanga ambao unatajwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na jana amerudia nashukuru, aweze kujengwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme miundombinu ni uchumi, kwa hiyo, tuchangamkie ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaondoka kwenye umaskini. (*Makofi*)

Mikoa ambayo ina rasilimali nyingi kama Mkoa wa Shinyanga ni lazima uiwekee miundombinu ya barabara za lami kwa kiwango kikubwa kinachowezekana. Hatusemi Shinyanga kwa sababu sisi tunatoka Shinyanga, tunazungumza kimkakati ndiyo, Mungu aliamua iwe hivyo sasa mnataka kubadili? Almasi ziko kule; dhahabu iko kule; pamba iko kule; mpunga, kama mvua imenesha sana, Shinyanga ndiyo ya kwanza, ng'ombe, kuku wa kienyeji ndiyo ya kwanza. Sisemi kwa kujidai, nawaambia ukweli Mungu alivyoupanga. Mali hii yote ni ya Watanzania siyo ya Wasukuma peke yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumza haya ili kuonyesha umuhimu wa kupanga vizuri ili miaka 50 tunapokuwa tunasherehekea tuwe tumeshafikia kwenye hatua ambayo kweli tunaweza tukajiridhisha kuwa sisi tuna mipango mizuri na tuna uongozi bora. Vinginevyo, tutatiliwa mashaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mlingwa. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa ushirikiano wenu, umetuwezesha angalau kupata michango mingine hapo ya wachangiaji.

Waheshimiwa Wabunge, lakini ninalo tatizo ambalo napenda niwashirikishe. Tulitenga hii kanuni 99, maana yake Waziri mtoa hoja sasa amebakiwa na dakika 30

Naibu Waziri dakika 15. Lakini Waheshimiwa Wabunge kutokana na mjadala huu tukimtaka Mheshimiwa Waziri au Serikali ifuate utaratibu huo naona itakuwa shida kubwa sana kwa sababu sehemu nyingi sana zimeguswa ambazo zinaombwa ufanuzi. Kwa hiyo, nashawishika basi kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishat na Madini aitengue ile kanuni tulioitengua ili mto hoja angalau kwa hoja hii tu basi apate dakika zilizomo sasa katika kanuni ambazo ni 60 na hiyo itatuwezesha kwenda vizuri zaidi. (*Makofî*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99 (9) na kwa kuzingatia mwongozo wako naomba kutoa hoja kwamba kanuni inayoelekeza wakati wa kuhitimisha mjadala, mto hoja atumie muda wa dakika 30, sasa tuitengue na Bunge lako Tukufu liliridhie ili hatimaye apate muda wa kutosha wa dakika 60 kwa ajili ya kuwezesha kupata fursa ya kufafanua hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)
(*Bunge iliridhia kutengua kanuni za Bunge zilitungwa*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mwongozo wa Spika

SPIKA: Wewe hujasoma chochote, umeniita jina tu.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, kanuni ya 68(7), leo asubuhi Serikali hapa iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwanza juu ya uendeshaji usioridhisha wa Shirika la kampuni ya *RITES* ya India na ya pili, taarifa ya utekelezaji wa maamuzi ya Bunge juu ya utendaji wa kazi usioridhisha wa kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya manufaa ya taarifa hizi mbili kwa Taifa la Tanzania kwa uchumi wetu hata kwa wananchi pia ningombwa mwongozo wako ili Bunge lako Tukufu lipata nafasi ya kuweza kujadili taarifa hizi. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya na hivyo ndivyo tutakavyofanya. Baada ya kuwa zimewekwa Mezani Taarifa hizo ni pamoja na taarifa zitakazokuja wakati wa Wizara kwa mfano ya Nishati na Madini na taarifa itakayokuja wakati wa mjadala wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuna hoja ambazo zilikwishapitishwa na Bunge na tulikuwa tunadai taarifa. Maana ya kuziweka hapa ni kwamba sasa nazipeleka kwenye Kamati. Kama umefuatilia kwenye ratiba yetu, tarehe 30 Julai, siku nzima na pengine na nusu ya Ijumaa tarehe 31 zimepangwa kujadili taarifa sasa za Wenyeviti kadri watakavyokuwa wamezingatia taarifa hizi. Niseme tu kwamba

taarifa hizi sasa ziko wazi pia, kwa hiyo, ukiona watu wa habari wananiuliza kama wanawenza kuzizungumzia hawazuiwi kwa sababu tayari zimewekwa mezani. Ahsante sana.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 leo jioni.

(*Saa 7.32 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepokea kutoka kwa Serikali, ombi la hoja ambalo litatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Nadhani litajieleza lenyewe. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa muujibu wa Kanuni ya 69 ya Kanuni ndogo ya Kwanza, naomba kutoa hoja kwamba, mjadala wa kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, sasa uahirishwe hadi kesho tarehe 3, Julai, 2009 asubuhi baada ya kipindi cha Maswali.

Mheshimiwa Spika, leo saa saba mchana, kabla hujasitisha shughuli za Bunge, Serikali ilipokea hoja ya kusudio la kufanya mabadiliko katika matumizi ya Fungu la 98, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Ilemela.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Bunge la bajeti kukutana, katika Mkutano huu wa kumi na sita, Wizara ya Miundombinu ilikwishawasilisha mapendekezo yake kwenye Kamati ya Miundombinu iliyofanya uchambuzi wa makisio na kuyapitisha bila mabadiliko na hatimaye yakawasilishwa Bungeni. Hoja ya mabadiliko iliyowasilishwa leo na Mheshimiwa Anthony Diallo, ina mapendekezo ya mabadiliko makubwa mno ambayo kwa kiasi fulani yanabadili madhumuni ya vifungu alivyokuwa amevitaja.

Mheshimiwa Spika, hali hii bila shaka imetokana na Mheshimiwa Anthony Diallo, kutokuhudhuria vikao vya Kamati hiyo wakati ikitafakari mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii ya Miundombinu katika ngazi ya Kamati husika. Kwa kuwa Kamati ya Miundombinu ilipitisha makisio halali, bila kuzingatia mabadiliko makubwa sasa yanayopendekezwa na Mheshimiwa Anthony Diallo na kwa kuwa ni busara sasa kushirikisha Kamati katika kupitisha mabadiliko makubwa au kutafakari mabadiliko makubwa kama haya, naomba kutoa hoja kwamba sasa mjadala uahirishwe ili kutoa nafasi kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kukutana na kufikiria jambo hili. Kama ilivyo kawaida na desturi ya Bunge letu, Wabunge wengine ambaio sio Wajumbe wa Kamati hii, nao pia wataalikwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika Naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na Serikali. Ningependa kuongeza tu kwamba mimi ndio nimepeleka kwa Serikali hoja ya mabadiliko aliyoileta Mheshimiwa Diallo na tukumbuke kwamba Mheshimiwa Diallo sio Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Kwa hiyo, ye ye ameona mambo hapa ambayo anadhani yanakiuka taratibu na Sheria na kadhalika.

Kwa hiyo, rai hii ya Serikali, nadhani ni nzuri na kwa hiyo, mimi nataka kutumia mamlaka mliyonipa chini ya Kanuni ya 53(3) ambayo inasema hivi nanukuu: “*Isipokuwa kama Spika ataamua vinginevyo, kila hoja ambayo taarifa yake imekubaliwa itapelekwa kwanza kwenye Kamati inayohusika.*”

Kamati inayohusika hapa ni Kamati ya Miundombinu na kwa hiyo, baada ya maelezo ya Mheshimwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge - Sera na Uratibu na akatoa hoja ya kuahirisha Bunge hadi kesho. Kwa maana hiyo, hadi kesho saa tatu, kwa sababu ye ye anaahirisha mpaka kesho baada ya Maswali. Sasa hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Bunge liliridhia Utekelezaji wa Hoja Iliyotolewa*)

SPIKA: Kabla sijahairisha, ninayo matangazo machache. Kwanza, Waheshimiwa Wabunge, kuna mabadiliko katika ukurasa wa 184 na 194 wa Kitabu cha Nne. Kwa hiyo, nimeagiza wagawiwe ili kila mmoja awe na nakala kabla ya kuendelea na mijadala kesho kwenye makadirio ya matumizi . Alla! haya ni ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Yanahu su Miundombinu? Aah, basi haya ni mengine tunaweza kuyashughulikia kesho asubuhi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naelekeza kwamba, Kamati ya Miundombinu iende sasa hivi baada ya kuhairishwa Bunge, ikakutane ili kututatulia huu utata uliopo na kesho wataweza kutupa taarifa ya kazi zao ili tujue namna ya kuendelea. Kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho asubuhi, siku ya Ijumaa saa tatu asubuhi.

(*Saa 11.07 Jioni Bunge lilihairishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 3 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)

